ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI
ZANZIBAR
MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa.

14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18. Mhe. Shawana Bukheti Hassan	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/ Jimbo la Dole
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Mpendae

30.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
31.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
32.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
33.Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais
34.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
35.Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
36.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
37. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
38.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
44.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
45.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
46.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
47.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
48.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
49.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
50.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
51.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
52.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni

53.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
54.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	Jimbo la Kiembesamaki
55.Mhe. Marina Joel Thomas	Kateuliwa na Rais
56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
57.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
58.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini
59.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad	Jimbo la Chambani
61.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
62.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali	Jimbo la Uzini
63.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
64.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
65.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
66.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
67.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
68.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
69.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
70.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
71.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
72.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
73.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
74.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
75.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake

76.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
77.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
79.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake
Ndugu Yahya Khamis Hamad	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Sita – Tarehe 23 Januari, 2013

(Kikao kilianza saa 3.00 asubuhi)

DUA

Mhe. Mwenyekiti (Mahmoud Muhammed Mussa) alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

(Mhe. Omar Ali Shehe - Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika (PAC): Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha mezani ripoti maalum ya kuchunguza na kudhibiti hesabu za serikali na mashirika, juu ya uchunguzi wa Utendaji wa Shirika la Umeme Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJI BU

Nam. 50

Kuwepo kwa mtaro wa maji machafu

Mhe. Nassor Salim Ali (Kny: Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa) - Aliuliza:-

Naomba kupewa maelezo ya mtaro wa maji machafu uliopo baina ya Block No. 5 na 10 na kuekelea msikiti mabati.

a) Je, ulijengwa kwa malengo gani na malengo hayo yametimia.

b) Je, Serikali imegharamika kiasi gani katika kujenga mtaro ule.

c) Je, Serikali ina mpango gani wa kufunika makaro ambayo mifuniko yake imevunjika au imeibiwa na kupelekea baadhi ya makaro hayo kuwa wazi na kuweza kuleta athari kwa watoto ambao wanacheza maeneo hayo.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti naomba kumjibu Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa wa Jimbo la Kikwajuni swali lake nambari 50 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:

a) Lengo la kujenga mtaro wa maji ya mvua wenye urefu wa mita 700 kutoka *block* namba 5 na *block* namba 10 kuelekea Msikiti Mabati ni kusaidia kupokea maji ya mvua yanayotokea barabara ya Michenzani na maeneo ya karibu na kuyapeleka bondeni

Kisiwandui kuelekea pwani. Malengo ya kuwepo kwa mtaro huo kwa kiasi fulani yamefikiwa kwa sababu kiwango cha kuridhisha cha maji ya mvua kwa sasa yanaingia katika mtaro huo, ingawaje ipo changamoto ya mtaro huo kuingia mchanga na uchafu mwengine, pamoja na sehemu chache ambazo kutokana na matatizo ya kiufundi kwenye ujenzi zinashindwa kuingiza maji kwenye mtaro huo.

Natoa wito kwa wananchi wanaokaa maeneo hayo kutoa ushirikiano wao katika kuweka mtaro huo kwenye hali ya usafi. Aidha naomba pia viongozi wa eneo akiwemo Mhe. Mwakilishi, Mhe. Mbunge, Madiwani, kusaidia kuwashajihisha wananchi wanaokaa katika maeneo hayo umuhimu wa kuweka hali ya usafi ndani ya mtaro huo.

Aidha serikali kwa upande wake nayo kupitia mradi wa ZUSP ambao tunatarajia wajenzi watakuwa *site* kati ya mwezi Machi na Aprili mwaka huu baada ya taratibu zote kukamilisha yale matatizo ya kiufundi yaliyojitokeza.

b) Ujenzi wa mtaro huu ulikuwa ni sehemu ya Mradi wa Michirizi wa awamu ya Pili ambapo kwa ujumla wake uligharimu serikali Euro 5, 000,00. Mradi huu wa michirizi kwa awamu ya Pili ulikuwa na ufadhili wa Serikali ya Ujerumani.

c) Baraza la Manispaa linachukua hatua ya kuyajenga upya mifuniko ya mitaro yanapovunjika au yanayoibiwa. Kipaumbele huwekwa kwa maeneo ya hatari zaidi kulingana na uwezo uliokuwepo. Aidha mawasiliano yanafanyika na mfuko wa barabara kusaidia hasa katika maeneo ya barabarani kwa mfano barabara ya Jang'ombe. Changamoto zinazotukabili ni kuongezeka kwa wizi wa mifuniko hasa ya chuma ambayo huwa inauzwa katika mkumbo wa chuma chakavu.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, mbali na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali hili la nyongeza kama ifuatavyo:

Katika majibu yake Mhe. Waziri amesema kwamba kwa kushirikiana na Mbunge na Mwakilishi wa Jimbo la Kikwajuni pamoja na manispaa je, serikali itapanga mikakati gani ya kusaidia hali ya maji yanayotuama katika maeneo yale, ili kuondoa usumbufu kwa wananchi kwa maji hasa kipindi kile cha mvua.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, mradi huu wa kuimarisha mji wetu wa Zanzibar kupitia ufadhili wa *world bank* au benki ya dunia ambayo tunaiita kwa kiufupi ZUSP, kwa kweli utahusisha matatizo yote haya ya kutuama maji au michirizi mibovu ng'ambu nakusudia mbali ya Mji mkongwe ng'ambu ninakusudia huko kwetu Kikwajuni na kwengineko mpaka Kwamtipura na kwengineko, sasa katika *plan* zetu matatizo haya kama nilivyosema ya Kikwajuni au ya Michenzani pale ambayo hayakukamilika katika ule mradi wa mwanzo, unajua ule mradi wa mwanzo tuliopata ufadhili wa Ujerumani wa SWANZA basi ule nao sasa umeletea kutokamilika kwakwe baadhi ya mambo ndio tukapata ufadhili wa mradi huu mpya wa benki ya dunia.

Kwa hivyo ni imani yetu kwamba matatizo haya aliyozungumza Mhe. Mwakilishi ya kutuama maji pamoja na Mnazimmoja yote yale yataondoka. Basi nakuomba tusubiri tushirikiane na *inshaallah* tulikwama kidogo kwenye mchakato ule wa wajenzi kupatikana. Lakini sasa mipango yote imeshakamilika *inshaallah* tukijaaliwa tutarejea Mwezi Machi, Aprili, wajenzi kama nilivyosema watakuwa *on site* na utekelezaji utaanza. Ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Waziri lakini Kikwajuni si shamba isipokuwa mwisho wa mji zamani ilikuwa Kisiwandui kwa hivyo ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Ninakushukuru kwa maelekezo yako, Kikwajuni mjini.

Nam. 54

Ucheleweshaji wa Marekebisho ya Mishahara ya Walimu Pemba

Mhe. Mohammed Haji Khalid - Aliuliza:-

Walimu kutoka Pemba wanapomaliza masomo yao kutoka ngazi moja kwenda nyengine (mfano kutoka Form VI kwenda Diploma) wanacheleweshewa sana kufanyiwa marekebisho ya mishahara yao.

Je, kuna sababu gani za msingi zinazosababisha kadhia hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 54.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba Marekebisho ya Mishahara ya baadhi ya Walimu wanaomaliza masomo yao yanachelewa. Marekebisho ya Mshahara ya Mfanyakazi aliyemaliza masomo yanafanywa kwa kufuata utaratibu ufuatao:-

a) Mfanyakazi awasilishe maombi ya Marekebisho ya Mshahara kwa Katibu Mkuu akiambatanisha na vyeti alivyohitimu mafunzo.

b) Baada ya vyeti hivyo kupokelewa na kuhakikiwa, Wizara inamwandikia Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kuomba mfanyakazi husika afanyiwe Marekebisho ya Mshahara wake.

c) Baada ya Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kuridhika na taarifa zilizowasilishwa kwake hutoa idhini ya marekebisho hayo kufanyika na kuainisha kiwango cha Mshahara Mpya mfanyakazi anaostahiki kulipwa na kuamuru Marekebisho hayo ya Mshahara yaingizwe katika vocha. Hatua hizo zote zinachukua muda lakini zinasaidia katika kuhakikisha taarifa zilizotolewa ni sahihi.

Baada ya maelezo hayo, sasa napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi suali lake kama hivi ifuatavyo:-

Kuchelewa kufanyiwa marekebisho ya mishahara kwa baadhi ya walimu kumesababishwa na wao kuchelewa kuwasilisha vyeti halisi walivyotunukiwa baada ya kumaliza masomo. Tatizo hili linatokana na baadhi ya vyuo kucheleweshа utoaji wa vyeti hadi baada ya kufanyika kwa mahafali au baadhi ya wahitimu wanashindwa kuwasilisha vyeti mapema kutokana na kuwa wana madeni ya vyuo ambapo vyuo huzuia vyeti vyao hadi hapo watakapolipa deni lao. Naomba kutoa wito kwa walimu, kuhakikisha kuwa wanapoomba kufanyiwa marekebisho ya mishahara wawe na vielelezo vyote vinavyotakiwa. Kutowasilisha vyeti vya kuhitimu masomo kwa wakati ndio sababu kubwa inayosababisha kuchelewa kufanyiwa marekebisho ya mishahara yao.

Nam. 21

Tatizo la Upakuaji Mizigo Bandarini

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Shirika la Bandari Zanzibar kwa muda mrefu kumekuwepo na tatizo la upakuaji wa mizigo kutofanyika kwa wakati kutokana na ukosefu wa vitendea kazi na wakati mwengine *cranes* zinapoharibika na kusababisha meli za mizigo kushindwa kushusha makontena kwa wakati.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuondoa matatizo hayo.

(b) Kwa kuwa Bandari hivi sasa zinakabiliwa na ushindani mkubwa. Kasoro hizo zinaondolewa vipi ili bandari ya Zanzibar iweze kuingia kwenye ushindani na kuweza kufikia malengo ya kuwa Kituo cha Biashara Afrika Mashariki.

(c) Kwa kuwa matatizo ya *cranes* za kunyanyua mizigo yamekuwa ya kawaida licha ya kununuliwa mashine mpya kwa gharama ya fedha nyingi lakini faida yake haionekani; Je, Wizara ina mpango gani juu ya hili.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti**,** kabla ya yote naomba nichukue nafasi hii kuomba radhi kidogo katika majibu yetu ya nyongeza ya juzi wakati tunamjibu Mhe. Mbarouk Wadi Mussa katika majibu yetu tulikosea tuliandika Mbarouk Wadi Mussa kwamba ni Mwakilishi wa Jimbo la Muyuni, jambo ambalo si sahihi. Usahihi ni kwamba Mhe. Mbarouk Wadi Mussa ni Mwakilishi wa wananchi Jimbo la Mkwajuni. Tunaomba radhi kwa makosa hayo na tunaomba Mhe. Mwakilishi atusamehe.

Mhe. Mwenyekiti kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi suali lake namba 21 lenye vifungu (a) ,(b) na (c) kama hivi ifuatavyo:-

a) Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kupitia Shirika la Bandari ina mpango wa kuongeza vyombo vya kuhudumia Makontena na mizigo bandarini kwa lengo la kuzidisha ufanisi wa kazi katika bandari hiyo. Mpango huo umeanza tokea mwaka 2009 ambapo Shirika liliweza kununua *Reach Stacker 2 na*

Terminal Tractor 2, mwaka 2011 Shirika lilinunua Kreni 2 kubwa na mwaka 2012 Shirika limeongeza *Reach Stacker 1, Container Empty Handler 1 na Forklift 1* kwa lengo la kuimarisha huduma za Makontena na mizigo bandarini hapo.

b) Ili kuondoa tatizo la kasoro zilizojitokeza za kuhudumia Makontena na mizigo, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kupitia Shirika la Bandari lina mpango endelevu wa kununua vyombo hivyo vya kuhudumia kwa madhumuni ya kuhimili ushindani wa utoaji huduma kutoa bandari jirani.

c) Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa kupitia Shirika itaendelea kununua vyombo ambavyo vitaleta tija katika Shirika la Bandari hasa katika kazi za kuhudumia makontena na mizigo mengine bandarini kwa ufanisi. Suala la viwango na umadhubuti ndio Sera ya Shirika letu

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri ya kuvunja moyo kutokana na serikali kutoa ahadi badala ya kutatua matatizo, kwa kuwa bandari ni nguzo ya uchumi wa nchi hii kwa nini hakuna utaratibu wa kununua vitendea kwa muda muafaka kulingana na mahitaji yake.

(b) Kwa kuwa hali hivi sasa ni mbaya kutokana na baadhi ya meli kushindwa kutendea kazi inafika pale meli hivi majuzi tu meli kubwa karibu makontena 70 mpaka 100 imeshindwa kufanya kazi kwa siku moja na nusu mpaka ikatafutwa *spare* kutoka Nairobi na huku msongomano wa meli unasubiri kufunga meli. Huoni ni kukosesha serikali mapato kwa kutokuwa makini utendaji wenu Mhe. Naibu Waziri.

(c) Kutokana na *crane* zilizonunuliwa kupitia mkopo kupitia PBZ tuliambiwa zinanyanyua tani 75 na ambao jambo hilo si kweli uwezo wake kununua tani 25 mpaka 40. Waziri ukiendelea kuahidi kuwa shirika linaendelea kununua vitendea kazi mpaka ukajibu swali la msingi na ukajisifu kwa madoido kulidanganya Baraza kwa vitendea kazi vilivyokuwemo humo ni vikongwe na havifai na niko tayari kuthibitisha hilo Mhe. Naibu Waziri kama nilivyoahidi. Na kwanza niipongeze wizara vile vile kuwa makini hivi juzi baada ya kupiga kelele baada ya Ofisi wakatumia mkoba wa ukili jana kuhamisha kupewa ofisi mpya ZSTC nimpongeze kwa hilo.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti hili la tatu azungumze taratibu mimi ninamsikiliza yeye niweze kumjibu wananchi waelewe naomba azungumze taratibu nimfahamu vizuri rafiki yangu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, Mheshimiwa rafiki yangu Naibu waziri tena sahiba wangu mkubwa, ulipokuwa ukijibu maswali haya sijui ulifanya utafiti au ulikuja tu ukawa unajibu lililokaa mdomoni unajibu Mhe. Naibu Waziri. Unajua Mwenyekiti sisi tunapata shida sana wananchi kutafuta haya masuala kuyaleta. Sasa Waziri au Naibu Waziri anapokujibu akawa hana uhakika swali la kujibu inakuwa mtihani kwetu sisi na wananchi wanatusikiliza.

Kutokana na serikali kutoa ahadi kutokana na matatizo kwa nini bandari ni nguzo ya nchi hii hadi hali hiyo hakuna utekelezaji wa ahadi hizo. Kwa kuwa hadi sasa hali ni mbaya bandarini na wananchi wanyonge wa nchi hii wakwezi na wachukuzi wanaopata shida kutokana na afya zao kama hana afya mtu pale hawezi kupata kula tofauti ya mimi na wewe. Hivi majuzi kuna meli imekuja ina c*ontainers* karibu 70 au 80 kwa siku moja na nusu huduma haikupatikana na huku kuna meli karibu tatu au nne ziko *queue* zinasubiri ukuta ule wa bandari mpaka *spare* ilipoagizwa kutoka Nairobi je umakini huu upo wapi.

Kutokana na *cranes* zilizonunuliwa kupitia mkopo wa benki zina uwezo wa kunyanyua tani 25 badala ya tani 75. Waziri ukiendelea kuahidi kwamba shirika litaendelea kununua vitendea kazi vyenye tija. Kauli hiyo si kuidanganya Baraza kutokana na mifano iliyopo bandarini hivi sasa na niko tayari Mhe. Mwenyekiti kuthibitisha kwa hilo.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, katika majibu ya msingi tumeeleza kwamba Shirika lilikuwa na mapungufu, kutoka mwaka 2009 shirika lilikuwa na mpango wa kuliendeleza shirika lenyewe. Katika utekelezaji wa mpango huo ndio unakwenda hatua baada ya hatua. Tumeeleza kwamba kutoka mwaka 2009 kuna vifaa ambavyo Shirika wamenunua katika kuimarisha na kuboresha huduma. Tumesema kwamba 2009 shirika lilinunua *Reach Stacker 2 na Terminal Tractor* 2, mwaka 2011 katika muendelezo huo huo Shirika likanunua crane 2. Mwaka 2012 shirika likanunua *cranes* nyengine 2 kubwa. Aidha katika mwaka 2012 tumenunua *MT handler 1 Reach Stacker* nyengine *1* mpya *Forklift* nyengine mpya. Lakini mwaka huu 2012 unaomalizia kuingia 2013 Shirika limenunua *Reach Stacker* nyengine moja mpya yenye uwezo wa kuchukua tani 45. Gharama za *Reach stacker* hiyo ni euro 559,833.

Katika utaratibu huo huo shirika limenunua *Forklift* nyengine mpya yenye uwezo wa kunyanyua tani 16 na *empty handler* nyengine mpya yenye uwezo wa tani 7 katika mwaka na matarajio yetu kwamba februari vifaa hivi vitafika, vimeshanunuliwa viko katika utaratibu wa kusafirishwa. Huu ndio utamaduni wa shirika katika kuimarisha huduma. Kama kuna mapungufu ndio maana tukasema endelevu hatujasema tumeshafika kikomo hatununui kifaa chengine. Tumenunua na tutaendelea kununua kuimarisha huduma ndio malengo ya shirika.

Mhe. Mwenyekiti, swali (b) Imani yetu tukiimarisha vitendea kazi mapato tabaan yataongezeka, yakiongezeka mapato katika shirika, mfuko wa serikali nao utakuwa umenona na hiyo ndio dhamira.

Jibu (c) Mhe. Mwenyekiti ninamuhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba sina dhamira, sina nia wala sijawahi kufikiria kuja kulidanganya Baraza hili. Ninachokisema nina hakika nacho, mimi niko tayari akatafute mzigo wenye tani 75 tukanyanyue kwenye *crane*. Inawezekana ikawa Mhe. Mwakilishi akawa hajafahamu vizuri uwezo wa utendaji kazi wa *crane*. *Crane* ninayoizungumza hapa ni ya mkonga na ili mkonga uweze kufanya kazi vizuri unakwenda kwa *radius* kwa maana kwamba *radius* kadri kitu kinapokuwa karibu na ule mkonga wenyewe ndipo unapopata nguvu ya kuweza kunyanyua. Utakapokiweka mbali nje ya *radius* mkonga hauna nguvu ya kuweza kunyanyua. Sasa mimi ninachomtaka Mhe. Mwakilishi atambue uwezo wa crane, eneo la kufanyia kazi na mazingira gani uwezo wa kunyanyua hizo tani 75 na kinyume na yeye anavyolidanganya Baraza kwa kusema kwamba *crane* hii ina

uwezo wa kunyanyua tani 25 analipotosha Baraza hili na anawapotosha wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, baada ya majibu mazuri ya ufafanuzi ya Mhe. Waziri naomba nimuulize swali lifuatalo. Kwa kuwa malalamiko ya uwezo wa *crane* yamekuwa ya muda mrefu kwamba serikali ilitenga fedha na Baraza hili wakaidhinisha kununua *crane* hiyo yenye uwezo wa kunyanyua mzigo wa tani 75. Na kwa kuwa mbali ya Mhe. Jaku ambaye tumesikia leo wapo wananchi wengi wanasema kwamba *crane* hiyo haina uwezo wa kunyanyua mzigo huo wakiwemo mafundi wa Idara yake. Kwa kuwa mali ile ni mali ya serikali, kwa maana ya mali ya umma haoni sababu sasa ya kuialika Kamati yake ya Miundombinu kwenda kushuhudia huo uwezo wa *crane* kama kweli ina uwezo wa kunyanyua tani 75 ili zile fedha zilizotengwa na serikali zisipotee ovyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, ninaamini mimi rai aliyokuja nayo Mhe. Mwakilishi itatusaidia sana, itaondoa huu uvumi, hii dhana na huu upotoshaji unaoendelea. Mimi nakubaliana mia kwa mia waiamini kamati yetu ya Ujenzi na Mawasiliano iende ikafanye ukaguzi baadae kamati italeta taarifa hapa.

Nam 35

Kuwekewa Majina katika Makaburi ya Wahanga wa Meli

Mhe. Hija Hassan Hija - Aliuliza:-

Mnamo usiku wa kuamkia Septemba 10, 2011 na ndani ya mwezi wa Julai, 2012, kipindi cha kasoro ya mwaka mmoja, Zanzibar imekumbwa na ajali mbili mbaya za kuzama kwa meli ya MV Spice Islanders 1 na MV Skagit katika mikondo ya Nungwi na nje kidogo ya Kisiwa cha Chumbe. Ajali zote mbili zilisababisha vifo zaidi ya 1200 na Majeruhi wengi sana pamoja na upotevu wa mali. Aidha baadhi ya maiti walizikwa na Serikali, katika makaburi huko eneo la Kama.

(a) Je, leo tunaweza kuyatambua majina ya marehemu waliozikwa katika makaburi yale kwa maana kwamba yameekewa vibao vya utambulisho.

(b) Tukio kama hili lililowahi kutokezea miaka ya nyuma kwa upande wa Tanzanaia Bara pale meli ya MV Bukoba ilipozama na kuua watu wengi, lakini wote walizikwa katika makaburi maalum na leo imekuwa ni sehemu ya kumbukumbu na historia kwa Taifa. Nini mipango ya Serikali kwa makaburi ya Kama.

(c) Kwa kuwa SMZ imeamua kununua meli yake mpya ili kuwaondoshea shida wananchi, na hatua hii baada ya umati mkubwa kupotea, Je, katika utengenezaji wa meli hiyo hatuoni haja ya kutiwa alama, jina au kumbukumbu yoyote ya wahanga wetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu:-

Mhe Mwenyekiti**,** kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi suali lake namba 35 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama hivi ifuatavyo:-

a) Suala hili la mazishi limeshughulikiwa na Idara ya Maafa iliyo chini ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa kushirikiana na Vikosi vya Ulinzi na Usalama vya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar pamoja na vile vikosi vya ulinzi na usalama vya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha kwa maiti waliopatikana siku ya mwanzowa tukio, wengi walitambuliwa na kuchukuliwa na jamaa zao, na wale waliofuatia siku ya Pili na ya tatu hawakuweza kutambuliwa. Tabaan wale ambao hawakuweza kutambuliwa sura zao hivyo hivyo na majina yao yalishindwa kutambuliwa.

b) Serikali imelizingatia suala hilo lakini jambo kubwa na la msingi ni kujikumbusha katika mila, silka na utamaduni wetu katika utekelezaji wa suala hilo.

c) Hivi sasa Serikali imo katika hatua za ujengaji wa meli mpya, kuhusiana na jina gani iitwe litaamuliwa baada ya ujenzi wa meli hiyo itakapokamilika. Aidha wazo la Mhe. Mjumbe serikali inalizingatia.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, baada ya majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri nataka aendelee kutuelimisha kwamba kuweka alama na kumbukumbu ya makaburi ya wahanga wetu ukilinganisha na mila na desturi za wazanzibari, kuna athari gani ya kuweka makaburi hayo alama au kumbukumbu ya makaburi hayo ili vizazi vijavyo vikitambua kwamba makaburi hayo ni ya wahanga wetu wa ajali ya meli ya mwaka Fulani.

Lakini (b), Kwa kuwa sasa hivi meli mpya ya serikali inaendelea kujengwa kwa mujibu wa taarifa ya serikali, kwa nini haiwekwi angalau alama mojawapo ya kutambua kwamba wahanga wetu ndio chanzo cha serikali kuamua kununua meli mpya kwa ajili ya maslahi ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, suala la kuyatambua na kuyahifadhi ni suala la msingi na serikali itafanya hivyo, nilichokisema kwamba kuweka zile alama kwa kulijua kwamba kaburi hili la Hija, hili la Jaku, hili la Jazira hilo hatuwezi kulifanya kwa sababu wale maiti wenyewe hawakuweza kutambuliwa kwa sura na majina yao. Lakini suala la kuweka ukuta kuyahifadhi ni jambo la msingi na serikali imelikubali tutalifanya.

Suala la jina Mhe. Mwenyekiti nimemjibu Mhe. Mwakilishi kwamba Serikali inazingatia. Mimi nadhani si vyema wala si busara kugombania hindi hata hilo shamba lenyewe halijamalizwa kufyekwa. Tusubiri meli ijengwe imalizike, serikali itatafakari tutaweka jina litakalokuwa na maslahi na wazanzibari wote.

Nam. 110

Hukumu za Mahamaka kwa Lugha ya Kiingereza

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Mahakama zetu hapa nchini zimekuwa zikiendesha kesi kwa lugha ya Kiswahili lakini mwenendo wa kesi (*proceedings*) na hukumu (*judgements*) zimekuwa zikiandikwa kwa lugha ya Kiingereza.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha hukumu zinaandikwa kwa lugha ya Kiswahili ili watuhumiwa wapate haki yao ya kujua hukumu zao kwa ufasaha na kwa lugha wanayoielewa.

(b) Je, ni lini Serikali itaanzisha utaratibu wa kuweka vitabu vya ripoti ya kesi za Mahakama Kuu ya Zanzibar kwa lugha ya Kiswahili ili kuwezesha wananchi kuzisoma kwa urahisi ili wapate kuelewa.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria -Alijibu:-

Mhe. Spika kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi suali lake Nam. 110 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Lugha rasmi ya Mahkama ni Kiswahili na Kiingereza, kumbukumbu za kesi zinaweza kuwekwa kwa lugha yoyote kati ya hizo na Mahkama zimepewa uhuru wa kuamua kutumia lugha moja kati ya hizo. Kwa hivyo kimsingi Serikali haina mpango wa kulazimisha lugha ipi itumike Mahkamani. Hii ni kwa sababu Mahkama zetu ni Mahkama muhimu na zinashughulikia hata mambo ya nje kwa hivyo zinaweza kukatiwa rufaa kwa Mahkama ya Rufaa Tanzania na Mahkama nyengine. Na kwa sababu Mahkama ya Rufaa mara zote hutumia lugha ya Kiingereza, basi ni vyema kwa ule mwenendo wa kesi unaotokea chini uwe kwa lugha ya Kiingereza ili kurahisisha mwenendo mzima wa kesi wakati wa rufaa.

Pili Mahkama zetu zinatumia mawakili wazoefu wa nje na ndani ya nchi, hivyo lugha rahisi wanayoweza kufahamiana ni lugha ya kiingereza. Ni vyema pia kuelewa kuwa Sheria zimewapa uwezo Mahkama za Kadhi na Mahkama ya Mwanzo pekee kutumia lugha ya Kiswahili, kwa sababu Mawakili hawaruhusiwi katika Mahkama hizi.

(b) Mhe. Mwenyekiti, serikali kwa kupitia wizara yangu na Mahkama Kuu pamoja na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu tumeshaanzisha kukusanya taarifa za kesi muhimu kwa lengo la kuwa na vitabu vya ripoti za kesi za Mahkama Kuu Zanzibar. Hata hivyo, kazi hiyo inahitaji maandalizi mengi katika kufanikisha kwa azma hiyo ikiwepo kuwa na fungu la fedha ambalo litatosheleza mahitaji muhimu ya kugharamikia kazi hiyo, kama vile posho la wataalamu watakaokusanya hukumu za kesi mbali mbali na kuzihakiki, kulipia gharama za uchapishaji wa vitabu hivyo na kadhalika. Kwa vile kazi hiyo inategemea upatikanaji wa fedha haitokuwa rahisi kutaja tarehe.

Lakini pia kazi hii ni nzito sana kwa sababu kitabu cha mwisho cha ripoti za kesi (*ZLR*) ni zaidi ya miaka hamsini (50) nyuma, nafikiri ni kuanzia 1956. Hivyo basi, kuifanya kazi hii ni vizuri na ni lazima kuanzia tarehe hiyo ya 1956 mpaka hii leo 2013.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na hayo kazi hii tumeshaianza lakini bado itachukua muda kutokana na umuhimu wake na wingi wake. Kama nilivyosema kumbukumbu hizi zitakuwemo katika lugha ya Kiingereza kwa sababu ndio lugha ambayo mara nyingi inatumika katika mahkama hizi na Mahkama za Rufaa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri kwa nini Kiswahili ni lugha yetu ya taifa lakini tunashindwa kukiheshimu na kuendelea kufuata lugha ya wakoloni wakati Zanzibar tumejigomboa.

Pili, kwa kuwa wafungwa wengi wanashindwa kukata rufaa kutokana na kushindwa kupata nakala zao za hukumu kwa muda muwafaka. Je, kitendo hicho si uvunjaji wa haki za binadamu katika matumizi ya mahkama.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli lugha ya Zanzibar au lugha ya taifa ni ya Kiswahili, lakini kama nilivyosema sisi tuna wenzetu na mahkama sio za Zanzibar tu, mahkama ni zetu pamoja na watu wa nje. Watu wa nje wanatumia mahkama zetu kwa kutafuta haki zao, kwa hivyo kuna maeneo maalum ambayo lazima shughuli za mahkama ziende kwa Kiingereza na ndio maana tukaruhusu mawakili hata wa nje waliokuwa hawajui Kiswahili ili waweze kuendesha kesi hizo. Sasa tukisema kwamba mahkama ziende kwa lugha ya Kiswahili tu kwa kweli tutawanyima haki watu wetu na watu wengine ambao wanataka haki yao katika mahkama zetu.

Lakini la pili Mhe. Mwenyekiti, kuna utaratibu maalum kama mtu ameshapelekwa gerezani ameshafungwa utaratibu uliopo kama anataka kukata *appeal* au rufaa basi askari wa Vyuo vya Mafunzo ndio wanaohusika kutayarisha mafaili yao na kuyapeleka mahkamani na utaratibu huo wanaujua. Tatizo linaweza likawepo kwamba labda zile nyenendo za kesi zinachelewa kupatikana na hii inakuwepo si mara zote lakini baadhi ya wakati tatizo hilo tumeligundua. Na katika utaratibu maalum tuliouweka wa mwenendo wa kusukuma kesi *priority* tumewapa wafungwa ili haki zao ziweze kutekelezeka haraka iwezekanavyo.

Nam 73

Kampuni za Simu Kudhalilisha Uislam

Mhe. Rufai Said Rufai - Aliuliza:-

Naipongeza serikali kwa kuweza kusajili Kampuni kadhaa za simu nchini jambo ambalo limerahisisha kwa kiasi kikubwa mawasiliano baina ya wananchi. Kwa kuwa Zanzibar zaidi ya asilimia 95 ya wananchi wake ni Waislamu ambao wamejikita katika imani yao ya kiroho kupitia dini hiyo, na kwa kuwa makampuni mengi ya simu kabla ya kuunganisha na upande mwengine

"*computer*" zao husema "UKITAKA KUKOPI WIMBO HUU BONYEZA NYOTA" ghafla utasikia aya ya Qurani Tukufu ikisomwa.

Je, kwa kufanya hivyo si kuudhalilisha Uislamu.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 73 kama ifuatavyo:-

Ni kweli kabisa Qur-an kuita wimbo ni kosa kwa mujibu wa Dini yetu ya Kiislamu na vile vile Qur-ani kusikika katika milio ya simu si jambo jema. Masheikh wetu wanatwambia kuwa inaposomwa Qur-ani ni lazima isikilizwe kwa utulivu na umakini. Kwa mantiki hiyo, Qur-ani kuifanya ndio mlio wa simu si vizuri, haipendezi na haifai.

Mhe. Mwenyekiti, kwa vile ni watumiaji wa simu wenyewe ambao hupendelea milio yao ya simu kuweka Qur-ani ningeliwashauri wao wenyewe kwanza kama kweli ni Waislamu wa kweli kweli na wanaipenda na kuifuata dini yao ya Kiislamu wakajiepusha na suala hili ili lisiendelee.

Lakini pili Mhe. Mwenyekiti, muumini wa kweli anapoona Qur-ani ikidhalilishwa au hata dini yetu ikidhalilishwa basi ni wajibu wake kukemea tabia hiyo na zaidi kuwapigia wahusika kutoa malalamiko hayo. Wengi wetu tumeshafanya hivyo nikiwemo mimi mwenyewe ninayejibu swali hili, nimeshawapigia *Zantel* na nikawaambia na wakarekibisha. Kwa hivyo, hilo ni jukumu la mtu binafsi kulifanya asisubiri serikali ndio imfanyie kama kweli ni Muisilamu wa kweli. Nawaomba Waislamu nyote wapenzi tuwe makini kuitekeleza na kuilinda dini yetu pamoja na kitabu chetu kitukufu tusisubiri mpaka Muislamu mwengine afanye kazi hiyo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa nataka nimpongeze kwa dhati Mheshimiwa muasisi, mwana mapinduzi kwa swali lake la msingi alilioliuliza ambalo lilikuwa linanikera kwenye roho ndani ya moyo wangu.

Mhe. Mwenyekiti, serikali inachukua hatua gani kuhusu bahati nasibu zinazochezeshwa na mashirika ya simu.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, mimi binafsi sina uhakika kwa sababu simu yangu nnayotumia ni kumpigia Mhe. Jaku Hashim na kusikiliza basi, sasa ikiwa kuna utaratibu huo mimi nafikiri Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano tutashirikiana tutizame utaratibu ulioko ili tujue ni kitu gani hasa kinachofanywa.

Mhe. Rufai Said Rufai: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru japo kuwa mwanzo nimesimama katika kutoa swali langu la nyongeza lakini umeninyima, lakini nashukuru kwa mara ya pili kuniona. Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwamba Mhe. Waziri amekiri kuwa hili tatizo lipo na kwa kuwa imani ya Waislamu kwamba Qur-ani si nyimbo na wala si mashairi bali ni maneno ya Mwenyezi Mungu matukufu. Na kwa kuwa mitandao mingi ya simu tuliyonayo inashindwa kufanya ufafanuzi baina ya nyimbo na Qur-ani.

Je, wizara yako Mhe. Waziri ijapokuwa umetwambia kwamba umewahi kuwapigia Zantel lakini ni Zantel hao hao hili jambo linaendelea. Je, utachukua hatua gani ya kinidhamu juu ya mitandao hii ambayo Qur-ani wanahusisha na nyimbo.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, naomba ieleweke kwamba serikali haina dini, dini ni ya mtu binafsi, dini ni ya muumini binafsi, muislamu huyo huyo pengine anaweza yeye mwenyewe angelipenda asikie wimbo katika simu na wako wengine wanafanya. Mimi ukiniuliza nitakwambia haifai na ndio maana mimi binafsi kwa sababu haifai simu yangu haina qur-ani, lakini muislamu mwengine anaweza akaona kwamba yeye anataka. Huo ni uhuru wake chini ya katiba serikali haiwezi kuingilia uhuru wa mtu kuamini dini anayotaka, kuamini imani anayotaka, kama wewe umekereka na kitendo hicho ni wajibu wako wewe mwenyewe kuwaambia shirika kwamba mimi katika simu yangu sitaki kama walivyofanya baadhi ya watu wengine pamoja na mimi waumini wa kweli.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru sana kwa leo kupata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, katika dunia hii kuna watu wanaofuata dini waitakayo na kuna watu hawana dini yoyote wale nafikiri wanaita Mapagan. Kwa sababu kila siku inasisitizwa kuwa serikali haina dini lakini sisi tulioiweka serikali ni watu wenye dini na tungetegemea serikali ijali sana dini yetu. Kwa hivyo, kwa kuwa serikali inasema haina dini je, msimamo huu wa serikali kutokuwa na dini wamepata katika nchi gani na serikali tukisema ndio chombo ambacho kinaongozwa na Mapagan kwa sababu ndio waliokuwa hawana dini serikali ni watu je sikukosea.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, tunaposema kwamba serikali haina dini si kwamba serikali inaongozwa na Mapagan, tunaposema kwamba serikali haina dini ni kusema kwamba serikali haina ule msimamo wa kusema kwamba serikali hii itaongozwa kwa misingi ya dini fulani. Kwa mfano, Serikali ya Uingereza unaweza ukasema kwa sababu wao wamesema hasa kua serikali yao ni ya Kikristo, sasa sisi tunasema hatwendi hivyo kila mtu tunamuachia uhuru aamini dini anayotaka na serikali inafanya shughuli zake. Ingawa serikali au viongozi wa serikali wote wana dini zao na wengi watakuwa ni Dini ya Kiislamu, lakini hatujasema kwenye katiba au kwenye sheria nyengine yoyote kwamba serikali yetu itaongozwa kwa misingi ya dini fulani ndio maana tukasema kwamba serikali haina dini kwa misingi hiyo, dini wameachiwa watu wenyewe.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe kabla katibu hajasimama kuna vitu naomba kuzungumza. Kitu cha kwanza hii kanuni yetu naona kidogo ina mapungufu fulani inaelekeza kwamba sio kuwa yule anayeuliza swali kwa niaba ana haki ya kupewa swali lake jengine la ziada kuuliza, haituongozi hivyo hii kanuni kama ambavyo Mhe. Rufai alikuwa amezungumza.

Lakini jambo la pili nilikuwa nataka kutahadharisha kwamba kwa mujibu wa kanuni zetu mtu mwenye kuuliza swali baada ya swali la msingi ana haki ya kuuliza maswali mawili tu ya nyongeza si matatu kama tulivyokuwa tumezowea.
Jana jioni tulipokuwa tumekaa na Mhe. Spika alinifahamisha hili na napenda tuwafahamishe na wenzetu kwamba maswali ya nyongeza ni mawili sio matatu. Ahsante Katibu tuendelee.

Nam 105

Maandalizi ya Kuifanya Hospitali ya Mnazimmoja Kuwa ya Rufaa

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Hivi karibuni Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alitoa kauli ambayo hata Mhe Waziri wa Afya aliisisitiza kwenye Baraza hili kuwa Hospitali ya Mnazi Mmoja itakuwa ya Rufaa.

(a) Je, ni maandalizi gani mpaka sasa yamefanyika kwa upande wa wataalamu wa kutosha, nyenzo za uhakika na maslahi mazuri kwa wanyakazi ili kufanikisha lengo hilo.
(b) Lini Wazanzibari wategemee Hospitali yao hiyo kuwa ya Rufaa.

(c) Hospitali hiyo itakapokuwa ya rufaa ni huduma zipi za afya ambazo hazikuwa zikipatikana Hospitalini hapo sasa zitakuwa zinapatikana.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam.105 lenye Kifungu (a), (b), na (c) kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein wakati wa kampeni zake za uchaguzi kupitia ilani ya CCM aliahidi kwamba, akipata ridhaa ya wananchi kuiongoza Zanzibar, Hospitali za *Cottage* zitapandishwa daraja kuwa za Wilaya na zile nyengine kubwa zilizoko Pemba zitapandishwa kuwa za Mikoa, Mnazi Mmoja Unguja kuwa ni Hospitali ya Rufaa.

Kwa kauli yake hiyo ya wakati wa kampeni, ndio maana anarudia kuyasema hayo ili kusisitiza ahadi yake aliyoitoa. Na Mhe. Waziri wa Afya aliweza kulisisitiza hilo kwenye Baraza hili kwa sababu Serikali yetu ya Umoja wa Kitaifa inatekeleza ilani ya Uchaguzi wa CCM.

(a) Mhe. Mwenyekiti, maandalizi ambayo sasa yamekwisha fanyika ni kujua ni maradhi gani yanayotakiwa yatibiwe kwa ripoti za wagonjwa wanaohudhuria katika mahospitali.Taarifa hizo ni muhimu kwa ajili ya maandalizi ya miundo mbinu na matayarisho ya nguvu kazi kwa maana ya wataalamu wa maradhi hayo kuandaliwa. Hili limeweza kuamuliwa kutokana na takwimu tulizonazo ambazo zinaonesha ni maradhi gani ambayo yanatumia fedha nyingi kuwapeleka wagonjwa nje ya Zanzibar kwa matibabu.

Suala la maslahi ni la Wizara ya Utumishi ambayo imeshaweka vigezo kwa wataalamu wa kada zote za afya kwa hiyo maslahi yao yatashughulikiwa ipasavyo kulingana na elimu zao.

(b) Hospitali kutoka hatua iliyopo na kuwa ya rufaa si suala la lini itakuwa. Huu ni mchakato ambao utachukuwa muda kuweza kufikia kuwa hospitali ya rufaa kamili,

kwa sababu jambo lenyewe lina hatua nyingi kutoka kwenye hali iliyopo sasa kuwa hali nyengine. Mhe. Mwenyekiti hata Rome haikujengwa kwa siku moja".

i. Mhe. Mwenyekiti, kwa kuanzia kuna haja ya kuondoa baadhi ya Idara ndani ya majengo hayo na kuhamishia sehemu nyengine. Na ndio maana kunatayarishwa ujenzi wa jengo jengine liliopo pembezoni mwa hospitali ya Mnazi Mmoja ili kuhamishia huko Idara nyengine zilizopo katika jengo kuu ili iweze kupisha hizo huduma mpya zitakazo anzishwa.

ii. Baada ya hapo kutakuwa na marekebisho mengi ya ndani ya majengo ili kukidhi uwekaji wa vifaa vya matibabu hayo.

iii. Ununuzi wa vifaa hivyo ambavyo vitafuata taratibu za zabuni na manunuzi. Vingi ya vifaa hivyo vitatoka nje ya nchi.

iv. Baadae tunaandaa kusomesha wafanyakazi watakaotoa huduma hizo za ziada. Hata hivyo kuna wafanyakazi wameshapelekwa kusoma na wengine wanaandaliwa.

v. Kuandaa kiwanja kwa ajili ya kujenga hospitali kubwa ya kuhamishia shughuli nyengine zitakazo ondoshwa Mnazi Mmoja.

Hayo yote yanahitaji bajeti iliyokuwa si ndogo, Kwa hiyo, baada ya kupata mchanganuo wa bajeti itakayohitajika kwa kazi hiyo kila mwaka wa Bajeti Serikali itatenga fungu la fedha za maendeleo na pia kutafuta wahisani kusaidiana kufikia azma hiyo.

Hata hivyo, mazungumzo na wahisani tofauti yanaendelea kwa ajili ya maandalizi ya idara tofauti. Pia viongozi na wafanyakazi wamepata fursa za kutembelea nchi tofauti zinazotoa huduma hizo ili kujifunza kwa wenzetu na kuona wanafanya vipi na watatusaidiaje kwa hizo huduma tunazoziandaa kuanzishwa kutoa hapa kwetu.

Si hivyo tu, wataalamu mbalimbali wamefika hapa na wataendelea kuja kwa ajili ya kufanya uchambuzi yakinifu kuhusu kuanzisha huduma hizo. Huduma zitakazo tolewa kwenye hospitali ya rufaa ni za maradhi ya saratani "*Oncology*", maradhi ya moyo, *Operesheni* za moyo"*Cardiac Surgery*", matibabu ya mafigo na usafishaji wa damu "Dialysis", na kitengo cha ajali na dharura "*Emergency Care Unit*".

Kitengo cha rufaa cha matatizo ya mama waja wazito na watoto, kitengo kamili cha upasuaji wa maradhi ya mishipa ya fahamu na vichwa maji kwa watoto *"Neuro Surgery*" na *ICU* katika Idara tofauti. Pia tayari kumeshafungwa mashine maalum zinazotumika kufanyia operesheni mbali mbali. Idara ya meno kufanya upasuaji wa midomo sungura, taya na shingo, upasuaji mkubwa unaotumia TV maalum kwa kupitia tundu ndogo, mashine za kisasa katika kitengo cha macho ambazo zitatumika kupima vipimo vyote vitakavyo hitajika kulingana na huduma zitakazotolewa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu marefu sana ya Mhe. Naibu Waziri naomba kumuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ulivyosema Mhe. Mwenyekiti.

(a) Kwa kuwa hivi sasa ni mwaka wa tatu wimbo huu umekuwa ni wa muda mrefu kuimbwa kuelekea hospitali ya rufaa. Anaweza kutueleza Mhe. Naibu Waziri mambo gani yashakamilika na mambo mangapi hayajakamilika tokea kutoa kauli hiyo Mhe. Rais.

(b) Kwa kuwa Hospitali ya Mnazi Mmoja inahitaji madaktari bingwa wakati idadi kubwa ya madaktari kuondoka na kuelekea nchi za nje. Serikali inachukua hatua gani za kuwalinda madaktari hao waliokuwepo ikiwemo kuwalipa haki zao. Kwa mfano hivi sasa kumekuwa na kilio cha miezi mine *call allowance* zao madaktari hawajalipwa pamoja na serikali kuidhinisha suala hilo. Mhe. Naibu Waziri naomba mashirikiano yako kupata jawabu.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, nafikiri kalisikia tu swali refu lakini hakusikiliza nilichokisema. Hilo swali la mwanzo nimejibu yote katika hilo swali la msingi alilonuliza na ndio maana majibu yakawa marefu kwa sababu nilikuwa nataka afahamu. Kwa hivyo, nafikiri sasa hilo sitoweza kurudia kwa sababu yatakuwa marefu tena. Kama anataka aende akachukue *Hansard* atayasoma yote kwa kuokoa muda.

UTARATIBU

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, mimi nilichozungumza ni Kiswahili wala sijazungumza Kihindi, nilichomtaka anieleze madaktari wengi wamekuwa wakiondoka na inaonekana ni kutokana na maslahi yao kutokulipwa. Leo mwezi wa nne madaktari hawajalipwa *call allowance* zao, narudia tena leo karibu mwezi wa nne madaktari hawajalipwa *call allowance* zao atawahakikishia vipi madaktari hawa waliokuwepo wasije wakaondoka kulipwa *call allowance* zao. Mhe. Mwenyekiti, wewe ndiye mwenye kukataa swali au kujibu swali.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe hata na sisi tulishuhudia namna Mhe. Naibu Waziri alipokuwa akitoa ufafanuzi wa hayo maswali. Kwa bahati mbaya wakati Mhe. Naibu Waziri anajibu wewe ulikuwa unazungumza na Mhe. Hija Hassan. Naomba ukubaliane na maelekezo ya Mhe. Naibu Waziri kama huna swali jengine acha utaratibu uendelee. Naomba ukae kitako tuendelee.

Nam 22

Matengenezo ya Uwanja wa *Mao-Tse-Tung*

Mhe. Nassor Salim Ali - Aliuliza:-

Kwa kuwa Chama cha Mpira wa Miguu Zanzibar (*ZFA*), tayari kimepata Rais wake mpya na kuanza kwa kasi zaidi ya kuleta maendeleo ya mchezo huo, kwa kuanza kuufanyia ukarabati mkubwa Uwanja wa Mao-Tse-Tung na kuonesha uzalendo wake kwa kushirikiana na viongozi wenzake wa *ZFA*.

(a) Je, wizara imechangia kiasi gani katika kufanikisha ukarabati wa uwanja huo wa *Mao-Tse-Tung.*

(b) Je, ni hatua gani Wizara imechukuwa kuwapa *ZFA* muongozo ulio bora wa kuufanya uwanja huo uwe wa kisasa.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 22 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, ni kweli Chama cha Mpira wa Miguu, *ZFA* kimeanza kufanya matengenezo ya uwanja wa *Mao-Tse-Tung*. Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu haijachangia katika kufanya matengenezo yaliofanywa hivi sasa katika uwanja wa *Mao-Tse-Tung* kwani wizara inaamini gharama hizo zimo ndani ya uwezo wa *ZFA* iliyopo hivi sasa na haijatarajia mchango wa wizara yangu katika kufanya matengenezo hayo yaliyofanyika.

(b) Wizara yangu na Baraza la Taifa la Michezo, Kamisheni ya Utamaduni na Michezo, imekua mara kwa mara ikitoa ushauri na miongozo kwa *ZFA* juu ya namna bora ya kuufanya uwanja huo uwe wa kisasa. Wakati huo huo, wizara yangu imewasiliana na washiriki wa maendeleo juu ya uwezekano wa kuujenga uwanja huo.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, katika majibu ya Mhe. Naibu Waziri amekiri kwamba wizara haikuchangia fedha zozote katika ukarabati wa uwanja ule wa *Mao-Tse-Tung* na amekiri kwamba wametoa ushauri tu kwa *ZFA.* Je, haoni kwamba wizara kutokuchangia fedha zozote katika kuufanyia ukarabati uwanja ule kumeufanya uwanja ule usiwe bora.

Pili, alinijibu pia kwamba kuna mashirika ya kimaendeleo ambayo wamezungumza nayo. Ni mashirika gani hayo ambayo yameonesha nia ya kuweza kusaidia kuufanyia ukarabati uwanja ule na kuwa wa kisasa na kuendana na wakati ambao tunautegemea katika miaka hii inayokuja.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utali ina Michezo: Mhe. Mwenyekiti, naomba kumueleza Mheshimiwa kuwa hiyo si sababu ya kuwa wizara haikuchangia ikawa uwanja wa *Mao-Tse-Tung* utakuwa hauna ubora. Kama nilivyoeleza kwenye swali mama kwamba hii *ZFA* ya leo kwa kweli ni nzuri na ina mwelekeo ambao unaweza kuwahudumia wananchi wake kwenye kutengeneza viwanja kama hivyo.

Swali la pili, kwenye swali mama kweli nilieleza kwamba washirika wa maendeleo tumezungumza nao akiwa ni Balozi mdogo wa China mimi mwenyewe binafsi pamoja na Katibu Mkuu na Mwenyekiti wa Baraza la Taifa la Michezo na *ZFA* tulikwenda kukiangalia kiwanja hicho na yeye mwenyewe binafsi akasema atasaidia serikali kwa kujenga kiwanja hicho.

Nam 23

Mashindano ya Kombe la *Challenge*

Mhe. Nassor Salim Ali - Aliuliza:-

Kwa kuwa hivi karibuni Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein aliutaka uongozi wa wizara, BTMZ na ZFA kuhakikisha kwamba kombe la *challenge* linakuja Zanzibar

a) Jee, wizara imejipanga vipi kwa kushirikiana na BTMZ na ZFA kuiandaa timu yetu ya taifa ya Zanzibar Heroes kulitwaa kombe hilo katika mashindano yatakayofanyika mwezi Novemba, nchini Uganda.
b) Jee, ni mikakati gani ya maandalizi iliyofanywa kuiandaa mapema na kuiweka kambini timu hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 23 lenye vifungu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein aliutaka uongozi wa wizara na BMTZ na ZFA kuhakikisha kwamba kombe la *challenge* la mwaka 2012 lije Zanzibar.

a) Mhe. Mwenyekiti, wizara kwa kuhakikisha na BMTZ na ZFA ilihakikisha kwamba anapatikana kocha mzalendo ambaye ana uwezo na uzoefu katika kufundisha timu yetu ya Zanzibar Heroes ili iweze kumudu ushindani wa kimataifa.
b) Wanachaguliwa wachezaji bora kabisa tulio nao ili kuunda timu yenye uwezo na uzoefu katika mashindano ya kimataifa. Mhe. Mwenyekiti, imewapa msaada na mashirikiano makocha na maarifa wachezaji katika muda wote wa mazoezi, ilifanya mikakati ya kuwatafutia hoteli nzuri na huduma zote zinazohitajika za kuwawezesha kufanya mazoezi kwa utulivu na hamasa, kuwapatia huduma za kifedha ambazo zinawawezesha kushiriki kwa moyo wao wote kwenye mashindano hayo.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, mbali na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ambaye ni Makamo Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Zanzibar Dkt. Ali Mohammed Shein bado ana kiu kubwa ya kuona Zanzibar inaleta kombe kwa mara ya pili hapa Zanzibar, pamoja na wananchi na wapenzi wa mpira wa miguu Zanzibar.

Mashindano ya mwaka huu ambayo yatafanyika nchini Kenya mwezi wa Novemba, timu yetu ya Zanzibar Heroes katika mashindano yaliyopita ilifika nusu fainali. Jee, wizara pamoja pamoja na Baraza la Michezo na ZFA kwa ujumla imeanza mikakati gani kuiandaa timu yetu ya Zanzibar

Heroes katika mashindano yanayokuja ya *challenge* ambayo yatafanyika nchini Kenya ili kuleta kombe hili kwa mara ya pili.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Mwakilishi kwa kweli wewe ukiwa ni mmoja wa mjumbe wa ZFA, kwa kweli suala hili wizara yangu inafuatilia vya kutosha ili timu yetu ya Zanzibar Heroes itakapokwenda Kenya ishinde na kuna uwezekano mkubwa wa kushinda kwa sababu wizara pamoja na ZFA na Baraza la Taifa la Michezo lina mashindano makubwa ya kuweza kuendeleza hapa nchini petu.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba nimuulize swali (a) na (b) kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Rais anapozungumza inakuwa ni amri au agizo na tayari amesema kwamba ana hamu ya kombe hili kuja Zanzibar mwaka huu ikiwezekana. Mhe.Mwakilishi amesema kwamba kuna maandalizi ya mchezo huo nchini Kenya.

Lakini Mhe. Naibu Waziri anasema wanafuatilia, naomba kwanza anielimishe wanafuatilia wapi. Hilo la kwanza.
Lakini la pili, mbali ya maandalizi ya Baraza la Michezo na ZFA pamoja timu yenyewe, ningependa kujua wao kama serikali wanaekeza nguvu gani ya kifedha kwa ajili ya kuiwezesha timu yetu kushinda au ndio bado wanafuatilia.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nimuhakikishie mimi mwenyewe binafsi kwa kushirikiana na wizara tunatoa pesa kwenye timu zetu ili zinapokwenda kwenye mashindano kupata ushindi na kupata mwelekeo ambao wa kimichezo na kucheza mpira ili kuendelea kusonga mbele kwenda kwenye mashindano ya kimataifa.

Nam. 67

Msaada wa Serikali kwa Wakulima na
Wavuvi wa Wawi Kupata Soko la Uhakika

Mhe. Salim Abdalla Hamad (Kny; Mhe. Saleh Nassor Juma) – Aliuliza:-

Kwa kuwa kupitia MKUZA serikali ina mkakati wa kuongeza kipato na kupunguza umaskini. Na kwa kwa kuwa wananchi wa Jimbo langu la Wawi huzalisha sana mazao ya kilimo kama vile tungule, ndizi nakadhalika. Aidha wengine wameekeza zaidi kwenye uvuvi wa madagaa na samaki.

Na kwa kuwa katika kipindi cha msimu, wakulima pamoja na wavuvi hao, kwa sababu uzalishaji huwa mkubwa kuliko mahitaji hulazimika kuuza mazao yao kwa bei ya chini mno jambo ambalo linateremsha sana kipato na hatimae kuzidisha umaskini.

Jee, ni lini serikali itawasaidia wakulima pamoja na wavuvi wa Jimbo la Wawi kupata soko la uhakika la mazao yao ya kilimo na uvuvi.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 67 kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba kutoa maelezo kama ifuatavyo.

Kupata soko la uhakika kunachangiwa na mambo mengi ikiwa ni pamoja na wakati muafaka wa kuzalisha viwango bora vya mazao shambani, usafirishaji salama, utunzaji, usindikaji na vifungashio bora vya kuvutia. Kimsingi ukiyatizama haya ni sawa na kuwa umeongeza thamani ya mazao kwa kuwa yatakubalika na walaji wa ndani na nje na hatimaye kupelekea kuongezeka kwa kipato.

Mhe. Mwenyekiti, ili kukidhi vigezo hivi ni lazima wazalishaji na wadau wengine wawe na taaluma ya mchakato ya mnyororo wa thamani wa zao husika tokea kuzalisha hadi kumfikia mlaji, taaluma hii inamuhusu mkulima, mvuvi, wasafirishaji wa vyombo vya nchi kavu, baharini na angani, wachukuzi, madalali na hata watunza maghala ya kuhifadhia.

Serikali kupitia programu ya miundombinu kuongeza thamani ya mazao na huduma ya kifedha vijijini imejipanga kuwawezesha wazalishaji na hatimaye kuwaunganisha na masoko.

Mhe. Mwenyekiti, kipengele hiki kitahusika sana na taaluma za kimasoko, usarifu wa mazao na kupunguza upotevu wa mazao shambani baada ya kuvuna kwa kutumia kituo chetu cha usarifu wa mazao kiliopo Kizimbani na chengine kinachotarajiwa kufanyiwa ukarabati huko Pemba Ole.

Makundi ya uzalishaji watapatiwa mafunzo ya vitendo na nadharia kwa mazao waliyoyapendekeza kupitia wilaya zao. Baada ya kuhitimu wazalishaji chini ya umoja wao watakuwa na fursa ya kusaidiwa na programu gharama za kununulia mashine za kusarifu pindi wakiwa tayari kuchangia asilimia 25 ya gharama.

Mhe. Mwenyekiti, utatuzi wa uhaba wa masoko ya mazao ya kilimo hasa wakati wa msimu utapatikana pale tu wadau wote husika waliomo kwenye mnyororo wa thamani watakapofahamu thamani hii wakatekeleza majukumu yao na kushajihishana, serikali imeshaanza mchakato wa kuwafikishia wakulima wazalishaji kuelekea kupata masoko ya uhakika almuradi mashirikiano kati ya wataalamu na maeneo husika na wakulima yanaimarika na kuelewana vizuri.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata majibu ya kitaalamu yenye azma nzuri hapo baadae ya kuwawezesha wakulima wetu kuweza kuzalisha mazao mazuri, kusafirisha na kupata fedha inayohitajika.

Lakini hata hivyo kutokana na suala lilivyo ni kuwa Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa yote haya hayajafanywa na kila sehemu inazalisha.
Swali langu ni hivi, kwa vile mazao yanayozalishwa katika jimbo hili la Mhe. Saleh Nassor Juma pia yanazalishwa katika sehemu nyengine na kwa sababu ni mazao yanayohitajika sana kweli hapa Zanzibar na hata upande wa pili wa muungano.

Hivyo kuwa serikali Mhe. Mwenyekiti, imeshindwa hivi sasa kuwashughulikia watu hao wa Jimbo la Wawi kwa mazao yao yanayozalishwa alau kuwapatia soko hapa Zanzibar wakati mahoteli yote yanahitaji mazao haya na badala yake mpaka kulazimika sisi kununua mazao kama haya kutoka nje ya Zanzibar, kwa mfano ni kweli
Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe tunaomba swali la nyongeza.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Ni kweli Vitongoji kunazalishwa tungule nyingi sana. Kwa sababu Zanzibar tunaagizishia tungule nyingi kutoka Bara, ndizi na kadhalika kwa kutumia sisi na kupeleka mahoteli tuliyonayo. Kwa nini kwa sababu na huko hakujafanywa hivyo viwango kama Mhe. Naibu Waziri alivyoeleza tusifanye mpango kuwasaidia watu hawa wa Vitongoji hizi bidhaa zao tukazieneza katika sehemu hizi badala ya sisi kulazimika kuagizishia kutoka Bara wakati petu zinazalishwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, serikali haijashindwa kuwashughulikia wananchi juu ya bidhaa zao isipokuwa kupata taaluma tu wakulima jinsi ya kusarifu mazao yao mpaka yakafika viwango vya kuuzwa na mheshimiwa masoko hivi sasa tunayo kwa sababu mahoteli yapo, lakini tunashindwa jinsi ya kutunza bidhaa zetu.

Nitakupa mimi mfano, mimi ni mkulima vile vile tuna machungwa mengi Ndijani na embe nyingi lakini embe ile wakati inapochumwa inachumwa embe changa, hapa panataka taaluma jinsi ya embe muda gani kuzichuma. Nakumbuka mimi zamani embe zinaekwa miembeni mpaka zinag'ogwa na nyuki lakini leo embe changa halafu zinatiwa moto.

Zikishatiwa moto embe zile zinapelekwa sokoni vipi mnunuzi atavutiwa na mazao yale. Ndio tunaposema kwamba tuwe na mafunzo ya kuwasomesha wakulima ambao wawe na bidhaa njema. Leo ukenda sokoni utakuta kuna tungule zinazoitwa za masalo, tungule zile tutanunua mimi na wewe lakini hatoki mwenye hoteli akaja kununua tungule zile.

Kwa hivyo bado serikali haijashindwa lakini tumo mtiririko mzima wa kuwaelimisha wakulima wetu ili tukapata biashara zilizokuwa bora na zikawa na soko zuri.

Mhe. Farida Amour Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali dogo la nyongeza.

Mhe. Naibu Waziri pamoja na majibu mazuri na marefu uliyotupa naomba kuuliza. Kwa kuwa hakuna mfumo mzuri wa wakulima kuhifadhi mazao yao kutokana na umaskini. Jee, serikali ina

mpango gani wa kuwa na sera ya masoko ya bidhaa za kilimo itakayosimamia kuleta ufanisi katika masuala ya masoko.
Swali la pili, kwa kuwa hakuna mfumo mzuri wa utunzaji wa bidhaa hizo, jee Mhe. Naibu Waziri unaweza kutueleza ni kiasi gani bidhaa za wananchi zinavyopotea.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Mwakilishi sera imeshakuwa inatayarishwa na itakapokuwa tayari sera hiyo italetwa hapa Barazani.

Swali lake la pili, ni kweli mazao ya wakulima yanapotea na yanapotea kwa kiwango kikubwa na kama nilivyosema kuwa mimi ni mkulima tayari tathmini tushaifanya ya viwango ambavyo vya biashara haya yanayopotea.

Ukichukulia tungule ambazo wanalima jamaa zangu wa Matemwe, asilimia 42 tungule zinapotea, ukichukua machungwa ambayo tunayo kwetu kule Ndijani, asilimia 34 yanaupotevu tangu kuchumwa kwake mpaka yakafikishwa sokoni. Ukichukua samaki wavuvi asilimia 25 samaki wanapotea, kuna mananasi asilimia 33 yanapotea, embe ambazo nilizosema kuwa zinachumwa embe changa ni asilimia 49 zinapotea na kadhalika.

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Shirika la Utangazaji la Zanzibar ya 2012 pamoja na marekebisho yake

(Kusomwa kwa mara ya Pili)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Mwenyekiti: Kwa mujibu wa orodha ambayo nimeikuta hapa tuna wachangiaji 9. Tuanze basi na Mhe. Hija Hassan Hija baadae atafuatiwa na Mhe.Bikame Yussuf Hamad

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai na uzima na nikushukuru pia Mhe. Mwenyekiti, asubuhi kuwa mchangiaji wa mwanzo kwa asubuhi hii kwenye mswada huu ambao Mhe. Waziri wa Habari ametuletea.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nianze na dhana nzima ya vyombo vya habari ambapo wapo watu mbali mbali wana nadharia tofauti juu ya dhana ya vyombo vya habari. Wengine Mhe. Mwenyekiti, wamekuwa wakisema kwamba vyombo vya habari ni sauti ya umma na wengine wakisema kwamba ni kimbilio la wanyonge, wengine wakisema kwamba ni mdomo wa serikali lakini wapo pia wanaoamini kwamba vyombo vya habari ni muhimili wa nne wa dola.

Mhe. Mwenyekiti, kwa Zanzibar na mtizamo wangu zote nadharia nne hizi bado hatujazifikia. Si sauti ya umma, si kimbilio la wanyonge, si mdomo wa serikali na wala si muhimili wa nne wa

dola. Kwa mtizamo wangu Mhe. Mwenyekiti, bado nadharia hizi nne za mtazamo wa kidunia bado Zanzibar kwa upande wa vyombo vya habari hatujafikia.

Mhe. Mwenyekiti, historia ya vyombo vya habari Zanzibar imeanza zamani lakini tuna TV na redio kongwe sana. Tumekuwa tukiambiwa mara kadhaa kwamba TV ya rangi Afrika Mashariki na Kati imeanza Zanzibar. Nimefurahi sana Mhe. Rais alipokuwa akizungumza anasema kwamba, visiwa vyote vya Bara la Afrika vilikuwa vipo nyuma sana kwa tasnia hii ya vyombo vya habari, lakini hii tumekuwa sisi ni tiro kuliko wengine. Alionesha Seychelles, Maritius, Madagasca na sehemu nyengine.

Kwa hivyo ni dhahiri kwamba tumepitwa sana na wenzetu katika maendeleo haya ya vyombo vya habari. Sasa kama serikali tuna wajibu wa kujiuliza kuna nini. Kwa nini tulianza mwanzo lakini leo tumekuwa ni wa mwisho kwa upande huu.

Mhe. Mwenyekiti, vina jukumu kubwa ndani ya umma na vina kazi kubwa ya kutoa habari ambazo zinazofanyiwa utafiti na habari ambazo ni za ukweli ikiwa ni pamoja na uwajibikaji wa serikali mbele ya wananchi. Mhe. Mwenyekiti, ni tofauti sana hapa Zanzibar hata Tanzania Bara.

Vyombo vya Tanzania Bara vimekuwa vikieleza mafanikio na hata matatizo ya serikali lakini vile vile vimekuwa vikieleza mafanikio ya jamii na mtu mmoja mmoja. Kwa Zanzibar Mhe. Mwenyekiti, ni nadra mno chombo cha habari kueleza matatizo ya serikali. Ni mara chache mno na kama sijasikia hasa niseme kwamba sijawahi kusikia TV au redio ikifanya tathmini na utafiti wa utekelezaji wa bajeti za serikali kwa wananchi.

Mimi ningependa kusikia Mhe. Mwenyekiti, kwamba angalau kila mwaka wa fedha kwenye mwaka wa bajeti TV na wataalamu wetu wa redio wanafanya uchambuzi wa utekelezaji wa miradi mbali mbali ya serikali mbele ya jamii, hilo limekuwa ni jambo muhimu sana, ni kama kwamba serikali haifanyi chochote wakati wanajua serikali ndio inayokusanya kodi na kwa vile serikali inakusanya kodi lazima ilete maendeleo kwa wananchi.

Kinyume chake sasa tumekuwa tukiandaa programu za wawakilishi majimboni na wabunge kama kwamba wawakilishi na wabunge ndio wenye jukumu la kuleta maendeleo katika majimbo, wamesahau wajibu wetu kwamba sisi ni kutunga sheria na sera na kusimamia serikali. Kwa hivyo mimi wito wangu Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba tunaunda shirika hili sasa watambue kwamba wajibu wao pia ni kuisemea serikali na kuikosoa serikali. Ni yale ambayo serikali inafanya mazuri sana mbele ya jamii basi waseme wazi na yale ambayo serikali wameteleza au wamesahau kidogo redio na TV ni wajibu wao ni kuwakumbusha na kuelekeza.

Hivyo Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba lazima vyombo vya habari vyetu au wataalamu wetu wa habari watafute habari za kina zinazowahusu wananchi ikiwa ni pamoja na bajeti na matumizi ya serikali.

Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba leo ni jambo la kawaida sana waandishi wa habari pengine hata kufika mwezi mzima hawajazungumza lolote linalohusu jamii mbele ya serikali. Mimi sitaki niwalaumu kwa sababu nyenzo, vitendea kazi hata mafao yao yamekuwa yakibanwa.

Wenzangu jana wamezungumza hapa mwandishi wa habari gani atakayefanya kazi kwa ufanisi wakati hana nyenzo au vitendea kazi na hana mafao ya kutosha. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, tunakoelekea sasa shirika hili linaanzishwa kisheria na ni lazima tuangalie maslahi ya wafanyakazi wetu ili waweze kufanya kazi vizuri mbele ya shirika hili kwa maana ya redio na TV.

Mhe. Mwenyekiti, jana hapa Mhe. Hamza alikumbusha kwamba wakati tunaelekea kwenye sheria mpya na sheria imesema kwamba shirika hili litarithi madeni na kila mali ambayo shirika kongwe lilikuwepo. Nikumbushie tu kwamba ni mara tatu nne Mhe. Waziri wazo hili amekuwa akiahidi kwamba atawalipa mafao yao wale wafanyakazi wote 20 waliokwenda kufanya kazi ya kimafunzo kule nchini Uholanzi.

Lakini kisingizio sasa kwamba serikali imekosa kumbukumbu, jambo ambalo mimi sikuwa nikiamini siku zote hizo. Mhe. Mwenyekiti, sasa katika kufanya utafiti nimegundua kwamba serikali wanaijua orodha ya wafanyakazi wao na si kweli kwamba hawana kumbukumbu ya wafanyakazi waliokwenda Uholanzi.

Mimi nimepata majina na wamewahi kuwalipa baadhi ya mafao wafanyakazi hao. Kwa hivyo kiliopo Mhe. Mwenyekiti, kwamba serikali haitaki kuwalipa wafanyakazi wetu. Sasa wakati serikali inadanganya Baraza, serikali inawakandamiza wafanyakazi wetu wa habari redio na televisheni, nani atakuwa na moyo wa kufanyakazi ndani ya nchi yake, kwa nini hao akina Marini Hassan wasikimbie.

Mhe. Mwenyekiti, nasema kwamba naungana na Mhe. Hamza iwapo munataka mswada huu upite na tuamini kwamba mutawalipa wafanyakazi vizuri, orodha hii ya wafanyakazi 20 waliokwenda Uholanzi walipwe haraka iwezekanavyo.

Hii gharama si zaidi ya milioni kumi na tano. Serikali uwezo huo wanao na muwalipe wafanyakazi wetu ili tuanze ukurasa mpya wa kuwatetea kuwa watafanya kazi vizuri katika mazingira mazuri, mazingira sanifu na mazingira ambayo wataalamu wetu wa redio na habari.

Mhe. Mwenyekiti, haiwezikani kabisa miaka mitatu iliyopita kwamba serikali inatwambia haiwajui wafanyakazi waliokwenda kule, wakati orodha huu munao mpaka *voucher* ambazo wafanyakazi hao wamewahi kulipwa sehemu ya fedha hizo. Ni dhahiri kwamba serikali kupitia wizara hii wanadanganya Baraza na hawawezi kutusaidia na lengo lao ni kukandamiza sekta nzima hii ya habari ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, sasa haya yanatoka wapi. Kwa nini hatukufanikiwa kwa muda mrefu ndani ya miaka 30 tupo nyuma au miaka 40. Mhe. Mwenyekiti, haya yanatokana na uongozi wenye sifa tatu kubwa.

Uongozi ambao una sifa ya kutowajibika huzaa matunda mabovu. Uongozi ambao una sifa ya ubinafsi huzaa matunda mabovu na uongozi ambao una sifa ya kuanzisha migogoro ndani ya chombo basi uongozi huo huzaa mafanikio mabovu.

Mhe. Mwenyekiti, tayari tumeshahudia TV na redio au ZBC migongano ya kiutendaji kila siku yanatokezea, migongano ya kimaslahi kila siku yanatokezea na hivyo wanaoathirika ni Wazanzibari ambao tegemeo lao ni hili Shirika hili la Habari la Zanzibar. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, wito wangu ni kwamba tujifunze na yale yaliyotendeka mazuri tuendeleze mabaya tuyakatae ili tuende na shirika jipya ambalo linaenda katika dunia hii ya ushindani ya kila hali.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya utangulizi wangu huo wa jumla sasa niende kwenye mswada haraka haraka na nianze kwenye kifungu cha 8, "Kuanzishwa kwa Bodi ya Wakurugenzi na kazi zake na majukumu yake".

Mhe. Mwenyekiti, ninaunga mkono kabisa hoja ya Kamati ya Habari kwamba kifungu cha 8 (1) (c) wakuu wa idara ni wajumbe kutokana na nyadhifa zao, ninaunga mkono kwamba hiki kiondoke kwa sababu hatuwezi kuunda bodi ya shirika ikiwa inaongozwa na wajumbe wa idara au shirika. Mhe. Mwenyekiti, hivyo ninapendekeza kwamba kifungu cha 8 (1) (d) Mwanasheria wa Serikali kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu pia kiondoke, kwa nini kiondoke.

Tayari tumeeka katibu wa bodi, kazi yake kubwa ni kwamba awe ni mwanasheria na huyu ndio kazi yake ya kulishauri bodi katika mambo ya kisheria na pia kumbukumbu za bodi. Kwa hivyo tunataka kuweka wanasheria wawili; mmoja wa serikali kuu, mmoja wa shirika tuendeleze migongano, kwa hivyo hakuna hoja ya msingi Mhe. Mwenyekiti.

Baraza hili ni shahidi kwamba bodi zote tunaweka katibu mmoja wa bodi mwanasheria kwa ajili ya kazi za bodi. Kwa hivyo kifungu cha (d) cha Mwanasheria wa serikali kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu naomba kiondoke ili katibu wa bodi atosheleze kufanya kazi kwa uhuru, yeye ndiye mshauri wa bodi mambo yote ya kisheria na naamini kwamba huo ni uzoefu wa mashirika yote hapa ndani na nje ya nchi. Tusiweke wanasheria wawili; mmoja wa serikali kuu na mmoja wa shirika tunasababisha migongano ya kikazi. Namshauri sana Mhe. Waziri kifungu cha 8 (1) (d) kiondoke mwanasheria wa bodi.

Mhe. Mwenyekiti, lakini kifungu cha 8 (1) (f) naunga mkono wazo la kamati kwamba wajumbe wengine watatu wateuliwe na Mhe. Waziri ili kuunga ile nambari ya wajumbe wa bodi.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 8(3) mtu hawezi kuteuliwa kuwa Mwenyekiti isipokuwa awe na maarifa na uzoefu katika nyanja ya utangazaji, teknolojia ya habari, utawala, sheria ya vyombo vya habari, usimamizi wa biashara, mawasiliano ya umma na nyanja nyenginezo zinazohusiana na hayo.

Mhe. Mwenyekiti, hapa hatukuweka sifa, sifa ya kuwa una maarifa na uzoefu, kila mtu akiwa sio mwendawazimu ana maarifa na ana uzoefu wa jambo. Mhe. Hamza Hassan jana alipendekeza kwamba mtu huyo awe na digrii ya kwanza. Mimi nasema kwamba huko ni mbali ni lazima tuweke sifa ya angalau diploma, tukimpata mwenye digrii ya kwanza ni jambo zuri, lakini angalau diploma tuweze kumweka. Sifa hii ya maarifa au uzoefu wa kazi, kila mtu Mhe. Mwenyekiti, ana maarifa yake na kila mtu ana uzoefu wa kazi yake. Kwa hivyo, sio sifa inayostahiki kuwekwa katika chombo hiki.

Naendelea kusisitiza kwamba tusitunge sheria za mashirika yetu ya serikali kwa kumuangalia mtu, tuangalie taifa linakwenda wapi, maendeleo yanaelekea wapi na nchi inaelekea wapi. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 8(3) lazima mwenyekiti wa Bodi awe na sifa angalau ya diploma kama kiwango chake cha elimu.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu chengine ambacho nataka kukiangalia ni kifungu cha 10(1) mpaka (j), napendekeza kwamba tuongeze kifungu (h), ili bodi miongoni mwa kazi zake ni kupokea maoni ya umma katika shughuli za utangazaji, yaani *public opinion*. Lazima bodi tuwape uwezo, wawe na kazi ya kupokea maoni ya umma na hiyo ndio kazi ya vyombo vya habari, lazima *public hearing* iwepo na hiyo iwe ni kazi ya bodi kusikiliza na kupokea maoni ya jamii ili kuwasilisha katika shirika kwa ajili ya kazi hiyo. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, napendekeza tuongeze kifungu (h) kama kazi ya bodi ili kupokea maoni ya umma katika shughuli za utangazaji, yaani *public opinion*.

Mhe. Mwenyekiti, sehemu nyengine ambayo ningependa kuchangia ni sehemu ya 4 kuhusu uongozi na wafanyakazi wa shirika. Bado Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 11(1) (a) tumeweka hapa sifa za kuteuliwa kwa Mkurugenzi Mkuu, imesema tu kwamba aliyehitimu kutoka katika Chuo Kikuu kinachotambulika au katika chuo kinacholingana na hicho Mhe. Mwenyekiti, bado hatujaweka sifa.

Mhe. Mwenyekiti, nilisema hapa jana kwamba kwa Kiingereza tumesema ni *graduate*, bila utata hiyo ni kuanzia digrii ya kwanza, kwa hivyo na hapa tuweke wazi wazi Kiswahili kwamba mtu huyo awe na sifa angalau ya digrii ya kwanza ili aweze kuwa Mkurugenzi Mkuu wa shirika hili, tuache kutunga sheria ambazo zinajifichaficha kwa ajili ya kutoa mwanya kwa watu ambao hawana nia njema kuja kufanya yale mambo ambayo yanagongana.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile naunga mkono kifungu cha 11(d) sifa nyengine yoyote kama atakavyoamua Rais basi huyo mtu ateuliwe. Mimi nadhani kifungu cha (a) (b) (c) kimeweka bayana sifa za kuwa mkurugenzi. Kwa hivyo, tusimuongezee Rais kazi nyengine ya kumuona vile anavyofaa. Kwa hivyo, naomba hicho cha (d) kiondoke.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu chengine ni kifungu cha 13(2) kinachosema kwamba;

Kifungu cha 13(2)

> "Hakuna kitu au jambo lolote litakalofanywa au kuachwa kufanywa na mfanyakazi wa shirika au mtu mwengine yeyote aliye chini ya maelekezo ya shirika kitakachofanywa, ikiwa kitu au jambo hilo lilifanywa kwa nia njema au vyenginevyo".

Mhe. Mwenyekiti, kifungu hiki kinakusudia kwamba kinga dhidi ya pengine wafanyakazi au waandishi wa habari. Mimi nadhani tuweke uhuru, unapotaka kulinda haki yako ni lazima ulinde na haki ya mwenzako. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, tusimzuie mwandishi wa habari kwamba asishtakiwe hata kama atafanya jambo kwa nia isiyokuwa nzuri, ili tukafanya kama tunamlinda, ni lazima tuweke wazi kwamba kila mtu anayefanya kazi, basi sheria ichukue mkondo wake na hivyo ndivyo hasa dhana ile ya kwamba hakuna mtu aliye juu ya sheria itakayofanya kazi, lazima tusubiri kifungu hiki cha kuwalinda watu, hii inadhihirisha wazi kwamba tutasababisha

matatizo kuwa watu wengine watafanya makosa kwa makusudi kwa ajili ya kukomoana au kufanya matendo yasiyokuwa mazuri.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 15(2), Mkurugenzi Mkuu sio zaidi ya miezi 3 kabla ya kumalizika kwa mwaka wa fedha, ataandaa na kuwasilisha kwa bodi, makisio na mapato ya matumizi yake kwa mwaka unaofuata ambayo baada ya kuidhinishwa na bodi itawasilishwa kwa Waziri.

Mhe. Mwenyekiti, hapa sina tatizo, lakini naomba tuongeze kuwa tuujue mwaka wa fedha ni upi. Kuna wengine mwaka wa fedha unakuwa ni Januari mpaka Disemba, kuna wengine wanafuata mwaka wa fedha wa serikali wa Juni mpaka Julai. Kwa hivyo, naomba Mhe. Mwenyekiti, hapa Mhe. Waziri akubali aweke maneno ambayo yanaonesha mwaka wa fedha wa bodi utakuwa ni mwezi gani hadi mwezi gani.
Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo ningechangia kwa haraka ni kifungu cha 7. Kifungu cha 7(2) naomba ninukuu;

Kifungu cha 7(2)

> "Uamuzi wa bodi unaweza kufanywa bila ya kikao kwa kusambaza nyaraka zinazohusika kwa ujumbe na maamuzi ya wajumbe walio wengi yataheshimiwa".

Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba kifungu hiki kiondoke. Tumechagua bodi na tumeweka idadi ya vikao vya bodi. Sasa leo unatuambia kwamba bodi wapigiane simu tu wasambaze nyaraka basi watakuwa wameamua. Nadhani tunataka kufuga wavivu wasiowajibika, na hivyo hatuwezi kurejea tena kifungu hiki. Bado naamini kwamba watu wanaendelea kufanya kazi kwa kutumia mitandao, lakini nadhani hatujafikia huko. Sasa mimi naomba kifungu kiondoke ili isije ikasababisha Mwenyekiti wa Bodi akaandaa ajenda, akasambaza na watu wakatia saini na hatimaye ikawa ndio maamuzi ya bodi, lazima tufuate vikao. Mhe. Waziri nakushauri kwamba kifungu cha 7(2) kiondoke hakina maslahi katika sheria hii.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu chengine ni kifungu cha 9 kinachosema;

> "Wajumbe wa bodi watalipwa posho, ada na malipo mengine kwa ajili ya kujikimu kama itakavyoamuliwa na waziri".

Mhe. Mwenyekiti, mimi nashauri kwamba wajumbe wa bodi walipwe posho, tena iongezwe, "wajumbe wa bodi walipwe posho la vikao vyake" na hii ada, malipo, mengineyo kwa ajili ya kujikimu tuyafute. Tusimlazimishe mtu kumlipa posho, halafu tukamwambia ujikimu, ununue mswaki, ununue pete na viatu. Mpe posho mwenyewe afanye kwa mujibu wa maslahi yake. Kwa hivyo, maneno haya kujikimu na malazi, nadhani hayana maana tusimfundishe mtu, ilimradi tuweke posho kwa maslahi ya mjumbe wa bodi, tena yeye mwenyewe akiamua kujikimu, akiamua kumgaia mtu, akiamua kuweka benki ni maamuzi yake mwenyewe, lakini tusiongeze maneno. Kwa sababu wasi wasi wangu Mhe. Mwenyekiti, hapa pataendelea kuliwa pesa za shirika kwa sababu mambo mliyoyaweka ada, malipo ya kujikimu ni mambo mengi.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, nashauri kwamba wajumbe wa bodi watalipwa posho la vikao vyake kama itakavyoamuliwa na waziri, hili sina pingamizi nalo. Lakini tusilazimishe kwamba lazima posho hiyo iwe ni kujikimu, kulala na nauli, tusichambue.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo ningeshauri ni bodi inaweza kwa kuweka masharti ya maelekezo mazuri ya kuteua kamati kama inavyoona inafaa, katika utekelezaji wa kazi au kuishauri bodi katika jambo ambalo bodi italielekeza.

Mhe. Mwenyekiti, hili ni jambo zuri lakini tuwe na umakini. Tusiwe tukawa rahisi bodi kuandaa kamati kila wakati, tukifanya hilo na bila sababu za msingi, bodi itasababisha kupotea kwa fedha nyingi za shirika. Kwa hivyo, kamati iundwe pale ambapo panahitajika kuundwa kwa kamati, sio kila mara kamati iundwe na bodi.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 11 kinasema;

Kifungu cha 11

> "Kutakuwa na mkutano mkuu wa mwaka wa bodi na wizara husika kuangalia na kutathmini juu ya watendaji wa shirika".

Mhe. Mwenyekiti, maneno haya naomba yaondoke, bodi na wizara kukaa ni utaratibu wa kawaida, ni utaratibu wa ndani. Tusiweke kuwa lazima iwe ni sheria kwamba kila mwaka ufanywe mkutano mkuu baina ya bodi na wizara. Huo ni utaratibu wa ndani wa kuitana na kufanya kikao. Tukifanya hivi maana yake hiyo fedha za shirika maana yake ni fedha za vikao tu. Kwa hivyo, kifungu cha 11 naomba kiondoke.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo na kama Mhe. Waziri atanikubalia maombi yangu, basi nitaunga mkono mswada huu. Nakushukuru.

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia asubuhi hii tukakutana hapa kwa majukumu mbali mbali ya serikali.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza napenda kukushukuru na wewe kwa kunipa nafasi hii kuweza kuchangia mawazo yangu machache katika mswada huu wa sheria ya kuanzisha Shirika la Utangazaji Zanzibar, kazi, majukumu na utawala wake pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Pili Mhe. Mwenyekiti, niwapongeze sana wizara hii ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kwa kuleta mswada huu ambao kuwa shirika lilikuwepo kwa kiasi fulani, lakini shirika hili lilikuwa kama ni mdomo mkuu wa serikali. Kwa kuona hilo serikali ikaleta mswada huu kwa kulianzisha upya shirika hili kufanya kazi zake na majukumu yale na utawala wake ambao kuwa watajiendesha wao wenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kuanza nianze kusema kwamba mswada huu wa kuanzishwa kwa shirika basi nauunga mkono kwa asilimia mia, nikiwa nina imani kwamba shirika hili la

utangazaji litakuwa na jukumu kubwa la kutoa elimu kwa jamii, kama walivyoelekeza wao katika sheria yao hii.

Mhe. Mwenyekiti, watu wa kale wanasema kuwa *choyo ni kuona*. Unapoona kitu kinapendeza basi pale na wewe utajenga uchoyo na sisi Wazanzibari tumekuwa na choyo kwa kuona mashirika binafsi yanavyofanikiwa katika kutoa huduma zao hizi za utangazaji kwa asilimia mia, ukilinganisha na shirika letu lililokuwepo la utangazaji ambalo lilikuwa limemilikiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, sote ni mashahidi kwenye vyombo vyetu vya habari, kwenye televisheni na redio. Kuna watu ambao hawana hata bajeti, tuchukulie mfano wa TV Imani na Redio Imani, zinavyotoka hewani masaa 24. Kitu ambacho kwa kupitia Shirika letu la Utangazaji Zanzibar lilivyokuwa dhaifu katika kutoa matangazo yake.

Mhe. Mwenyekiti, sisi tulikuwa tunajiuliza kulikoni kwamba watu binafsi wanaweza wakafanya jambo lao na wakapata lile wanalolikusudia kufanikiwa, ukilinganisha na serikali ambayo kuwa ina mambo yake kamili. Sasa Mhe. Mwenyekiti, sisi tunaona choyo sana Wazanzibari, tunaona choyo sana na ndio maana tukasema labda kupitia kuanzishwa upya shirika hili na kupewa kazi zake na majukumu yake, basi litaweza kutufikisha pale ambapo kuwa na sisi tunategemea tufike.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika kifungu cha 5 ambacho kinazungumzia malengo ya shirika ni kutoa taarifa, elimu na burudani kwa jamii. Ni kweli haya ndio malengo makubwa ya shughuli za utangazaji. Lakini kutoa taarifa gani, tunaomba Mhe. Mwenyekiti, kutoa taarifa zilizokuwa ni sahihi, kutoa taarifa kwa wakati unaostahiki, sio kutoa taarifa tu kwa wakati wanaotaka vile vyombo vya habari vitoe. Kwa hivyo, mimi ningeomba sana shirika litakapoanzishwa basi kitu hiki wakipe umuhimu mkubwa kwa hili lengo la kutoa taarifa kwa wakati unaostahiki.

Mhe. Mwenyekiti, tuchukue mfano ulio hai. Ilipotokea ajali ya hii meli ya MV Skagit, basi chombo cha kwanza kilichotoa taarifa ni redio Noor kama hivi. Lakini tulipofungua ZBC kuna watu wanacheza taarabu. Kwa hivyo, ukiangalia tukio lile linatokea katika kisiwa hiki hiki, lakini katika taarifa unakwenda kusikia katika vyombo binafsi ndio vinatoa taarifa ile na wakati chombo chetu cha serikali tunacho, kinakuja kutoa taarifa baada ya tukio lile limeshapita kwa masaa. Sasa hii Mhe. Mwenyekiti, haipendezi. Kwa hivyo, tunaomba taarifa zitolewe kwa wakati na pale linapotokea tukio, tunaomba shirika hili litakapoanzishwa basi wawe makini kwa shughuli zao, wasiwe tayari kukaa kuwatafuta mawakala wa kuwapa taarifa baada ya matukio kwishatokea, wao wenyewe wajishughulishe kwa kutafuta taarifa mbali mbali ya matukio yanayotokea katika kisiwa chetu hiki cha Zanzibar.

Pia Mhe. Mwenyekiti, pamoja na kutoa taarifa lakini pia na elimu, elimu ni kitu muhimu sasa hivi kwa wananchi wote. Kwa hivyo, saa zote tusitegemee tu kupewa elimu na vyombo vyengine vinavyotoka Bara na kwengineko. Sisi tunataka tupewa elimu na chombo chetu hiki ambacho ndio tegemeo la Wazanzibari, hasa katika maeneo ya vijijini ambapo tuna kilio kikubwa cha kuikosa *ZBC* televisheni, hili ni tatizo kwa nini. Kwa nini tukose matangazo ya *ZBC* na hata hizo redio.

Mhe. Mwenyekiti, Unaweza ukainunua ile redio hapa Unguja na ukiifungua utafikiria labda uko pale kwenye kituo. Lakini redio ile ukiichukua ukenda nayo Pemba kwenye baadhi ya maeneo sauti zao zinakuwa hazitoki vizuri. Kwa hivyo, elimu ni kitu muhimu kwa jamii. Kwa hivyo, tunaomba sana shirika litakapoanzishwa basi wajipange kwa umakini ulio mzuri zaidi.
Jengine Mhe. Mwenyekiti, tunaomba sio wanaleta vipindi vyao hata ikifika saa fulani wanafunga, kwa nini wafunge wana kazi gani na kazi zao ni za kutafuta habari na kutoa elimu pamoja na mambo mengine. Kwa nini wenzao waweze kuendesha vipindi vyao kwa muda wote wa masaa mangapi halafu wao washindwe. Kwa hivyo, tunaliomba shirika litakapoanzishwa shirika hili basi liweze kupanga vipindi vyake vizuri viwe vya redio au viwe vya televisheni, ili muda wote watu waweze kusikia ZBC yao ikitoa taarifa kwa wananchi wake.

Mhe. Mwenyekiti, jengine kuna kifungu cha 12(2) ambacho kinasema;

Kifungu cha 12(2)

> "bila ya kuathiri masharti ya sheria ya Utumishi wa Umma, Wakuu wa Idara watateuliwa na bodi na kila mkuu wa idara atakuwa ni mtu mwenye taaluma husika na uzoefu wa kutosha wa kutekeleza majukumu katika idara husika".

Mhe. Mwenyekiti, mimi hapa nilikuwa na ushauri, kwa nini wakuu hawa wa idara wateuliwe na hii bodi, wasiweze kuteuliwa na waziri mwenye dhamana ya wizara hii na ukizingatia pengine hawa watakuwa ni waajiriwa wa serikali, kwa nini wasiweze kuteuliwa na waziri. Naomba kifungu hiki nipewe ufafanuzi kama sheria inaruhusu, basi ningeomba wakuu hawa wa idara wateuliwe na waziri mwenye dhamana ya wizara hii.

Kwa hayo machache Mhe. Mwenyekiti, nasema tena kwamba naunga mkono mswada huu kwa asilimia mia kwa mia, ahsante.

Mhe. Hamad Masoud Hamad: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nikushukuru kwa kunipa nafasi hii asubuhi ya leo kuweza kuchangia machache tu katika mswada huu muhimu sana, wa kuanzisha Shirika la Utangazaji Zanzibar, kazi zake, majukumu yake, utawala pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa nimpongeze Mhe. Waziri kwa kuuleta mswada huu. Mhe. Mwenyekiti, mimi nimefarijika sana kwa sababu kuletwa kwa mswada huu kunaendana kabisa na ilani ya uchaguzi ya chama changu ya mwaka 2005/2010. Kwa bahati nzuri nilikuwa napitia *documents*, hiyo ilani yenyewe ninayo, sitosoma kila kitu, lakini nitasema pale ambapo panalingana na uanzishwaji wa hili.

CUF itaziunganisha pamoja Idara ya Televisheni ya Zanzibar (TVZ) na Idara ya Sauti ya Tanzania Zanzibar STZ na kuunda Shirika la Utangazaji Zanzibar. *Zanzibar Broadcasting Corporation*. Kwa hivyo kuletwa kwa mswada huu inaendana kabisa na sera yetu.

Mhe. Mwenyekiti, tumekuwa na TV kwa muda mrefu kabla ya nchi nyingi za Afrika, tena TV ya rangi hapa Zanzibar. Lakini kama alivyosema Mhe. Mwakilishi wa Mji Mkongwe jana kwamba suala la redio hapa Zanzibar lina zaidi ya miaka 100. Lakini pamoja na kuwa na vyombo hivi TV na redio bado hatujawa. Kuna wenzetu wameanzisha vyombo hivi hasa televisheni chini ya

miaka 10 iliyopita, lakini leo wametupita na tofauti yetu sisi na wao ni ardhi na mbingu, hatufanani na hata kimoja chetu sisi na chao wao. Hao ndio wameanzisha juzi.

Mhe. Mwenyekiti, kuja kwa sheria hii na baada ya malalamiko makubwa, tunategemea kwamba sheria hii itakuwa imekamilika na itatuondoa hapa tulipo katika aibu hii, maana mimi nasema ni aibu, kwamba tumeanza TV na redio kwa miaka mingi iliyopita, lakini leo tunashindwa na walioanza jana.

Mhe. Mwenyekiti, sijui tuna mapungufu gani hadi kila tunachokianzisha sisi kwa muda mrefu tunashindwa na walioanzisha kwa hivi karibuni. Lakini mimi najua *procedure* ya kuanzisha vyombo hivi. Vinaanza na wizara yenyewe tena pengine baada ya sisi Wawakilishi hapa kuzungumzia jambo hilo. Lakini kuna kamati, nikisema wizara pia kamati ya uongozi wa wizara inakaa kitako, inapeleka mswada gani, mswada huu unakwenda kwa Mhe. Mwanasheria Mkuu, unakwenda kwenye kamati ya makatibu wakuu, unapitia Baraza la Mapinduzi, unakuja kwenye kamati zile za Baraza na hatimaye ndio unaletwa hapa.

Kwa hivyo, kuna mambo mengi ambayo walioupitia mswada huu wameyaona. Lakini na sisi hapa kwa sababu ndio wajibu wetu na kazi yetu kutunga sheria, *infact* sheria inatungwa kila mahala sisi hapa ndio tunao-*finalize* kwamba sheria iweko hivi. Kwa hivyo mimi kufutwa kwa vifungu vingi humu na kuandikwa vyengine, saa nyengine kidogo vinanipa wasi wasi, kwa sababu *procedure* zote hizo wizara, Baraza la Mapinduzi, kamati ya makatibu wakuu na kamati nyengine kama hawakuviona kweli.

Mhe. Mwenyekiti, ninachokusudia kusema ni nini, ni kwamba leo nimeona karatasi napewa hapa kuna vifungu kama; kifungu cha 8, kifungu cha 5(c) na kifungu cha 18 hivyo vyote vimefutwa na vimewekwa vitu vidogo vidogo, maana yake kifungu cha mswada kilichopo, halafu kuna marekebisho ya kifungu cha suala hili. Vingekuwa vifungu hivi havijarekebishwa. Maana yake hii ni karatasi ya leo asubuhi basi ningekuwa na mchango mkubwa sana.

Mhe. Mwenyekiti, kuna *BBC* yaani *British Broadcasting Corporation*, kuna *TBC* yaani *Tanzania Broadcasting Corporation*, kuna ZBC ya Zimbabwe, kuna *ZBC* ya Zambia na leo sisi hapa tuna *ZBC*. Kuna *KBC* yaani *Kenya Broadcasting Corporation*. Mimi suala langu ni hili, kwa sababu tunaanzisha sheria hii na tunataka tuondoke hapa tulipo itupeleke mahali ambapo tutakwenda na wakati, hakuna ubaya wowote kuiga kitu kizuri.

Mhe. Mwenyekiti, namuuliza Mhe. Waziri, katika kutunga sheria hii wamechukua miswada ya mashirika gani *BBC, KBC, TBC, ZBC* nakusudia Zimbabwe, Zambia na kwengineko. Ni vitu gani ambavyo mule walivichukua wakaviweka hapa. Kwa sababu ni lazima twende na wakati kwa kukaa tu sisi wenyewe tu hapa, kuna vitu kama hatujapata pahala pengine pa kuangalia wenzetu wamefanyaje mpaka wakafika huko. Kwa hivyo, Mhe. Waziri atakapokuja hapa aniambie kwamba tulichukua sheria hii na hii, na katika hii tulichukua hiki na hiki. Kama hawakufanya hivyo basi bado tuko pale pale. Sio vibaya hata kidogo ku-*copy* vitu ambavyo ni vya msingi.

Mhe. Mwenyekiti, miongoni mwa mambo ambayo yanarudisha nyuma vyombo vyetu vya habari ni moja ni muhali. Jana kuna mmoja katika waandishi aliniuliza wewe unataka kuchangia basi

aliniambia nakuomba katika utakayozungumza na hilo usilisahau, nilimuuliza lipi, aliniambia kama baada ya sheria hii kutunga na kukamilika na kufanya kazi, kama uongozi ni ule ule uliopo sasa basi isiitwe *ZBC* na iitwe *MBC*. Sasa mimi nilimuuliza hii M maana yake nini, alitaja jina la mtu na wala sitaki kumtaja.

Mhe. Mwenyekiti, nafikiri nasikika maana yake nini, ni kwamba sheria hii hata iwe nzuri kiasi gani kwa uongozi uliopo hivi sasa kwenye *ZBC*, basi bora isiitwe *ZBC*, kwa sababu Zanzibar ni kubwa ni hadhi yake na bora iwe *MBC*. Kwa hivyo, 'M' ni jina la mtu ambaye yumo kwenye *administration* ya *ZBC* mtamtafuta na mimi hakuniambia. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, baada ya dibaji hiyo fupi niende kidogo kwenye mswada wenyewe, naomba nianze kifungu cha 6 kuhusu kazi za shirika zitakuwa na zimetajwa pale a, b, c, d, e, f, g na h. Sasa mimi naomba miongoni mwa kazi za shirika hili iwe ni kile kifungu cha 18(e) na hilo la kwanza.

Vile vile kifungu cha 5 kuhusu malengo ya shirika yatakuwa ni, kuna lengo liko 18(a) lakini halikuwekwa kama lengo. Kwa hivyo, 18(a) iingizwe hapa kwenye kifungu cha 5 kuhusu malengo ya shirika yatakuwa ni.

Nikiendelea na mchango wangu kwenye kifungu cha 8(f) hichi kinazungumzia kuanzishwa kwa Bodi ya Wakurugenzi wa Shirika ambalo itakuwa na wajumbe wafuatao. Sasa kifungu cha 8(f) Mhe. Mwenyekiti naomba kunukuu.

Kifungu cha 8(f) kinaeleza hivi:-

> "Wajumbe wengine wasiozidi wawili kutoka kwa watu maarufu wa Zanzibar ambao wameteuliwa na waziri wenye ujuzi, taaluma na uzoefu katika nyanja za utangazaji, teknolojia, utawala, sheria ya vyombo vya habari, taaluma ya biashara, fedha na uandishi wa habari".

Mhe. Mwenyekiti, mimi hii nataka iwe *re-written*, kwa sababu ukisema watu maarufu wa Zanzibar ambao wameteuliwa na waziri wenye ujuzi. Kwa hivyo, nataka iandikwe wasiozidi wawili kutoka watu maarufu wa Zanzibar ambao wana ujuzi, halafu hii walioteuliwa na waziri ije mwisho ni uandishi. *(Makofi)*

Kifungu cha 9(2) Mhe. Mwenyekiti naomba kunukuu.

Kifungu cha 9(2) kinaeleza hivi:-

> "Katibu wa Bodi atakuwa na wajibu:
>
> (i) Kupanga taratibu za shughuli za bodi.
> (ii) Kuweka kumbukumbu za kufanya kazi nyengine zozote kama bodi itakavyoelekeza.

Mhe. Mwenyekiti, mimi zote hizi sijaziona kama ni kazi za Katibu wa Bodi, kwa sababu ukisema kuweka kumbukumbu ina maana nyingi, kuna watu kazi yao ni kusoma kumbukumbu pale, yaani anapewa na kuweka sasa hii ndio kazi yake. Kwa kweli mimi nafikiri kazi za katibu wa Bodi ni kuandika kumbukumbu, yaani *minutes* na halafu kuziweka ni kazi nyengine.

Kwa hivyo, hapa pia ningeomba kama nilivyosema kwamba sheria hii imepita katika ngazi tofauti tena ngazi kubwa ambazo ni za wazito, kwa sababu BLM ndio *organ* ya juu kabisa katika nchi hii yenye maamuzi, lakini ule ni muhimili mmoja na muhimili mwengine ni sisi Baraza la Wawakilishi. Sasa huyu Katibu wa Bodi awekewe kazi zake hasa mahsusi, kwamba ni moja, mbili, tatu na hizi sio kama si kazi zake, lakini ile mahsusi hasa anayotakiwa afanye hapa haijatajwa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 10(2) hii imeelezwa vizuri sana na Mhe. Ismail Jussa Ladhu, lakini na mimi naomba kuweka msisitizo, naomba kunukuu Mhe. Mwenyekiti.
Kifungu cha 10(2) kinaeleza hivi:-

> "Bodi inaweza kukasimu uwezo wa mamlaka yake kwa mjumbe yeyote …"

Mhe. Mwenyekiti, bodi ina majukumu makubwa tena ni bodi inayoendesha shirika, kwa sababu bodi ndio shirika na shirika ndio bodi. Sasa bodi hii itakasimu majukumu au mamlaka yake kwa mtu yeyote maana yake ni mtu mmoja tu, kwa sababu ni mtu yeyote nadhani hapa tungefanya marekebisho makubwa, ili hii tusiiruhusu.

Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba niende kwenye kifungu cha 18(e) hii ni katika kutekeleza majukumu yake kama ilivyoelekezwa chini ya sheria, kwamba bodi itakuwa na Sera ya Uhariri kama kawaida. Lakini kazi imeandikwa ni kukusanya, kutafuta, kuchambua na kutangaza.

Mhe. Mwenyekiti, hii vile vile nadhani ingekuwa *re-written*, kwa sababu unakusanya na halafu unatafuta, mimi nafikiri kwanza tungetafuta na halafu tukusanye na baadaye ndio tuchambue na hili ni suala la maandishi.

Jambo jengine ambalo naomba Waheshimiwa Wajumbe ni suala zima la vikao vya bodi, ambapo vikao vya bodi hapa vimeelezwa kwenye kifungu cha 3 ukurasa wa 298 Mhe. Mwenyekiti naomba kunukuu.

Kifungu cha 3 kinaeleza hivi:-

> "Bodi itakuwa na vikao visivyozidi vinne kwa kila mwaka wa fedha, lakini ikitokea dharura Bodi inaweza kukutana"

Mhe. Mwenyekiti, nafikiri hapa tungewawekea hasa kwa sababu kwa *statement* hii, basi wanaweza kufanya vikao vyote hivi kwa mwezi mmoja nasema kwa *statement* hii. Kwa hivyo, ni vyema kusema hasa kila baada ya muda gani iwe ni kwa miezi mitatu au kadri ambavyo itakavyoamuliwa, lakini ukiweka hivi *blank* k, basi wajumbe watasema wacha tufanye vikao vyote hivi vitatu au vinne. Sasa hichi ni kitu ambacho naomba Mhe. Mwenyekiti kiangalie na kiwekwe vizuri kama ambavyo sheria nyengine tumekuwa tukiziwekea muda wao maalum.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyokwambia kwamba marekebisho mengi yamefanywa. Kwa hivyo, nataka niishukuru sana wizara kwa kuleta mswada huu *in time*. Lakini naomba niwakumbushe kwamba baada ya mswada huu kukamilika na kuanza kutumika, ili utufikishe hapo tunapotaka na tuondokane na aibu tuliyonayo TV yetu kupewa jina ambalo halistahiki, basi ilifika wakati hapa TVZ ilikuwa ikiitwa TV Kitangi, maana yake kila ukifungua kuna habari hizo tu na redio yetu ilikuwa ikiitwa Redio bi Kidude na mnakumbuka nyote.

Kwa hivyo, sasa tunataka *ZBC* kweli, yaani *Zanzibar Broadcasting Corporation* na ikitajwa Zanzibar kila mtu aseme *yes*, kwamba kuna Shirika la Utangazaji la Zanzibar lenye hadhi yake kama Zanzibar ilivyo na hadhi yake. Sasa katika hili wafanyakazi wana umuhimu wake sana.

Kwa kweli *ZBC* iliopo hivi sasa kuna migogoro hata ya wenyewe kwa wenyewe, yaani watu wanagombea ofisi, wewe usikae hapa, wewe ondoka hapa na wewe kaa hivi, yaani migogoro ambayo imefika kila mahala, pia ubinafsi umezidi. Mhe. Mwenyekiti, kama tunataka tutoke hapa tulipo na twende na wakati na huu ni wakati wa *digital* na kila siku tunahimizwa hapa na mambo ya *analogue* yaachwe.

Kwa hivyo, kama tunaacha *analogue*, basi tuachane pia na ubinafsi na wala tusirudi huko tulikokuwa hapa lililetwa *satellite dish* hapa na Marekani, na likafungwa pale kwa vishindo miaka miwili tunashinda tu kwamba litumike au lisitumike, kwa sababu likitumika kuna *films* na watoto wetu wanaharibika, mambo haya. *(Makofi)*

Nadhani Mhe. Mwenyekiti tutafute wataalamu hata kwa kuwakodi kama hatuna. Kwa mfano, jana Mhe. Ismail Jussa Ladhu alisema vizuri na alitaja mpaka watangazaji, ambao ni watangazaji mashuhuri duniani, ukienda Redio ya Ujerumani tunaweza kwenda kuwatoa, ukienda *BBC* ndio hao hao.

Vile vile hata kesho kutwa hapa *TBC* si tulikuwa naye Marin Hassan Marin tena namtaja makusudi na leo *is the one of the star announcer* wa *TBC* alikuwepo hapa *TVZ*, palitokea nini yeye anajua. Kutokana na hali hiyo, bila ya kuacha muhali, ubaguzi, majungu, familia *ZBC* tutatunga sheria mia hapa, isipokuwa tukate jongoo kwa meno.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nakushukuru sana na ninaunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii na mimi nikaweza kuchangia mswada huu muhimu sana kwa chombo hichi ambacho kimeshaanzishwa hapo nyuma, ambapo kilianzishwa bila ya kuwa na sheria iliyopitishwa hapa na ilianzishwa kwa mujibu wa Tangazo la Sheria Nam. 111/2 kama ilivyoelezwa ili liweze kuanza shughuli zake.

Mhe. Mwenyekiti, niliyotaka kuchangia hapa kama unavyojua jana kidogo nilikuwa maadhura sikuwepo, kwa hivyo michango mingi sikuweza kuisikia ya Waheshimiwa Wajumbe wenzangu.

Kwa hivyo, kwenye mchango wangu naweza kuchangia mambo ambayo tayari yameshazungumzwa na wenzangu na hapo nitakuwa ninasisitiza au nitachangia mambo mengine

mapya. Lakini kwa bahati sikupata bahati ya michango ya wenzangu ya akina Mhe. Ismail Jussa Ladhu.

Mhe. Mwenyekiti, nilipofika nimepewa karatasi hii ya marekebisho yaliyofanywa na Mwenyekiti na Kamati pia nimepewa karatasi nyengine ambayo imeandikwa jaduweli ya marekebisho Kanuni ya 84(2) (a) ya Baraza la Wawakilishi na nimejaribu kuyasoma.

Kwa kweli inaonekana *document* hii ni muhimu katika marekebisho, lakini imekosa sifa, kwa sababu ni *document* muhimu ambayo tunataka tutumie haya yaliomo humu kwa ajili ya kutunga sheria na wala haina saini wala kielelezo chochote huku mwisho.

Kutokana na hali hiyo, nimekuwa na mashaka na *document* hii kuweza kuitumia, kwa sababu ni kosa kubwa na nimeangalia *document* zote. Kwa mfano, hii ya Mwenyekiti imewekwa saini na Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari, kwa hiyo tunayakubali marekebisho haya, lakini hata na huu mswada wenyewe unawekwa saini na Mhe. Waziri anayehusika.

Lakini *document* hii ambayo imefanya marekebisho haina saini na wala hatuijui ameifanya nani. Kwa hivyo, inaweza kuleta mashaka au ikakataliwa wakati wowote. Sasa Mhe. Mwenyekiti, sijui Mhe. Waziri wakati atakapokuja atatueleza nini juu ya jambo hili.

Jambo jengine nimemuangalia Mhe. Waziri anayehusika na Wizara hii yuko wapi, nimeambiwa amesafiri. Lakini Mhe. Mwenyekiti, nadhani sisi hatuko *serious*, kwa sababu kama leo tunapitisha sheria hii ambapo Mhe. Waziri wa wizara hii angetakiwa awepo aone na asikilize *concern* za Waheshimiwa Wajumbe na asikilize marekebisho ya Wajumbe, lakini kuna waziri anayekaimu wizara hii, kwa kweli hatuko *serious*. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mimi ningekuwepo tokea jana basi ningewashawishi Waheshimiwa Wajumbe wenzangu turejeshe mswada huu, ili tumsubiri Mhe. Waziri kwa ajili ya kuja kujadili kwa pamoja, kwa sababu kwa vyovyote vile Mhe. Waziri yeye ndiye atakayesimamia sheria hii.

Kwa kweli unajua jambo la kuambiwa si la kuwepo na kusimamia ni tofauti. Kwa mfano, unapomwambia mtu neno basi yule unayemtuma anaweza kulibadilisha na hapa tunafanya kitu kikubwa, tunatunga sheria ambayo inahitaji marekebisho na leo humu yamo marekebisho mengi ambayo yangehitaji mwenyewe Mhe. Waziri awepo.

Kwa hivyo, mimi nathubutu kusema Mhe. Mwenyekiti kwamba bado suala hili lina kasoro kubwa na tutaonekana tunaripuaripua na wala hatujui wakati gani twende wapi na wakati gani tuwepo na wakati gani tufanye nini.

Mhe. Mwenyekiti, tunaanzisha Shirika la *ZBC*, ambalo shirika hili kama nilivyotangulia kusema kwamba lipo tayari limeshaanzishwa. Kwa kweli shirika hili ni muhimu kwa sababu linasimamia vyombo ambavyo vinatoa habari kwa umma, yaani vinatuhabarisha.

Vyombo hivi kama vitakuwa vizuri, basi vitatoa elimu kwa umma na kama vitatuharibikia maana yake vitapotosha umma na ndio maana tunasema kwamba tunatayarisha sheria ya

kuanzisha shirika muhimu kwa wananchi, kwa sababu kwa vyovyote itakavyokuwa shirika hili ndio itakuwa mdomo wa serikali.

Tunavyo vyombo vingi. Kwa mfano, tunazo televisheni pamoja na redio za binafsi, lakini *ZBC* itakuwa ndio mdomo wa serikali. Wakati mmoja Mhe. Mwenyekiti kuna Siku ile ya Wajinga Duniani (*April Fool*), nadhani kila inapofika tarehe 01 mwezi wa Aprili na *ZBC* na wakati ule ilikuwa ni Sauti ya Tanzania Zanzibar, kwamba wananchi wanaitwa pale Rahaleo waende wakachukue mchele na vitu vyengine.

Mhe. Mwenyekiti, asubuhi watu wamejaa pale na wengine wametoka mashamba na kuvamia pale na wala hawakujua kwamba siku ile ni siku ya wajinga duniani, lakini imetoka kwenye chombo kikubwa cha serikali, yaani chombo cha umma.

Kwa hivyo, hiyo inaonesha ni namna gani kwamba chombo hichi ni muhimu. Kwa maana hiyo, Mhe. Mwenyekiti chombo hichi kitakapoanzishwa kinahitaji kupewa uwezo mkubwa, kwa kweli serikali ni lazima shirika hili liliwezeshe katika mambo mbali mbali. Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa shirika leo liko taabani na sote ni mashahidi, bajeti yake ni finyu na wala haina uwezo wa kuliendeleza. Kwa mfano, tutakuwa tunalaumu na ndio wajibu kulaumiana. *(Makofi)*

Lakini unapomlaumu mtu kufanya jambo, basi lazima kwanza umuwezeshe, ili aweze kufanya shughuli zake. Mhe. Mwenyekiti, juzi Mhe. Rais wakati alipokuwa akifungua mtambo wa *digital* alizungumzia juu ya kukosekana kwa vipindi kutokana na ukosefu wa umeme na akasema tu kwamba kuona majenereta yapo katika kila eneo, lakini unapokatika umeme na matangazo hakuna, na mwenzangu ananiambia hapa na fedha za mafuta zinatoka. Sasa inakuwaje leo vyombo vyetu hivi vinakatisha matangazo kutokana na umeme.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nimejaribu kufuatilia, lakini nimeona kwamba kweli fedha zipo isipokuwa hazitoshi kwa ajili ya kuendesha majenereta na huu ndio ukweli ulivyo. Kiwango cha fedha kinachohitajika kwa ajili ya kuendesha jenereta ni kikubwa mno na wala hakilingani na *OC* wanazopewa.

Kwa hivyo, ili tufanye mambo mazuri Mhe. Mwenyekiti, basi lazima tuiwezeshe *ZBC* na tutakapoliwezesha *ZBC* hapo sasa ndipo tutakapoweza kufuatilia na kuona jinsi gani jambo hili linavyokwenda na bajeti yao ni finyu na wala haiwezi kutekeleza jambo lolote. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na hayo, ili shirika letu liende vizuri ni lazima tuwapatie maslahi mazuri wafanyakazi wa shirika hili. Kwa kweli wafanyakazi wa Shirika hili la *ZBC* wanafanya kazi katika mazingira magumu hata zile posho zinazostahiki basi wanazikosa. *(Makofi)*

Kwa mfano, leo Mhe. Mwenyekiti tunao humu wafanyakazi wa televisheni na redio wanafanya kazi humu tumefanya vikao na tunaendelea na vikao sijawauliza, lakini naamini ukiwauliza kama tayari posho kwa ajili ya kazi hii ngumu wanayoifanya wameshapewa hiyo ndogo ya shilingi 2,000/= wameshapewa, majibu itakuwa hakuna. *(Makofi)*

Lakini sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi Mhe. Mwenyekiti *Alhamdulillah* tunapewa posho zetu hata hatujaanza vikao, lakini je wenzetu hawa tunaoshirikiana nao kuanzia asubuhi mpaka usiku wao wako katika hali gani. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, redio na televisheni zetu tumeziongezea uwezo wa kufanya kazi. Hivi sasa redio na televisheni zinafanya kazi kwa muda wa masaa 24. Hebu tujiulize Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, wakati atakapokuja aje kunieleza, kwamba wale wafanyakazi wanaofanya kazi usiku pale Televisheni ya Zanzibar wanapewa maposho kwa ajili ya kukesha pale tena nataka aje na jibu sahihi, kwamba wanapewa maposho yao kwa ajili ya kazi zile za kukesha na sisi tunalala majumbani kwetu *alhamdulillah*. *(Makofi)*

Sasa wao wapo pale wanafanya kazi usiku, yaani kuanzia saa 2 za usiku mpaka saa 2 za asubuhi, yaani wanafanya kazi zaidi ya ule muda uliowekwa wa utumishi wa masaa 8, kuanzia saa 2 usiku mpaka saa 2 za asubuhi ndio wanatoka, je tunawawezesha kupata maposho yao ya kujikimu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, *ZBC* inahitaji kuwa na *scheme of service* ya wafanyakazi wake na hili halikwepeki lazima kuwe na s*cheme of service,* kwa ajili ya maslahi ya wafanyakazi wake, ili wapate maslahi yanayolingana na kazi zao. *(Makofi)*

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, kukipatia chombo hichi vitendea kazi na wala hakina vitendea kazi vya kutosha, hakuna vyombo vya usafiri na hawa shughuli zao ni za kufuatilia kwenda huku na kule kwa ajili ya kutafuta habari. Kwa mfano, leo ukiuliza wanazo gari ngapi, pikipiki ngapi ni aibu, lakini hata majengo yao yamechakaa vibaya. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, juzi nilialikwa pale Idara ya Televisheni kwenye kipindi, kwa kweli ni aibu kwa sababu jengo limechakaa halina rangi utafikiri limejengwa miaka mingapi, halikadhalika utakapokwenda redio na wala jengo lile si la zamani sana. Lakini wanashindwa kuyafanyia matengenezo kutokana na ufinyu wa bajeti.

Kwa hivyo, lazima bajeti ya chombo hichi iongezwe katika bajeti ijayo Mhe. Mwenyekiti tunataka kuona kwamba kunakuwa na ongezeko la kutosha, ili kuviwezesha vyombo hivi viweze kufanya shughuli zao. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu huu ni wakati wa ushindani, na vyombo hivi vinakabiliwa na ushindani mkubwa. Kwa mfano, kuna redio na televisheni za binafsi zipo vizuri na zinakwenda na wakati, yaani zinakwenda na ule mfumo wa kileo wa *digital* na wameondokana kabisa na *analogue*.

Sasa na chombo hichi tukiwezeshe kiendane na wakati na ili kuweze kwenda na wakati, basi ni lazima tukiwezeshe pamoja na hali yetu ngumu lakini tukiwezeshe na wafanyakazi wa chombo hichi basi wajione kwamba sasa wametoka kwenye Idara za Serikali na sasa wako kwenye chombo hichi cha mashirika, yaani waone tofauti kwa sababu hivi sasa hawaoni tofauti yoyote, pale walipokuwa idara na hivi sasa ni shirika hakuna tofauti yoyote mambo ndiyo yale yale. Kwa hivyo, tunataka waone mabadiliko kwamba kweli sasa ZBC ni Shirika la Serikali na limetungiwa na sheria, kuliko vile ilivyokuwa mwanzo.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo sasa niingie kwenye bodi, lakini kabla sijaingia kwenye bodi nitakuja kwenye kifungu ambacho kimeongezwa. Kuna kifungu kimeongezwa "Waziri anaweza" halafu kuna 13(1) (a), (b) na (c). Ni kifungu kizuri kwa mtazamo wa wenzetu wamekiongeza lakini kina athari yake. Kina athari vipi?

Tunaanzisha Bodi za Wakurugenzi kama ilivyoanzishwa Bodi ya Wakurugenzi katika sheria hii kifungu cha 8(1) na imetajwa kazi zake, Katibu wa bodi halkadhalika na mambo mengine. Lakini tunapoanzisha hizi bodi tunataka ziwe bodi zenye mamlaka zifanye shughuli zake kwa mujibu wa sheria za bodi. Tuzigeuze bodi hizi kama ni Idara za serikali na hili ndio tatizo katika nchi hii.

Mhe. Mwenyekiti, hivi karibuni Kamati yangu ya Fedha, Biashara na Kilimo tulifanya ziara katika Wizara ya Biashara Viwanda na Masoko. Kuna Bodi ile ya ZSTC ambayo tumeipitisha hapa kwa mujibu wa sheria. Imepewa majukumu chungu nzima. Tulivyokwenda kwenye Kamati tukawaambia wenzetu wa Wizara ya Biashara kwamba iacheni Bodi ya ZSTC ifanye kazi zake, watafute soko la karafuu, wauze karafuu, wafanye kila ambalo lipo kwa mujibu wa sheria.

Lakini cha kusikitisha Mheshimiwa Bodi hii imekuwa ikiingiliwa mno na Wizara. Watu wanakwenda wakitafuta wateja wa karafuu wamekuwa madalali sasa, kwenda kutafuta masoko ya karafuu kuwaletea watu wa bodi ya ZSTC. Mpaka tunafika pahala tunajiuliza kuna nini hapa kwenye karafuu mpaka watu unapokuja msimu wa karafuu wanahangaika huku na huku kutafuta masoko. Tuwaachie Bodi ya Shirika la ZSTC itafute masoko, iuze karafuu. Wizara isubiri yanapotokea matatizo wawaelekeze. Lakini vyenginevyo vyovyote tutasababisha hasara.

Mhe. Mwenyekiti, leo Shirika la ZSTC tayari limeshaingia hasara ya zaidi ya dola laki sita, ni hasara kubwa. Hili linatokana na vyombo hivi kuingiliwa katika majukumu yake. Kwa kweli tunapoanzisha bodi kwa mujibu wa sheria tuziachie bodi hizi zifanye kazi. Wizara au Waziri anayehusika aingilie pale zinapoharibika. Kwa sababu mambo haya yana kawaida mnapofanya jambo likifanikiwa basi bodi itapongezwa. Lakini linapoharibika basi bodi italaumiwa.

Mhe. Mwenyekiti, juzi tumepata taarifa yule mama Mkurugenzi wa ZSTC amepanda *pressure* kalazwa hospitalini. Ni mwana mama mzuri tu anafanya kazi vizuri na ni muaminifu. Lakini haya mambo ya kuingiliaingilia kila wakati tunawapandisha *pressure* wale tuliowapa dhamana ya kufanya kazi. Tuwaachie hawa tuliowapa dhamana wafanye kazi zao kwa mujibu wa sheria.
Mhe. Mwenyekiti, kwenye marekebisho, haya yamempa Waziri kifungu (a) (b) kinasema hivi:-

Kifungu cha 3(1) "Kutoa maelekezo ya jumla au maalum kwa bodi kuhusiana na utendaji wa shughuli za shirika na matumizi ya uwezo wa shirika, bodi itasimamia maelekezo hayo."

Ukiangalia katika hali ya kawaida ni maelezo mazuri ya Waziri kuweza kusimamia Bodi zake na Wizara zake. Je, katika utekelezaji vifungu hivi ndivyo vinavyoleta matatizo katika sheria. Tumekua na kawaida kuyaingilia zaidi majukumu ya bodi na kuvitumia vifungu hivi visivyo. Mimi nakubaliana kifungu ni kizuri tu. Lakini je, matumizi yake yanatumika vizuri. Mimi naomba kifungu hiki kifanyiwe marekebisho. Kimetoa mamlaka makubwa sana juu ya bodi, mamlaka mazito. Ili basi *at least* kiendane na hali halisi ilivyo.

Mhe. Mwenyekiti, kwenye hii bodi ya zamani na hii mpya ambayo tumeletewa inaonesha kuna wajumbe wasiopungua wanane kwa mujibu wa huu muundo wa sasa. Lakini kwa mujibu wa sheria ya mitaji ya umma bodi hizi za mashirika hazitakiwi kuwa na wajumbe wanaozidi sita. lakini hapa kuna wajumbe wasiopongua wanane. Kwa hivyo hii sheria tutakayoitunga hapa itakuwa inakwenda kinyume na sheria tuliyoipitisha wenyewe hapa ya sheria ya mitaji ya umma juu ya kuanzisha bodi za mashirika. Kwa hivyo mapendekezo yangu sasa nasema wajumbe hawa wapunguzwe na wabakie sita kama ilivyo sheria ya mitaji ya umma.

Mhe. Mwenyekiti, kuna mjumbe mmoja huyu mjumbe wa (c) atakayeteuliwa na Waziri kutokana na mapendekezo ya jumuiya ya wafanyabiashara, wakulima wenye viwanda na masoko. Mimi mjumbe huyu Mhe. Mwenyekiti, sioni umuhimu wa kuwekwa. Kweli tunahimiza hizi tunazoziita PPP. Lakini wajumbe hawa wanakuwa wanaingizwa katika bodi zile ambazo wao wana uhusiano nao. Unapomuingiza kwenye PPP masuala haya ya kilimo, mambo ya viwanda, mjumbe katika Bodi ya Utangazaji hivi tutapata wazo gani katika eneo hili. Au hili ni eneo la biashara kwa kuwa tumesema Shirika litakwenda kibiashara.

Mimi nakubaliana nao sana na mimi napiga kelele sana waingizwe kwenye bodi lakini zile bodi ambazo zinawahusu. Kwa mfano bodi hizi za ZSTC, kwa sababu ni bodi zinazosimamia masuala ya biashara na mambo mengine. Kwa hivyo mjumbe huyu katika hao wajumbe wa kupunguzwa huyu apungue. Na wajumbe wengine hawa ambao wamepewa mamlaka Mhe. Waziri kuteua, ameambiwa ateue wajumbe watatu, miongoni mwa watu maarufu. Hapa Mhe. Waziri sasa tumpe wajumbe wawili baadala ya watatu.

Isitoshe katika kifungu cha 8(2) kinasema:

> “Wajumbe waliotajwa chini ya kifungu kidogo cha (d) na (e) cha kifungu hichi, watateuliwa na Waziri baada ya kushauriana na Mkuu wa taasisi husika”

Mimi naomba kifungu hiki kidogo cha (2) kifutwe. Tunaposema kwamba Mjumbe mmoja ni mwanasheria wa serikali kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali basi Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali itoe mwanasheria pale kumpeleka katika bodi.

Lakini kuna mjumbe mwengine ningehitaji maelezo Mhe. Waziri utakapokuja kutoka Wizara inayohusiana na mambo ya Fedha kuna mantiki gani? Kwenye mitaji ya umma Mhe. Waziri wa Mitaji ya Umma hapa anasema, basi sina tatizo. Nilikuwa najiuliza huyu mjumbe huyu ameingizwaje hapa lakini kumbe ni mitaji ya umma.

Mhe. Mjumbe mwenzangu hapa alizungumzia juu mjumbe kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu na kusema kwamba wanasheria watakuwa wawili. Mimi nilivyoisoma naona mwanasheria bado ni mmoja kwenye bodi, isipokuwa yule mmoja atakuwa ni Katibu na kwa mujibu wa sheria hii atakuwa si mjumbe wa bodi.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, kuna eneo hili la kwenye jaduweli kwenye kifungu cha 4 kinasema:

> "Mwenyekiti akiwa hayupo katika Kikao cha Bodi wajumbe waliohudhuria kikao watamchagua mjumbe mmoja miongoni mwao kuwa mwenyekiti, kuendesha kikao kwa muda wa mjumbe huyo, atakuwa na jukumu na kutoa taarifa"

Mhe. Mwenyekiti, mimi sikubaliani na maelezo haya kwamba achaguliwe mjumbe mmoja miongoni mwao, awepo Makamu mwenyekiti wa bodi. Sheria nyingi tunazopitisha hapa kutakuwa na Mwenyekiti na makamu mwenyekiti. Makamu mwenyekiti atateuliwa na wale wajumbe watakapokaa, sio kuchagua mjumbe yoyote. Kwa sababu tukitoa fursa hii maana yake leo kama Mwenyekiti akiwa hayupo atakuwa huyu mara atakuwa huyu mara atakuwa huyu. Awepo makamu mwenyekiti, sheria iseme kwamba:

> Bodi itamteua Makamu Mwenyekiti ambaye Mwenyekiti anapokuwa hayupo maana yake Makamu Mwenyekiti ataweza kuendesha kikao. Lakini pia katibu wa Bodi atapata nafasi ya kushauriana naye pindipo kama Mwenyekiti hayupo.

Unapoacha tu kwamba hakuna makamu mwenyekiti, kwamba mjumbe yeyote anaweza kuwa Makamu mwenyekiti. Huyu katibu inapotokea makamu mwenyekiti hayupo atashauriana naye nani. Kwa hivyo bodi hii iwe na Makamu mwenyekiti, iseme hawa kwamba kutakuwa na makamu mwenyekiti ambaye atateuliwa na bodi, anapokuwa mwenyekiti hayupo yeye sasa anachukua nafasi hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nikubaliane na hoja ya Mhe. Mjumbe mmoja aliyesema kifungu cha 7(2) kifutwe, ambacho kinasema kwamba uamuzi wa bodi unaweza kufanywa bila ya kikao na kusambaza nyaraka zinazohusikana na wajumbe na maamuzi ya wajumbe walio wengi yataheshimiwa.

Mimi nakubaliana na Mjumbe aliyejenga hoja hii, mimi niliona lakini naisisitiza, kwamba haiwezekani maamuzi ya bodi yakaamuliwa kila mmoja kwa upande wake. Maamuzi yoyote ya jambo yanafikiwa baada ya majadiliano. Haiwezekani mtu akakaa nyumbani kwake akasoma akisha akamua, hajasikiliza *comment* za wenziwe. Maamuzi yote ya chombo kama hiki yanapatikana kwa majadiliano, kwa hivyo kifungu hiki kifutwe, kitolewe. Zaidi tukizingatia kwamba bado nafasi ya kuitisha vikao vya dharura ipo wanapohisi kuna jambo muhimu linahitaji mamuzi, aitishe vikao vya dharura tu, kwani ana hofu ya nini mpaka mtu apelekewe ki- *memo* nyumbani kwake.

Mhe. Mwenyekiti, Kifungu cha 12 (1) kinasema Shirika litakuwa na idara na vitengo kama vitakavyoamuliwa na bodi. Nafahamu kwamba tuna vyombo viwili vya habari labda pengine tunaweza tukaongeza na kingine, tuna televisheni na redio. Hizi sasa zitakuwa ndio idara zetu. Tutakuwa na Mkurugenzi wa Idara ya Televisheni na Mkurugenzi wa Idara ya Redio. Sasa tutakaposema kwamba Bodi itaweza kuanzisha tena idara, idara hizi tutazitoa wapi. Mimi nahisi kifungu hiki kinaweza kikafika pahala kikawa – *demote* hawa wakurugenzi wa hivi vyombo viwili.

Nadhani sheria iseme au isitoe mwanya vyenginevyo labda pale tutakapoanzisha chombo kingine iseme tu kwamba Idara zitakuwa ni mbili; ya Idara ya Redio na Idara ya Televisheni lakini bodi inaweza ikaanzisha idara nyengine, pale kitakapoanzishwa chombo kingine. Kwa sababu hii inanitia hofu kwamba Mheshimiwa wanaweza kuwepo tena wakuu wa idara mbali

mbali wakati shirika letu hili limesimamia vyombo hivi viwili. Kwa hivyo sheria hii isitoe mwanya kwa kuanzisha idara nyengine, vitengo ni sawa lakini hizi idara ziendelee kubakia idara mbili ya televisheni na ya redio zitakuwa chini ya Mkurugenzi Mkuu wa ZBC. Nadhani hapo tutakuwa tunakwenda sawa na Wakurugenzi wale watakuwa na hadhi na kwa mujibu wa kusimamia majukumu yao.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu 9(3) naomba nikinukuu kinasema:

Kifungu 9(3) "Ikiwa Katibu hatokuwepo kutokana na ugonjwa au kutokana na sababu nyengine yeyote hawezi kutekeleza majukumu yake, bodi itateua mfanyakazi yeyote mwengine wa shirika kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya Katibu kwa muda ambao katibu hatokuwepo mpaka nafasi yake itakapojazwa."

Mhe. Mwenyekiti, mimi naona bodi itateua mfanyakazi yeyote mwengine. Kifungu hiki kidogo kinahitaji kuangaliwa upya. Kwa sababu tunaweza kumchukua mtu mwengine yeyote tu kwa utashi tukamuweka pale. Mhe. Waziri kifungu hiki kinahitaji kuangaliwa upya, tusitoe nafasi kama hii ili anapoondoka katibu tumpate katibu mwenye sifa ambaye anaweza kufanya kazi za ukatibu.

Mhe. Hamad Masoud Hamad alisema kwamba sheria hizi zinapitia mikondo mingi mpaka kufikia hapa kwetu tunapozijadili. Lakini kuna mambo ambayo kwa kweli yanahitaji wenzetu wawe wanayaona. Kwa sababu ni mambo muhimu katika kutunga sheria zetu na katika kusimamia mambo yetu haya.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo basi niunge mkono hoja pale Mhe. Waziri anayekaimu Wizara hii atakapofanya masahihisho juu ya yale maeneo ambayo nimeyazungumza na kama atatoa maelezo ya kuridhisha juu ya maeneo haya basi sina tatizo Mhe. Mwenyekiti, nitayakubali. Lakini pale ambapo sitopata maelezo ya kuridhisha itabidi liwe jambo jengine. Ahsante Mwenyekiti.

Mhe. Ashura Sharifu Ally: Ahsante sana Mhe. Mwenyikiti, awali ya yote sina budi nimshukuru Mwenyezimungu Mtukufu (S.W) aliyetujaalia uhai, uzima tukawepo hapa kutekeleza majukumu yetu kwa maslahi ya taifa letu. Lakini pia nikushukuru na wewe Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipatia nami nafasi hii ya kutoa mchango wangu.

Mhe. Mwenyekiti, nampongeza Waziri pamoja na watendaji wake kwa kuamua wakati huu kutuletea Mswada huu wa Sheria ya Shirika la Utangazaji Zanzibar. Maamuzi haya ya kuviunganisha vyombo hivi viwili vya televisheni pamoja na redio kwa kweli hili ni kupiga hatua kutokana na wakati huu tuliokuwa nao. Hili nadhani limekuja kufuta ile Sheria ambayo ilikuwepo ya 111ya mwaka 2011.

Mhe. Mwenyekiti, katika sheria hii endapo itakuwa sheria ningependa nikumbushe kwa wakati huu ambapo hali tuliyonayo iko haja ya serikali ya kuleta au kuunga mkono mabadiliko ya Shirika hili la Utangazaji Zanzibar. Umefika wakati wa kuona kwamba Shirika hili ni lazima kwanza kuangaliwa ili lijipange kwa kuwa na vitendea kazi. Ni wazi kwamba sote tunafahamu

hilo kwamba lina ufinyu mkubwa wa vitendea kazi. Lakini pia lina matatizo makubwa ya wafanyakazi katika maposho na mishahara yao.

Mhe. Mwenyekiti, hili shirika tunasema kwamba litakuwa ni shirika la kibiashara ambalo linalazimika liwe na viwango vya kitaifa na kimataifa. Hivyo basi shirika hili tumesema litakuwa ni shirika la umma. Kwa hivyo ipo haja ya kuleta mabadiliko makubwa kabisa katika shirika hili kwa wafanyakazi wake. Msingi huu wa mabadiliko katika vyombo vya habari Zanzibar ni hatua moja ya maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, vyombo vya habari popote pale duniani vinanafasi pana kabisa katika chachu ya maendeleo ya taifa. Nidhahiri kwamba mambo mengi ambayo yanafanyika ni uwazi mkubwa kwamba lazima vyombo vya habari vipatikane. Kuna mambo mengi ambayo yanafanyika bila ya kupatikana taarifa zake kwa usasahihi wake na kujua nadhani haitawezekana kabisa kuweza kufikia malengo. Shirika hili kwa kwetu Zanzibar lina nafasi pana pia ya kukuza demokrasia na usawa katika habari.

Shirika hili liwe na uwezekano mkubwa wa kufuata misingi ya haki, usawa, uwazi, ufanisi, uwajibikaji na kujenga utawala bora katika sekta ya habari. Pamoja na hayo lakini pia ni kukidhi mahitaji ya wananchi wa Zanzibar katika sekta hii muhimu ya habari. Hivyo basi isiwe sehemu ya kikundi cha watu wachache tu. Hiyo itakuwa ni kukiuka maadili. Lakini kwa kuwa ni shirika la umma basi taarifa zake zinapaswa ziwe na mabadiliko ya kweli yaendane na wakati husika, pahala na matokeo yenyewe.

Nadhani sote ni mashahidi wakati wa tokeo la ajali ya meli zetu taarifa zilipatikana katika vyombo vyengine vya nje vya habari Zanzibar, kisichokuwa chombo hichi cha serikali. Ndio maana nikaanza kusema kwamba iko haja ya kuliletea mabadiliko ya kweli Serikali kuliwezesha ili wafanyakazi wake waweze kufanya kazi saa 24 lakini kwa kuwezeshwa.
Mhe. Mwenyekiti, tumeshuhudia MV. Spice Islander inazama lakini taarifa zake zilipatikana kupitia katika Zenji FM wakati tukiwa na televisheni yetu na redio yetu ya serikali. Lakini ilishindwa kuzitoa taarifa hizo na zikaja baadaye. Hii ni aibu, jambo ambalo linawagusa wananchi moja kwa moja nadhani wananchi nafurahia zaidi kuona kwamba serikali inakuwa ya mwanzo kutoa taarifa yake kupitia vyombo vyake.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kusema kwamba katika hivi vyombo vya habari iko haja kubwa ya kupatikana habari ambazo zina usahihi, usawa lakini pia zinazoendana na mila na desturi katika sehemu ya uburudishaji. Imekuwa ni ajabu sasa katika televisheni zetu kuona michezo ya ajabu ambayo haiendani na mila na desturi na utamaduni wa Kizanzibari. Hii nadhani kwa mila na utamaduni, desturi kama tujuavyo kila nchi ina mila zake, ina utamaduni wake, ina utaratibu wake. Iko haja michezo ambayo inaonyeshwa iwe inakighi haja kwa Wazanzibari wenyewe kwa rika tofauti watoto, vijana na wazee.

Tuna historia kwamba Zanzibar ilianzisha televisheni kwa muda mrefu nyuma. Kwa kweli napongeza sana pale mwanzo jinsi tulivyoanza naye. Kulikuwa na utamaduni sisi watoto tukienda kwenye televisheni basi kulikuwa na kipindi cha watoto na kinapomalizika tu basi kunakuwa na utamaduni maalum na watoto hao kuondoka hapo na baadae kuletwa vipindi vya

watu wazima ambavyo navyo pia ni vya mafunzo na pia vinaendana sambamba na utamaduni wetu.

Baada ya kwisha kuyasema hayo Mhe. Mwenyekiti, kama utangulizi wangu basi sasa niingie kwenye huu muswada. Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye ukurasa wa 294 katika kifungu cha 9(3) hapa inasema kwamba, 'ikiwa katibu hatokuwepo kutokana na ugonjwa au kutokana na sababu nyengine yoyote hawezi kutekeleza majukumu yake, bodi itateua mfanyakazi yoyote mwengine wa Shirika'. Hapa sasa, hapa Mhe. Mwenyekiti mimi nisingependa awe mfanyakazi yoyote bali awe mfanyakazi mwenye sifa ili aweze kutekeleza jukumu hilo.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea nije kwenye sehemu ya nne ambayo ipo kwenye ukurasa wa 295 katika kifungu cha 11(2) kuna neno hapa linasema, 'mtu atakuwa' hapa kusiwe na mtu atakuwa na badala yake pia katika marekebisho ya kamati sijaiona hiyo, kwa hivyo nasema kwamba mtu atakayekuwa na sifa hizo naomba iwe hivyo.

Mhe. Mwenyekiti nikiendelea tena katika hii hii sehemu ya nne 2(c) anasema kwamba 'mwenye uzoefu na maarifa'. Mimi hapa Mhe. Mwenyekiti, kusema kwamba mtu atakuwa na maarifa kama wenzangu walivyotangulia wamesema kwamba sote nadhani kila mmoja ana maarifa juu ya shughuli yake, lakini ingetajwa kwamba mwenye elimu.

Baada ya kutoka hapo Mhe. Mwenyekiti, nateremka chini hapa kwenye sifa nyengine hapa (d) 'sifa nyengine yoyote kama itakavyoamuliwa na Rais'. Hapa Mhe. Mwenyekiti na mimi nasema kwamba tumpunguzie Rais majukumu makubwa. Nadhani sifa hizi ambazo zilitangulia huku zilikuwa zinatosha, lakini tusimpe tena Rais nafasi hii ya kumpa majukumu mazito haya wakati sifa hizi tayari tumeshazikamilisha hapa, nadhani inatosha sana tumpunguzie sana Rais wetu ana kazi kubwa na ngumu kabisa. Tukisema tu kwamba Rais afikirie na yeye sifa nyengine atakavyoamua yeye, nadhani haitakuwa imekaa vizuri, lakini nadhani tuziache hizi (a) mpaka (c) na hizi nyengine tuziache kama zilivyo. Labda tukifute hichi kifungu cha (d).

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea hapa katika ukurasa 298 hapa kuna kifungu cha 19 kinasema kwamba, 'waziri atatunga kanuni'. Mhe. Mwenyekiti, hapa napenda kumkumbusha Mhe. Waziri ili aweze kuleta ufanisi wa kweli katika Shirika hili basi aharakishe sana kutunga kanuni hizi ili ziweze kumuongoza katika utendaji wake wa kazi. Nadhani kama atachelewa kama sheria nyengine zilivyo, kwa sababu kuna sheria zimekuja mpaka zimefika tena kuja kuzifanyia marekebisho hazina kanuni zina miaka 9 na 10. Nimuombe tu Mhe. Waziri hapa aharakishe sana kuweza kuzitunga hizi kanuni na nadhani Shirika hili ndipo litapoweza kupata ufanisi na kupata njia hasa sahihi ya kuweza kufuatwa.

Mhe. Mwenyekiti, hapa katika jadueli sasa ukurasa huu wa 298 katika kifungu cha 2 kwenye jadueli, anasema hapa, iwapo mjumbe yoyote atashindwa kuhudhuria vikao 3 mfululizo vya bodi bila ya kuwa na sababu za msingi, bodi itatoa taarifa kwa waziri na waziri naye atafuta uteuzi wake na atateua mwengine. Lakini hapa atakaa ofisini. Mhe. Mwenyekiti hapa mimi ningeona kwamba ingependeza zaidi kwamba Waziri atateua mtu mwengine ambaye atakuwa mjumbe wa bodi kwa muda uliobakia, nadhani ingekaa vizuri zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa wengi wa wajumbe wameshatoa mchango wao wa kutosha na kuvipitia vifungu vingi kabisa na kutoa ufafanuzi wa kina na mambo mengine mengi ambayo nilikuwa nimeya-*note* hapa tayari wajumbe wameshayafanyia ufafanuzi wa kina na nafsi yangu iliridhika, hivyo nisingependa niendelee bali na mimi niseme kwamba naunga mkono na kuwatakia kheri kubwa katika kutumia sheria hii itakapopitishwa na shirika kulitakia ufanisi wa kina ili kuona kwamba tunaigandua Zanzibar katika mfumo wa kihabari ambao umeganda kwa muda mrefu bila kuweza kutekeleza kazi zake kwa ufanisi, kwa kuwawezesha wafanyakazi wake, vitendea kazi na shirika hili kuwa huru kufanya kazi popote pale bila kuingiliwa uhuru wao na mtu yoyote. Habari zao ziwe zinatoka ama za kisiasa, kiuchumi na kiutendaji alimradi tu wasivunje sheria bila ya ubaguzi wowote.

Baada ya kwisha kuyasema hayo Mhe. Mwenyekiti mimi naunga mkono hoja hii kwa asilimia 100.

Mhe. Abdalla Mohammed Ali: Mhe. Mwenyekiti, na mimi ninashukuru kunipatia fursa kusema machache adhuhuri hii katika hoja iliyoko mbele yetu. Kama alivyomaliza au alivyosema aliyenitangulia kwamba mengi yameshasemwa kwa hiyo sisi tutabakia na machache tu lakini na sisi ni wajibu wetu wa kusema yale ambayo tunahisi yatatupeleka mbele.

Mhe. Mwenyekiti, imekuwa ni kawaida yetu kwamba tunaleta sheria ya kuanzisha aidha shirika au mambo mengine tofauti tofauti. Lakini kinachojitokeza ni kwamba kabla ya kuanzisha sheria ile au kabla kuja na sheria ya kuanzisha shirika fulani huwa hatuangalii kasoro zetu, ufanisi wetu katika hilo ambalo tunataka kuliendeleza. Juzi tulikuwa tunachangia kuanzishwa kwa Shirika la Meli na wengi walisema lakini mchangiaji wa mwisho alimaliza kwa kusema kwamba, kwa nini tuendelee kuwa na Shirika lile ambalo lilikabidhiwa karibu meli nne lakini limeshindwa kuchangia chochote katika utayarishaji wa kununua hii meli mpya.

Alikuwa na hoja na mimi ninajiuliza tunataka kuanzisha Shirika ambalo nyuma utendaji upo tunapata habari kwa njia ya televisheni na tunapata habari kwa njia ya redio. Lakini leo tunasema aa tuje na sheria mpya ya kuanzisha shirika, lakini je tunataka kuunda chombo chengine kipya zaidi ambacho labda kitakuwa ni kikubwa zaidi lakini *foundation* yake ni ile ile ya nyumba ndogo ya chini sio nyumba ya ghorofa. Nina imani kwamba tukija kunyanyua ghorofa basi *foundation* itabomoka. Mhe. Mwenyekiti haya mazoea napenda serikali tuyaondoe. Kama tunakuja na kitu kipya basi tuje na kitu kipya, wale waliokuwepo kwa maoni yangu katika hivi vitengo walishindwa lakini nina wasiwasi kwamba wale wale ndio tutakaokujawakuta wanaendesha hilo shirika ambalo tunalitegemea liwe hivyo.

Madhumuni ya kuanzisha shirika hili ninafikiria ni mazuri lakini je tutaweza kufikia huko? Tumeunganisha nguvu kwa kusema kwamba televisheni sasa iwe pamoja na redio kwenda pamoja huku ndiko kutakotusaidia kwenda mbele.

Mhe. Mwenyekiti jana nilipokuwa ninamsikiliza balozi wa Norway alisema kitu pale lakini kiingereza changu sijui kama nilimkamata vizuri au vipi. Yeye alisema kwamba kama tunataka kwenda haraka utakwenda peke yako yaani hakuna mtu atakayekuunga mkono kwenda haraka. Lakini kama unataka kwenda mbele basi tutakwenda pamoja hivyo ndivyo alivyosema. Sasa

mimi ni imani yangu kwamba kuanzisha shirika hili kwa kuunganisha vyombo vyetu hivi viwili ni kama tunakwenda pamoja ili twende mbele na sio kwenda haraka haraka.

Kihistoria Mhe. Mwenyekiti, Shirika la ZBC lipo tuna televisheni na tuna redio, lakini cha kushangaza hata kama wengine walisema kwamba televisheni hizi zipo zamani sana na wengine wanafika hadi kujisifia kwamba *the second coloured television* yaani televisheni ya rangi ya pili kwa Afrika hii, lakini utendaji wake umekuwa ni zero hakuna maendeleo yoyote tuliyoyaona katika televisheni hii na redio ni vile vile. Tumefika wakati kisiwa kimoja cha nchi hii kwa muda karibu wa miezi sita ikawa hakuna hasa upatikanaji wa habari kama hii. Lakini leo tunakuja hapa tunasema tunataka kuanzisha Shirika, je shirika hili kweli litaweza kumudu mambo kama hayo.

Lakini mimi Mhe. Mwenyekiti nimeanza kutoka imani hii leo hapa tunasema tunahama na ulimwengu unahama kutoka *analogue* unaingia katika mfumo mpya. Lakini hadi leo Mhe. Mwenyekiti bado hatujaiona hiyo nyumba mpya ya kuhamia. Wenzetu waliokwisha kuwa tayari wameshatutangulia wao wameshaingia mapema mno katika huo mfumo tunaoutaka. Sasa leo hapa tunasema tunaunga shirika ambalo linataka kujihudumia wenyewe kiutendaji tuko tiro. Mimi imani yangu tulipokuwa huduma hii ya matangazo tunaipata bure, basi watu walikimbilia kule sehemu ambazo wanatoa ada fulani ili wazipate hii wakaikimbia.

Hivi leo tunataka kuanzisha shirika hili ambalo kwa imani yangu tutakuwa huduma tunailipia, watu kweli watajiunga, na malipo haya ndio yatakayosaidia kuliendesha shirika, watu wangapi watakuwa na moyo kwenda katika kitengo hiki Mhe. Mwenyekiti. Hivi sasa tumeshapata dalili mbovu kwamba hili shirika litashindwa. Hivyo tunavyotarajia viwepo havipo hadi hii leo watu wameshajiunga zamani katika mitandao mengine. Na kuendesha katika shirika hili kutategemea fedha. Mhe. Mwenyekiti mimi ninakata tamaa mapema kwamba uongozi ulioko utakuwa ni ule ule na umeshindwa na nakata tamaa kwamba hilo shirika lishachelewa, kwamba watakaokuja hivi sasa watawakuta wenzao wameshawahi soko na hasa tukiangalia hata huo utendaji wao basi haupo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka niwakumbushe tu kuna mwaka mmoja nilikuwepo nchi moja ya Uingereza, wao wana mashirika mengi yale ya utangazaji na yanajiendesha kwa mfumo kama huu tuliokusudia. Moja katika mashirika hayo ni BBC nilikuwepo pale katika kipindi kimoja cha majira ya baridi na nilibahatika kuwa ni mmoja ya wanaofagia zile ofisi pale. Sasa kuna siku moja nilikwenda katika semina moja lakini mwandishi mmoja wa habari akawa anaeleza pale kwamba, naomba ninukuu yale ambayo niliyoyasikia siku hiyo aliyoyatoa kwa lugha ya kiingereza. "*Is commercial enterprise and exists to make profit it cannot exist for long without making a profit" Sasa* leo soko lote sasa hivi limeshachukuliwa na washirika wengine wanaotoa matangazo katika nchi hii, hivyo tukianzisha shirika hili nani tutampata wa kuweza kupata hiyo *profit* ya kuliendesha shirika.

Lakini huyu alimalizia kwa kusema *of course you have got to give the profit, you have got to give the public what it want otherwise you go out of business.* Kwamba wewe hutoweza kuwapa wananchi kile wanachokihitaji Mhe. Mwenyekiti basi wewe utakuwa nje ya biashara. Sasa wasiwasi wangu kwamba kwa vile hawana chochote walichotuandalia, wataendesha biashara vipi na hivyo vipindi vyao havina mvuto kwa mwananchi yoyote nani atakwenda kujiunga.

Sasa nia ni nzuri lakini je, hawa wenzetu wameshajiandaa kukabiliana na ushindani? Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti naomba nikinukuu kifungu hiki masharti mengineyo, "kuhakikisha kila mwananchi ana haki ya kupata taarifa wakati wote wa matukio mbali mbali nchini na duniani kote". Hivyo ninajiuliza hivyo shirika hili litakuwa na uwezo wa kuwapatia wananchi huduma hiyo. Mhe. Mwenyekiti, wananchi wana haiba tofauti tofauti. Lakini sijui katika huo mfumo ambao tutaingia tutaweza kweli kuwatosheleza wananchi na kuwapatia hicho ambacho wanakihitaji kama *public* haitotosheka na kile kinachotoka basi *business* haipo, na kwa maana hiyo shirika litaanza kunywea kabla halijaanza kazi.

Lakini Mhe. Mwenyekiti hii ni sekta ya uchochezi, ya uvumilivu na mengineyo. Katika kazi za shirika hili moja ni kudumisha uhuru wa wahariri. Mhe. Mwenyekiti bado tumo katika nchi za ulimwengu wa tatu na tulichojifunza au tunachoendelea kujifunza ni kwamba wahariri wengi wa habari wametoweka katika ulimwengu. Aidha kwa kupata kifo au kwa kuondoka katika nafasi zao. Nini kilichosababisha ni sababu ya kutaka kuutumia uhuru wao wa kuwa wahariri au waandishi wa habari. Sasa najiuliza je, serikali imeshajipanga kuwapatia hao wahariri uhuru huo? Kuna mengi yatatakiwa katika kuandika kwao na mengi wametakiwa wayaweke wazi ili wananchi wayafahamu, lakini kwa uzoefu wetu kipengele hiki hakipo katika nchi zetu za kiafrika. Tumeshaona huko akina Wole Soyinka wameishia wapi na wengine wengineo.

Sasa mimi ninahisi ikiwa tayari tumeshajiandaa basi wajiandae kwa ukweli ili huu uhuru upatikane, isije kuwa leo mimi ni *freelance* nikasema nataka kuandika habari keshokutwa nikaja nikafuatiwa na watu siwajui wanatoka wapi.

Mhe. Mwenyekiti lengo ni kuimarisha upatikanaji wa habari na ndio tukaleta shirika tukaunganisha vyombo na televisheni. Lakini katika nchi hii nakumbuka kuna kijigazeti kimoja kinaitwa Zanzibar Leo, kwa nini tusikiunganishe nacho tukakiweka katika shirika hili hili moja ili tukaongeza nguvu zaidi. Leo tuna Bodi ya Shirika hicho cha kigazeti kimoja hicho nahisi ni upotevu wa raslimali za umma. Kama ni hivyo basi tungekuwa na shirika moja ambalo litakuwa na bodi moja tu pengine tutapunguza gharama za uendeshaji, kwani tukiunda shirika moja tu ambalo litaendeshwa na shirika hili la magazeti basi gharama zitapungua kulikoni kuwa hivi na nina imani kwamba utendaji unaweza ukawa bora zaidi.

Mhe. Mwenyekiti kama nilivyokwambia mwanzo mimi sitokuwa na mengi, kwa hivyo juu ya hayo kwa vile mswada ni mzuri wa kuanzisha shirika, mimi maoni yangu ni hayo na naunga mkono hoja.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Mhe. Mwenyekiti, ahsante na mimi kunipa fursa hii ya kuchangia mswada huu ambao wenzangu tokea jana wenzangu wameshachangia na wamechangia kila kifungu. Mhe. Mwenyekiti kama ulivyo mswada huu kwamba una sehemu sita kubwa ambayo sehemu ya kwanza inasema masharti ya awali. Lakini kabla ya hayo kwanza nimpongeze Kaimu Waziri ambaye ame-*present* mswada huu na vile vile niwashukuru watendaji pamoja na waziri wao ambaye leo hayupo lakini nimshukuru kwa kutuandalia mswada huu.

Kama wenzangu walivyotangulia kusema kwamba habari ni muhimu na habari ni jambo la kuliendeleza kwa sababu habari ni kila kitu. Na kama alivyokwisha kusema mwenzangu hapa, kwa muono wangu ningesema hata hii sheria baada ya sheria kuwa ya utangazaji ili kwa sababu

ukiwa na watoto wako basi na hata wale wengine uwafikirie. Kwenye habari inabeba uchapaji pia ni chombo cha habari vile vile ukitizama hata na gazeti. Kwa hivyo mimi ningependekeza labda sheria hii badala ya kuwa sheria ya utangazaji lingeitwa Shirika la Habari badala ya shirika la utanganzaji kwa mnasaba ule wa kupunguza matumizi au kuweko na bodi tofauti tofauti.

Mhe. Mwenyekiti baada ya hapa niende kwenye ukurasa wa 291 ambayo inasema chini kabisa kuna mwaka wa fedha maana yake ni kipindi cha miezi 12 kuanzia tarehe 1 Julai, na kuishia tarehe 30 Juni. Mimi niseme nimefarijika sana kwa kuona kwamba kipindi cha mwaka wa fedha ukawa kama hivi ulivyo. Kwa vile niseme kwamba uzoefu wa mashirika mengi hawafuati hii *financial year* hii na hufuata ya kalenda ambayo inasema tarehe 1 Januari mpaka tarehe 30 Disemba, sisi kama Zanzibar tunakwenda na *financial year* kuanzia Julai kwenda Juni.

Kwa hivyo hata tunapokaguliwa mahesabu yetu vile vile kwa mujibu wa Mdhibiti kama nilivyosema juzi kwamba mdhibiti yeye anataka apelekewe taarifa zile zote si zaidi ya miezi mitatu baada ya kufunga mahesabu. Lakini tatizo linalojitokeza ni kwamba hapelekewi na hasa Mashirika yetu mengi yanafanya hivyo yanakuwa hayapelekewi kwa sababu kuanzia Julai, Agosti na Septemba, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali hutaka apelekewe. Kwa hivyo hapa mimi nimefarijika sana kuona kwamba *financial year* ni kuanzia Julai mpaka Juni.

Nikienda sehemu ya pili kuanzishwa shirika na majukumu yake, niende kifungu cha pili kuanzishwa kwa Shirika. Shirika litakuwa na mrithi wa vyombo vya habari vya serikali vinavyojulika kama Televisheni ya Zanzibar na Radio Sauti ya Tanzania Zanzibar. Hapa ni ile kwamba nimeshaisema huko mwanzo kwamba kwa sababu vyombo vya habari ni pamoja na magazeti na pia Idara yetu ya Upigaji chapa inaingia hapa. Kwa sababu nimepata uzoefu nilipokuwa Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Vijana. Kwa hivyo Habari ilikuwa imebeba magazeti pamoja na Idara ya Upigaji chapa, kwa hivyo ilikuwa navyo vijisikie na kujiwekea mazingira ilikuwa na wao katika shirika hili na wao wamo kwa mnasaba ule ule wa kuendeleza mbele vyombo hivi na kuleta ufanisi mzuri.

Vile vile suala la mhuri niseme mhuri ni lazima kuwepo kama nilivyochangia huko nyuma tulivyoona kuna sehemu za mihuri katika taasisi mbali mbali. Kwa hivyo, nayo mhuri ni lazima na ule mhuri wenyewe uwe na picha zinazoelezea kitu chenyewe, kama ni habari basi kuwe na mtu kama ni mtangazaji, ikiwa ni kitabu, ikiwa nini hilo mimi sina wasi wasi nalo.

Vile vile niende katika kifungu cha 5, kifungu hiki kinazungumzia kwamba malengo ya shirika yatakuwa ni kutoa taarifa, elimu na burudani kwa jamii (a) hiyo.

Kifungu cha 5(b) kinasema kwamba,

> "Kutoa huduma za utangazaji za redio, televisheni na huduma nyengine zinazohusiana na hayo na vipindi ambavyo vitachangia maendeleo ya kijamii, kiuchumi, kisiasa na kitamaduni pamoja na kutilia mkazo umoja wa kitaifa katika upanuzi wa utamaduni".

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli vyombo vyetu hivi vinatoa burudani kwa hivyo hizi burudani ndani yake zinatoa elimu na kila ukitizama kwamba elimu ni jambo la msingi kabisa. Mimi nashangaa kwa vyombo vyetu hivi, ukizaa mtoto ukawa unampa majina ya ajabu ajabu itafika

siku mtoto yule atakuwa wa aina gani na ndio tunapoambiwa kwamba tukizaa watoto wetu ni lazima tuwape majina mazuri, lakini mimi nashangaa majina haya.

Wenzangu wamesema vyombo vya habari hivi vinatoa majina ya ajabu ajabu kwa *interest* zao wenyewe watu, kama hiyo TV Kitangi mimi nakumbuka na hata aliyesema namjua. Kwa hivyo, pia hili suala la kutoa maneno haya ndio yanayoturejesha nyuma, ni lazima sisi sote tujuwe kwamba tuna-*responsibility* ya kuvisimamia. Sisi kama Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi juzi tumetoka semina kwamba sisi kamati ndio zitakazosimamia serikali na serikali ni pamoja na haya mashirika hivyo ni lazima tuyasimamie na tujue kwa niaba ya wananchi wetu waliotuchagua na sisi vile vile tuna dhamana hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, niki-*quote* mwandishi mmoja wa kitabu Ndugu Emerson anasema *"Every man believes that has a greater responsibility"*. Kwa hivyo na sisi sote tuna *responsibility* hiyo ya humu ndani kusimamia serikali na kusimamia vyombo hivi ili vilete ufanisi na tuachane na maneno au majina ya kuvipa vyombo hivi kwa *interest* zetu wenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, nikienda katika malengo ya shirika nimesaoma lakini kutakuwa na kazi za shirika, kuandaa vipindi vya ndani vyenye ubora na kuchukua vipindi vya kigeni vinavyoendana na mahitaji ya wazawa. Hapa kidogo Mhe. Mwenyekiti, sijui kama itakuwa ina-*sound* vizuri kuandaa vipindi vya ndani vyenye ubora na kuchukua vipindi vya kigeni vinavyoendana na mahitaji ya wazawa. Mimi ningependelea labda haya maneno ya mbele huko yakaondoka, kuandaa vipindi vya ndani na vya nje vyenye ubora haya maneno mengine huku mbele sijui wazawa sijui tutaanza kutafuta wazawa wako wapi, wengine watasema mimi mzawa wa wapi au unataka uzawa wa wapi. Kwa hivyo, mimi hapa ningependelea haya maneno ya mbele yakaondoka.

Mhe. Mwenyekiti, uwezo wa shirika kwenye kifungu nambari 7 ukurasa wa 293 kinachosema kwamba,

"Kwa kuzingatia sheria zinazotumika, Shirika linaweza kufanya kazi zote zinazotokea au kupelekea kufanya kazi zake vizuri katika kutekeleza majukumu yake na bila ya kuathiri masharti ya jumla shirika litakuwa na uwezo ufuatao:

(a) Kumiliki, kukodi, kununua, kumiliki mali, kuuza na vyenginevyo kuuza mali ambayo lazima ithibitishwe na bodi".

Sasa hizi bodi nasema ni sawa sawa na mtu ni watu wenyewe binafsi kwa hivyo mtu anaweza kusema *interest* yake mwenyewe huku kuuza lazima kuzingatie kile kitu kinachouzwa, unaweza kukiuza kitu kwa sababu kuna utaratibu wa kuuza mali za umma na vitu vinakuwa bado vizuri tu na vikauzwa. Kwa hivyo, hapa mimi niseme hii kuuza basi kuwe kile kitu kinachouzwa kiwe hakiwezi kutumika tena labda serikali inaona kuwa ni tatizo kwa hivyo hapa unaweza kuuza, lakini kwa kusema kwamba bodi imekaa tu inauza aa. Tumeshapita maeneo mengi tu tunapokagua tunaona matatizo yanayojitokeza na bodi zenyewe kuamua kwa sababu ni bodi ikaamua kwamba inauza kitu ambacho bado ni kitu kinachohitajika. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, hilo pia nimeliona na nasema hizi bodi ziwe na uadilifu zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, nikienda ukurasa nambari 295 kwenye sehemu hiyo hiyo ya tatu inasema kwamba, "kuidhinisha mpango wa utekelezaji wa shirika pamoja na bajeti ya kila mwaka". Kwa hivyo, hapa Mhe. Mwenyekiti, ningependa huu mpango wa utekelezaji kuidhinisha mpango wa matumizi wa shirika pamoja na bajeti ya kila mwaka. Kwa sababu ni lazima unapokuwa na jambo lolote basi uwe na bajeti, hivyo hapa baada ya mpango wa utekelezaji ningesema labda tungechukua mpango wa matumizi kwa sababu inahusu na bajeti.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea nije ukurasa wa 296 kwenye sehemu hiyo hiyo inayosema uongozi na wafanyakazi wa shirika kifungu nambari 12. Shirika litakuwa na idara ya vitengo kama itakavyoamuliwa na bodi, uanzishwaji wa idara kama walivyosema wenzangu kuwa hizi idara nyengine ni zipi. Ningetoa pendekezo basi, kwa kuwa kule kuna Shirika la Utangazaji na kwa bahati nimesema kuna vyombo vyengine ambavyo navyo vinakuwa vinabebwa kwenye utangazaji basi ibebe idara hizi ambazo ni Idara ya Upigaji Chapa na Idara ya Gazeti.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile kuna kifungu nambari 13(1) wafanyakazi wa shirika. "Shirika linaweza kuajiri wafanyakazi wengine kama vile bodi itakavyoamua kwa kuzingatia masharti ya utumishi wa wafanyakazi. Hakuna kitendo, kitu au jambo lolote litakalofanywa au kuachwa kufanywa na mfanyakazi wa shirika au mtu mwengine yoyote aliye chini ya maelekezo ya shirika kitakachomfanya akiwa kitendo, kitu au jambo lolote hilo lililofanywa au kuachwa kwa nia njema katika utekelezaji wa sheria hii. Mfanyakazi au mtu huyo hutiwa hatiani binafsi kwa hatua zozote za kisheria au madai mengine".

Hapa kidogo Mhe. Mwenyekiti, akija Mhe. Waziri anifafanulie sijafahamu vizuri. Kuwa shirika linaweza kuajiri kama vile bodi hii tunajua kwamba wafanyakazi ni lazima kuajiriwa na wafanye kazi.

Vile vile jambo jengine ninalolizungumzia ni kama wenzangu walivyolizungumzia sana ni kuhusu maslahi ya hawa wafanyakazi. Kwa kweli wafanyakazi wa vyombo vya habari kwa kweli nasema wana rizki, tumeshaona maeneo mbali mbali, tumeshashuhudia kudhalilishwa na mpaka kuuwawa kwa wanabahari. Kwa hivyo, vile vile ni jambo ambalo na wao kwa maslahi watizamwe, tunawaona hapa kama walivyosema wenzangu waandishi wa habari wapo hapa wanatupiga picha saa zote mpaka tunaondoka nao lakini maslahi yao bado hawayapati na tena yako chini ya kile kiwango.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sasa hivi tunasema posho la mfanyakazi wa kawaida lisipungue shilingi elfu tano, lakini leo wanapewa sifikirii mimi nimesafanya uchunguzi kwamba wanapewa shilingi 2,500 na wala hawapewi kwa wakati. Kwa hivyo, mimi ningesema kwamba hili posho lao lizidi wapewe maslahi yao ni watu ambao na wao wanajituma na halafu kazi yenyewe ni nzito ya lawama. Sasa Mhe. Mwenyekiti, nigesema vile vile waandishi wa habari ni watu muhimu sana kwa sababu tunataka habari zetu zitoke vizuri lazima tuwasaidie kwa hilo.

Halafu nikienda na sehemu ya tano anasema masharti ya fedha. Hapa ndio hupenda kuogelea zaidi kwa sababu masharti ya fedha mimi mwenyewe nilikuwa fani yangu ni ya uhasibu. Kifungu kinasema fedha za rasilimali ya shirika zitatokana na mtaji kutoka serikalini, kwa hivyo kama fedha hizi zinatoka serikalini basi ni lazima zifuate yale masharti na kanuni za fedha, ni

lazima zifanyiwe ukaguzi ingawaje mbele iko huko hivyo ni lazima fedha hizi zitumie kanuni na taratibu za fedha.

Nikiendelea niende katika kifungu cha 15(1) kinazungumzia malipo yote ya fedha zinazohitajika kufanywa na shirika katika kutekeleza, kukamilisha na kufanya kazi zake na wajibu wake chini ya sheria hii yatatokana na fedha zake, ina maana hapa kutakuwa na bajeti. Mimi hapa Mhe. Mwenyekiti, sina *objection*.

Mhe. Mwenyekiti, nikienda katika ukurasa wa 297 kifungu cha 16(1) kinasema kuwa hesabu na ukaguzi. Shirika linatakiwa kuweka na kuhifadhi vitabu vya hesabu kuhusiana na fedha zilizopatikana na zilizotumika, mashirika na risiti matumizi yaliyofanyika. Hapa ukaguzi hilo ni lazima ufanyike kwa fedha ambazo zimepatikana ni lazima zikaguliwe na mkaguzi ni yule yule Mkaguzi wa Hesabu za Serikali isiwe kwamba ni shirika likawa lina uwezo zaidi wa kutafuta watu kutoka nje. Mimi sioni mantiki hasa kwamba sisi wenyewe hapa tunapiga kelele sana humu ndani ya Baraza kwamba Jamhuri ya Muungano, matatizo ya Kimuungano, lakini sisi wenyewe saa nyengine tunajipeleka wenyewe kule kwenda kufanya mambo yetu.

Kwa sababu kama ni Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali tunae kwa nini twende tukachukue wakaguzi wengine, ni kwamba bado sisi wenyewe hatujakuwa na uwazi tena kwenye bodi hizi unakuta ni Makatibu Wakuu, Wakurugenzi Wakuu lakini kwa nini tunakwenda huko, kwa nini hatuwi na uwazi tukampa hadhi yake Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali wetu, hatuoni sababu ya kwenda huko labda kutakuwa na *interest* nyengine kwamba mtu unajua ukienda ukimchukua mkaguzi nje na yeye ana *interest* zake, atakuja hapa madhali anajua unampa pesa kwa kuwa mara nyengine apate tena nafasi ile hatatoa *query* zilizokuwa nzito, hataibua zile kesi hasa zilizokuwa nzito. Kwa sababu anataka na mwaka mwengine ukamchukue aje akufungie tena mahesabu aje akukague atakuwa hasemi ule ukweli mana yeye anakwenda kibiashara zaidi. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, hili niseme kwamba CAG wetu tumpe hadhi yake.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo niende kwenye ukurasa wa 298. Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli hapa kuna uwezo wa kutunza kanuni. Waziri kwa kushauriana na bodi anaweza kutunga kanuni kwa ajili ya utekelezaji bora wa masharti ya sheria hii na bila ya kuathiri ujumla wa masharti hayo. Juzi ilijitokeza vile vile anaweza ni kwamba anaweza akafanya anaweza asifanye. Kwa hivyo, hapa ibadilike kidogo iwe waziri kwa kushauriana na bodi atatunga kanuni kwa ajili ya utekelezaji bora wa masharti ya sheria hii na bila ya kuathiri ujumla wa masharti hayo.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo kwa niaba ya wananchi wangu wa jimbo la Amani nasema naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsane sana.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipatia fursa hii niweze kuchangia machache katika mswada huu. Mhe. Mwenyekiti, kabla sijaanza kuingia katika huu mswada naomba nichukue fursa hii adhimu kuwapongeza sana wafanyakazi wetu wa ZBC *Television* na ZBC *Radio*.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli wafanyakazi hawa wanajitahidi sana kadiri ya uwezo wao unavyoruhusu kuweza kutekeleza majukumu yao, wanastahili pongezi na sifa kubwa.

Mhe. Mwenyekiti, nayasema hayo sisi wenyewe tukiwa mashahidi kamatunavyowaona kutwa nzima wapo hapa wamesimama wanaweza kutafuta ripoti hizi za Baraza ambazo tunashughulika hapa viongozi tunakuwa nao pamoja asubuhi mpaka usiku. Kwa kweli kazi zao ni ngumu na zinastahili kufikiriwa kwa kina zaidi. Wenzetu hawa vyombo vyao vinatumia *electronic* kwa muda wote kwa hivyo wanahitaji kuangaliwa katika posho ambalo litaweza kuwasaidia vizuri hata katika afya zao.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo nianze na mimi kuchangia mswada huu kwani wenzangu wengi wamechangia na wametoa michango mizuri sana. Nataka nianze mchango wangu katika ukurasa wa 292 kwenye kifungu Nam. 5. Mhe. Mwenyekiti, hapa kuna malengo ya shirika naomba ninukuu.
Kifungu Nam. 5 kinasema kwamba:

> "Malengo ya shirika yatakuwa ni: (a) kutoa taarifa, elimu na burudani kwa jamii".

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli taarifa tunazipata na elimu tunapata kupitia njia hii kwa wenzetu mbali mbali, wasanii, mashehe watu mbali mbali ambao wanatoa elimu kupitia njia ya televisheni au redio. Lakini mimi nilichokuwa nataka niombe hapa hizi elimu ambazo tunazipata je, zinakwenda sambamba na yale mahitaji yetu ambayo sisi tunayahitaji? Kwa sababu tunaweza kusema kuna elimu kupitia njia ya burudani, lakini ukakuta nyimbo ambayo inaimbwa labda pengine haiendani na mila na silka za Mzanzibari utakuta hiyo nyimbo wewe mwenyewe itakuchukia. Sasa niombe elimu hii ambayo inatolewa basi iwe ni elimu ambayo inazingatia sana kuona jamii inafaidika kupitia elimu hii na sio inakula hasara.

Kwa sababu unaweza kumuelimisha mtu ukategemea unafanikiwa kumbe unaharibikiwa. Kwa hivyo, kupitia chombo hiki kwamba hiki ni chombo kikubwa ambacho Wazanzibari sote na kwengineko kinategemewa hivyo tungependa kiweze kutuelimisha vizuri hasa ukizingatia mila na utamaduni wetu.
Mhe. Mwenyekiti, niende katika mswada huu katika kifungu nambari 6 ambacho kiko katika ukurasa wa 293 kazi za shirika zitakuwa. Naomba ninukuu kidogo,

Kifungu Nam. 6(a) kinasema kwamba:

> "Kuanzisha mfumo endelevu wa kukusanya, kuhifadhi, kuchambua na kusambaza habari kwa umma".

Mhe. Mwenyekiti, kweli shirika lina kazi kubwa ya kutupatia vipindi vyenye ubora, tunaona vipindi vingi vinaoneshwa lakini utakuta havina ubora kwa sisi, tunaomba tupatiwe vipindi vyenye ubora ambavyo vitaweza kukidhi mahitaji yetu. Lakini pia katika Kifungu cha 6(b) kinasema kwamba,

> "Katika kuandaa vipindi vya ndani vyenye ubora na kuchukua vipindi vya kigeni vinavyoendana na mahitaji ya wazawa".

Hili pia nalo ni la msisitizo kwa sababu sisi tunajihisi labda hatuna vipindi vizuri vya kuonesha lakini kumbe tuna vipindi vizuri vya kuonesha na vinavyopendwa hasa na wenyewe Wazanzibari lakini tunaacha na tunaleta vipindi ambavyo ni vya kigeni lakini utakuta havina maana sana na sisi. Kweli vipindi vya kigeni tunavihitaji lakini viendane na sisi wenyewe upenzi wa kuvipenda.

Mhe. Mwenyekiti, katika hili niombe, kama kazi ya shirika itakuwa ni kuhifadhi basi kweli iweze kuhifadhi kwa sababu kuna vipindi vingi tu ambavyo vimerikodiwa nyuma na mimi nitaomba kama vipindi hivi bado vingalipo basi pia tuweze kuoneshwa. Nije katika vipindi kama vya michezo ya tamthilia, michezo ya zamani ilikuwepo ambayo wame-*act* kina Bwana Mashaka na wenzake au marehemu Suwedi vilikuwa ni vipindi vizuri na vinaendana na mila na utamaduni kabisa wa Mzanzibari. Kwa hivyo, kama kweli vinahifadhiwa na hifadhi hizi kama zipo katika shirika basi tunahitaji tuoneshwe kwa sababu ni vya zamani lakini bado vinakwenda na wakati na wenzetu wanasema *old is gold*. Hivyo bado tunavihitaji ni vizuri na vina mvuto tuoneshwe kama vipo.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu huu naomba niende katika ukurasa wa 295 kifungu nambari 10 kuna kazi za bodi. Katika kazi hizi za bodi mimi nilikuwa naomba, zamani katika TVZ kulikuwa na *censor board* ile ambayo ilikuwa kabla ya msanii au muimbaji yoyote kutoa nyimbo yake ilikuwa ikiweza kupitia kwanza ile bodi kuona kama haina athari yoyote na baadae ndio ikitolewa. Kwa hivyo, hii ilikuwa imeleta mazingatio makubwa kuona kitu kama kitakuwa hakipendezi au hakifai kukionesha kwa jamii yetu kiliweza kudhibitiwa. Nasema hilo kwa ushahidi kwa sababu iko nyimbo iliwahi kutoka iliyokuwa ikiimbwa kwamba, "Ingawa haramu malipo yake moto, msaidie mwenzako". Sasa hiyo nyimbo ilikuwa imetokana na maadili yetu hivyo iliondoshwa na ilifutwa. Kwa hivyo hii ikiweko itaweza kutusaidia na itaweza kutuhifadhi kwenda vizuri na jamii yetu.

Mhe. Mwenyekiti, halafu katika kifungu (d) kuna kuandaa na kusimamia kanuni za wafanyakazi, kanuni za fedha na muundo wa mishahara ya wafanyakazi pamoja na maslahi mengine. Hili Mhe. Mwenyekiti, ndio la msisitizo, tunasema wenzetu wanafanya kazi katika njia ya kujitahidi sana kwa hivyo ni vizuri maslahi yao yakaangaliwa kwa kina, kama kuna marupurupu yao yakashughulikiwa, kama kuna madeni wanayodai wakaweza kulipwa kwa sabau kuna wafanyakazi wengi tu ambao malipo yao hayaridhishi wanafanya kazi bila ya kupata malipo au malipo yasioridhisha. Kwa hivyo, hili tunalisisitiza ili tuone sasa tunakwenda katika shirika jipya ambalo litaweza kuwathamini sana wafanyakazi wake.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika ukurasa wa 296 katika kifungu cha 13(1). Mhe. Mhe. Mwenyekiti, kifungu hiki kinasema, Shirika linaweza kuajiri wafanyakazi wengine kama vile bodi itakavyoona kwa kuzingatia masharti ya utumishi wa wafanyakazi. Mhe. Mwenyekiti, shirika bado liajiri ili tuweze kupata wafanyakazi ambao wataweza kufanya kazi vizuri katika shirika.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nikija katika wafanyakazi kuna wafanyakazi wengi bado wanahitajika katika shirika tukianza na sehemu ya wahariri, wahariri ni wachache sana na ndio watu muhimu sana. Mhe. Mwenyekiti, hatuna mhariri wa mambo ya kisiasa au wa habari nzito wanaziita, hatuna mhariri wa michezo, hatuna mhariri wa mambo ya nje, tunaomba kufanyiwa kazi vizuri ili tuweze kupata shirika ambalo litakuwa lina watendaji wazuri na ambao kila mmoja anakaa katika nafasi yake.

Lakini pia katika shirika letu hili kuna vijana wengi ambao wanafanya kazi kwa njia ya kujitolea katika ZBC na hawajaajiriwa na kwa muda mrefu sana. Hawa sidhani kama hata wanalipwa posho na kama wanalipwa mimi naweza kusema litakuwa ni dogo sana haliwezi likakidhi mahitaji yao, hawa tungeliwafikiria ili tuwaajiri waweze kuwepo pale. Kwa sababu kazi ndio wanazifanya wao kwa hivi sasa, tuweze kuwaajiri ili waweze kufanya kazi zao pale vizuri lakini vyenginevyo tunaweza tukawa tunatafuta shirika jipya kila siku lakini utakuta haliendani na mahitaji. Kwa sababu shirika linataka wafanyakazi na kila mmoja kwa nafasi yake, sasa mimi kama nipo unanitumilia tu kwa kwamba hujaniajiri mimi nina hiari yangu naweza nikaja au nisije, inawezekana mimi nasoma taarifa ya habari lakini wakati wa taarifa ya habari mimi nikaingia mitini, sasa pale itabidi tena kamata kamata hii itakuwa haileti sura nzuri katika shirika hili ambalo tunakusudia kuliunda tena upya.

Mhe. Mwenyekiti, kuna wafanyakazi wa *master control*, hawa na wao wanajituma kutwa kucha wako pale wanaliviana tu, anaingia huyu anatoka, anaingia huyu anatoka lakini na wao hawana maposho ya kuwawezesha kwenda vizuri katika shughuli yao ile.

Mhe. Mwenyekiti, shirika hili mimi kwanza nalipongeza kwa sababu lishazalisha wataalamu wengi tu, wengi wamekuja kujifunza pale halafu ndio wanakwenda kuanzisha wao vituo vyao huko kwengine. Sasa hii ni pongezi kwa sababu imekuwa ni walimu wa kufunza watu wengine. Lakini je, hatuoni kama tunakula hasara kila siku sisi tunawafunza watu baadae wanatukimbia? Hii pia itakuwa ni hasara kwa shirika kwa sababu umeshamlea mtu kwa kipindi kirefu lakini baadae ameshapata ujuzi wa kutosha hadumu tena katika shirika na hiyo inatokana kwa sababu bado hatujamthamini na kumtunza vizuri ili akaweza kukaa pale katika shirika.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitoe mfano na hii niseme tutapoteza watu wengi ambao wana vipaji na tutaweza kuwakosa kwa haya mahitaji yao ambayo hatuyashughulikii.

Mhe. Mwenyekiti, kuna ZBC kule Bara imeanzishwa kwa nia nzuri na sote tumeipokea kwa kuifurahia. Kuna kijana pale anaitwa Juma Mmanga anatupa habari za magazeti, kwa kweli kilipoanzishwa kipindi kile mimi nitoe pongezi sana kwa ZBC wameona umuhimu wa kuanzisha kipindi kile cha magazeti na wakaweka kule, kwa kweli kimekuwa kinatupa ripoti nyingi ambazo sisi watu wa vijijini tulikuwa hatuwezi kuzipata kiurahisi. Kwanza magazeti kwetu ndio kwanza yanaanza kuja hivi sasa hata huo utamaduni wa kuanza kuchukua kuyasoma bado, lakini tukisikia magazeti yale kwa kweli mtu unaondoka nyumbani hali ya kuwa habari umezipata. Tunae kijana Juma Mmanga lakini huyu na yeye anaweza pengine akahama akahamia kwengine ni kijana ana kipaji sana, lakini maslahi ya wafanyakazi ndio yanayorudisha nyuma na ukaona wafanyakazi wanashindwa kuendelea kudumu katika chombo chao.

Lakini nawapongeza pia wafanyakazi hawa kwamba ni wazalendo sana, tushukuru ni wazalendo wanaipenda nchi yao, wanaipenda serikali yao, tena wanawapenda viongozi wao, hili lazima tukubaliane nalo. Nayasema hayo Mwenyekiti kwa ushahidi, wafanyakazi hawa humu ndani tu wewe ukiangalia kama utasinzia wewe hapo watakuchukua sasa hivi, lakini kama atasinzia Waziri wa Habari Wallahi huji kumuona katika kioo hawamchukui wanamuheshimu sana kiongozi wao, lakini hapo hata awepo Spika basi watamchukua, wanawapenda sana viongozi wao na wanawaheshimu na ndio maana wanafanya kazi kwa uadilifu. Mimi naomba tuwatendee

haki wafanyakazi hawa ili waweze kufanya kazi hali ya kuwa wanaipenda kazi yao, waweze kufanya kazi hali ya kuwa wanawapenda mabosi wao hivyo ndivyo watakapofanya kazi na wao kiuadilifu.

Mhe. Mwenyekiti, kuna wafanyakazi ambao wamekwenda masomoni China, Cairo na mpaka muda huu hawajalipwa fedha zao hii haileti sura nzuri. Sisi tunasema tunaunda upya kwa hivyo kutafuta kitu kipya ni lazima uondoshe kasoro zile za zamani ili uweze kuweka kitu kipya. Tunaomba sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niongeze tunasema tunaondoka katika TVZ tunakwenda katika ZBC ili kuweza kulifanya hili kuwa shirika ambalo litaweza kukidhi mahitaji yetu. Mhe. Mwenyekiti, shirika halina vifaa, halina vitendea kazi hivyo kweli tumejidhatiti sisi kwamba tunaingia katika ushindani mana hili ni shirika la kibiashara hivyo kweli sisi tunaingia katika ushindani wa kibiashara hata kamera pia hatuna. Mhe. Mwenyekiti, ni tatizo ukitaka kwenda mbio mpaka uagane na nyonga yako kwanza, leo shirika hili na ni chombo muhimu sana kamera tuna moja hizi nyengine unazoziona za watu binafsi wanafunzi wenyewe wanaosoma kule TVZ akitoka anatoka na kamera yake, akiamua leo siji haji nayo, kweli hii itatufikisha wapi na hiki chombo ndio sasa tunataka tukitafutie habari hasa zitafutwe, mana hizo habari kama zilikuwa hakuna sasa tuna shirika tunataka hizo habari sasa zipatikane, mimi nataka sasa hivi nikitoa habari kule Mkokotoni nataka ifike ZBC sitaki iwe kiporo. Kwa hivyo ni lazima tuwe na vitendea kazi.

Mhe. Mwenyekiti, hakuna gari na kama iko hakuna mafuta, wafanyakazi wanafanya kazi katika mazingira magumu kabisa, hairidhishi haipendezi, ni lazima madhali tunataka kuingia katika ushindani wa kibiashara basi ni lazima tuweze kubadilika. Hapo utaona kisiri siri ZBC lakini kidhahiri TVZ kwa mfumo huu wa kuwa hatuna zana.

Mhe. Mwenyekiti, ving'amuzi. Ving'amuzi tunavihitaji na kama vipo waziri akija kutoa ufafanuzi atwambie ili tuvifuate wapi tunataka na sisi tuingia katika hiyo *digital* tuondokane na *analog*. Kwa hiyo ving'amuzi kama vikija tunaomba Waheshimiwa hapa Barazani tuandikwe sote tuorodheshwe ili tuvipate ving'amuzi hivyo tuendane na huo wakati japo umeshatupita, mana wenzetu washaingia sasa sisi huo wakati wa ziada tuliopangiwa basi na sisi tuweze kumudu tuwe tushavipata tuweze kuvitumia.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, kwa nini tunakuwa masikini sana hili shirika la biashara, mimi naona kuna matangazo mengi ya biashara pale kwa nini tunakuwa masikini wa kununua hata kamera, hata wa kutia mafuta gari mimi nahisi kuna mahitaji; lazima tubadilike, lazima tubadilike. Mhe. Mwenyekiti, shirika hili ni la serikali na tusilifanye likawa kama la mtu binafsi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli mimi nilitaka nichangie hayo lakini pia nilitaka niwaombee wafanyakazi wa shirika ikiwezekana basi hata muwapatie mikopo ya vespa ili waweze kwenda kazini kwa wakati. Juzi wafanyakazi walichelewa hapa laiti wangelikuwa na usafiri wangewahi wanaheshimu sana taratibu zao na kazi zao wanazopangiwa, lakini usafiri. Kwa hivyo, naomba ikiwezekana hata wakopeshwe vespa ili waendane na wakati na wao.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo na baada ya kutegemea labda majibu mazuri ambayo atakuja kutupa Mhe. Waziri atakapokuja mimi sina pingamizi na nadhani tunaunga mkono

mswada huu kwa silimia mia moja kwa sababu lengo letu ni kufanikiwa na si kuharibikiwa ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante mhe. Mjumbe kwa kumalizia na naona dakika umezimaliza zote. Kwa hivyo, imepelekea Mhe. Jaku Hashim Ayoub kushindwa kutoa mchango wake. Lakini pia tuseme tu kwamba tutakaporejea saa 11:00 jioni itakuwa ni zamu ya Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko baadae Naibu Waziri na mwisho waziri atakuja kumalizia ili tuweze kuendelea na masuala mengine na wale ambao hawakubahatika tuwaombe radhi kwa hilo na wanaweza kuchangia kwa maandishi. Hilo ni la kwanza.

Lakini vile vile kabla hatujaakhirisha Baraza kuna matangazo matatu hapa naomba kuyatoa. Tangazo la kwanza limeletwa na Katibu Msaidizi wa Mnadhimu, linasema kile kikao cha Wawakilishi wa CCM kipo pale pale mchana huu baada ya kuakhirishwa kwa Baraza hili. Kwa hivyo wawakilishi wote wa CCM wanatakiwa waelekee katika ukumbi wa mkutano juu kwa ajili ya kuendelea na taratibu zao.

Tangazo la pili Katibu wa Baraza la Wawakilishi anaendelea kuwakumbusha tena kwa mara nyengine wale Wajumbe waliokuwa hawajaenda kujiandikisha katika vitambulisho vya uraia Tanzania bado nafasi hiyo ingalipo wanatakiwa waende juu wakamalize masuala hayo ili waondokane na usumbufu ambao utaweza kujitokeza baadae katika majimbo yao.

Na suala la tatu naona haya mambo yanaingiliana kidogo, kuna taarifa kwa Wajumbe wote wanawake kuwa yale mafunzo yao yatakuwepo leo mara baada ya kuakhirisha kikao cha mchana huu katika ukumbi wa juu vile vile, nao wanaombwa kuhudhuria. Kwa hivyo, hayo ndio matangazo ambayo yapo. Baada ya maelekezo hayo nachukua fursa hii vile vile kukushukuruni sana ndugu Wajumbe kwa mashirikiano yenu na tunaakhirisha Baraza hili hadi jioni saa 11:00 kamili tutakapoendelea na taratibu zetu. Ahsanteni sana.

(Saa 7:00 mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11: 00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii jioni hii kuchangia waraka huu muhimu kama wenzangu walivyochangia tangu jana.

Mhe. Mwenyekiti, leo nilikuwa nataka kuzungumzia lile suala lililozungumzwa na baadhi ya wachangiaji kuhusu masuala kuona kwamba waziri anapewa mamlaka makubwa katika kuendesha hizi bodi au haya mashirika.
Akatoa katika kifungu cha 3 kwamba Waziri aweze kutoa maelekezo ya jumla na maalum kwa bodi kuhusiana na utendaji wa shughli za shirika na matumizi na uwezo wa shirika, bodi itasimamia maelekezo hayo.

Sasa wanasema kwamba hapa waziri kapewa mamlaka makubwa ya kuingilia bodi. Mimi naona kwamba si sahihi waziri hakupewa mamlaka makubwa, kwa sababu waziri hapa katika hili

Baraza letu tukufu ndiye anayeulizwa kuhusu shirika hilo. Hapa haji mkurugenzi wala haji hapa mwenyekiti wa bodi kuja kujibu masuala ya Waheshimiwa Wajumbe watayouliza kwenye Baraza hili, bali waziri ndiye anayehusika kuja kujibu yote yaliyofanywa kwenye bodi yakiwa mabaya basi lazima waziri ajibu na waziri ni lazima awajibike.

Utakuta kutokana na hilo basi ukisema kwamba waziri anapewa mamlaka makubwa si kweli, lakini waziri apewe nafasi ya kuweza kufanyakazi kutoa maelekezo yake katika bodi na maelekezo yake yafuatwe ili bodi hiyo ifanye kazi kwa mujibu wa *policy* ya serikali ilivyo.

Tuchukue mfano Tanzania Bara. Waziri wa Viwanda na Biashara Tanzania Bara ameivunja bodi ya TBS yote kutokana na uzembe uliokuwepo. Mamlaka yale amepewa kutokana na hali halisi ilivyokuwa mbaya katika TBS.

Waziri wa Uchukuzi na Miundombinu Mhe. Mwakyembe amemsimamisha kazi Mr. Mgawe ambaye ni Mkurugenzi wa Bandari ili uchunguzi ufanyike kutokana na hali halisi. Uchunguzi ulifanyika madudu yakaonekana sasa hivi anapelekwa Mahakamani. Kwa hivyo huu ndio uwezo anaopewa waziri katika kuyalinda na kuyaendesha mashirika. Lakini leo ikiwa waziri hamumpi nafasi ya kuweza kuendesha mashirika haya, halafu munakuja katika Baraza hapa kumuuliza maswali waziri, ajibu madudu yaliyofanywa na bodi au na mkurugenzi. Nahisi kwa kweli itakuwa waziri huyo hatumtendei haki, kwa sababu tunakuja kumuuliza maswali ambayo kwamba hana uwezo nao hawezi kuya-*control*.

Kwa hivyo mimi nasema kifungu hiki ni kifungu muhimu sana. Hapa katika mchangiaji na nnayo *hansard* ya mchangiaji wa asubuhi leo Mhe. Salmin Awadh Salmin, Mwakilishi wa Jimbo la Magomeni ambaye ni mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi na Kilimo. Ameeleza kwamba Wizara ya Biashara ZSTC imepitisha sheria yake hapa na bodi imeundwa, nanukuu maneno yake lakini cha kusikitisha mheshimiwa bodi hii imekuwa ikiingiliwa mno na wizara. Watu wanakwenda kutafuta wateja wa karafuu wamekuwa ni madalali sasa kwenda kutafuta masoko ya karafuu kwenda kuwaletea watu wa bodi ya ZSTC mpaka imefika mahali tunajiuliza kuna nini hapa kwenye karafuu mpaka inapofika msimu wa karafuu wanahangaika huku na huku kutafuta masoko.

Mimi nataka nikuhakikishie Mhe. Mwenyekiti, kwamba maneno haya ni ya upotofu ya kupotosha Baraza hili, si kweli bodi imeundwa na bodi imepewa mamlaka kamili ya kutafuta, kwanza ya kupanga bei za kuuzia karafuu na bei za kununua karafuu, hawakuingiliwa, bodi imefanya kazi yake hawakuulizwa, hata waziri hawakumshauri, waziri kasikia kwenye redio tu bei ya karafuu ni kiasi kadhaa na nikasikia mara ya pili kuwa bei imeongezwa waziri hakushauriwa wala hakushirikishwa.

Bodi ina mamlaka yake, kwa hivyo kuja hapa Mwakilishi akaanza kupotosha haipendezi hata kidogo. Unaposikia jambo basi ni bora ukafanya utafiti na mimi wizara yangu milango yake ipo wazi, madirisha yake yapo wazi Mwakilishi yeyote mwenzangu aje aulize nimueleze. Lakini kuja kuleta maneno ya upotofu hapa kwa ajili ya kuwapendezesha watu fulani au kwa ajili ya kuwakuza watu fulani au kuwatukuza watu fulani na kuwabomoa wengine, hili hapa si pahala pake.

Hili ni Baraza tukufu la Wawakilishi tunawakilisha wananchi, tuzungumze maneno yenye ukweli ambayo kwamba yatayoweza kusaidia wananchi wetu na sio maneno ya kupotosha. (Makofi).

Anamalizia kwa kusema kwamba wizara au waziri anahusika aingilie pale linapoharibika. Anasema wizara isubiri, nanukuu maneno yake hapo, wizara iweze kusubiri yanapotokezea matatizo waelekeze.
Mimi sikubali mpaka maziwa yamwagike ndio niende nikazoe, nitazoa nini tena mimi. Waziri nikiona panaharibika nitengeneze kabla haijapatikana hasara au hapajaharibika. Tena kasema tena mara ya pili, wizara au waziri anayehusika aingilie pale zinapoharibika kwa sababu mambo haya yana kawaida unapofanya jambo likifanikiwa basi bodi itapongezwa, lakini linapoharibika bodi italaumiwa.

Mimi nasema kwamba wizara na waziri ndio *answerable* wa masuala yote yanayohusiana na shirika na bodi, kwa hivyo awe na mamlaka kamili ya kuweza kuendesha shirika kwa mujibu wa sheria ilivyotungwa na kwa mujibu wa kanuni zilivyoekwa.
Hii ni mara ya pili Mhe. Salmin anapotosha. Wakati alipochangia kwenye bajeti iliyopita alisema kwamba waziri alizuia biashara iliyokuwa inafanywa na watu wameuza karafuu Singapore, waziri akazuia.

Nilimshauri Mhe. Mwakilishi kwamba wakati wowote anapopata maburungutu kama haya basi aje anione na mimi nitatia, hata Mwenyezi Mungu anasema kwamba ikiwa usisikilize maneno ya upande mmoja lazima usisikilize maneno ya pande mbili, *you have no right if you haven't done research*. Fanya *research* halafu ndio useme. (Makofi).

Kwa hivyo mimi nilikuwa nataka nikuhakikishie Mhe. Mwenyekiti, kwamba suala alilozungumza Mhe. Salmin Awadh Salmin si suala la bodi hii. Bodi hii iliyoundwa na kwa sheria hii iliyopitishwa katika Baraza tukufu hili hapa hakujatokea hasara ya shilingi laki sita, hii ni hasara iliyotokea nyuma kabla ya kuundwa bodi.

Mhe. Mwenyekiti, na hii imetokana na *incompetence* ya mtu na sio mfumo, uwezo wa mtu ni kitu mbali na mfumo wa sheria ni kitu mbali. Kwa hivyo ikiwa kuna mtu kasababisha hasara ya shilingi laki sita itakuwa ni mtu lakini sio mfumo au sheria tuliyotunga hapa. La busara ni kuwa tuhakikishe kwamba tunawateuwa kuchukua nyadhifa hizi wawe ni watu *competent* watu wenye uwezo.

Mhe. Mwenyekiti, suala la dola laki sita lililozungumzwa hapa ni hasara iliyotokana Meneja wa ZSTC aliyepita kwa kutia mikataba saini ambayo kuwa mikataba hiyo hakushauriana na mtu yeyote wala haikupita kwa Mwanasheria Mkuu. Sisi ni kawaida yetu kwamba mikataba yote ya serikali lazima ipitishwe kwa Mwanasheria Mkuu ipasishwe ndio iweze kutumika.

Sasa kutokana na uwezo wake mdogo na *business as usual* akatafuta mkataba wake mwenyewe akatunga mwenyewe na hao anaowauzia, akafanya mkataba wake akaweka saini bila ya kuzingatia kanuni na sheria za mfumo ziloekwa.

Kwa hivyo hasara iliyotokea ya dola laki sita ilitokana na *incompetence* au uwezo wa huyu meneja aliyekuwepo kwamba hakuweza kufikiri kwamba mikataba yote lazima iridhiwe na Afisi ya Mwanasheria Mkuu na vile vile Baraza hili akenda katika kipengele kama kutakuwa matokeo yoyote yale, basi kesi hiyo iende ikahukumiwe London kwenye Shirika la GAFTA, ambapo sifikiri kama Mwanasheria Mkuu atakubali kwamba mkataba huo unatiwa saini iende ikahukumiwe kesi London kwa kufuatia Shirika la GAFTA isipokuwa ni utashi wake tu wa kufanya mikataba hiyo ya kipuuzipuuzi.

Sasa nasema kwamba katika bodi hii mpya na kwa sheria hii mpya tuliyotunga hakuna hata mkataba mmoja uliotiwa ambao una matatizo, hayo ni matatizo ya nyuma si ya leo. Kwa hivyo Mhe. Salmin alikuwa anapotosha Baraza hili, naomba niweke sawa kwamba bodi mpya iliyoundwa haijafanya matatizo hayo ya dola laki sita.

Mimi nataka nimuhakikishie katika Baraza lako tukufu kwamba hakuna mtu yeyote anayoingilia ZSTC, hakuna anayeingilia meneja na meneja huyo mkurugenzi akaanguka chini kwa *pressure* akalazwa mimi sijasikia suala hili, na kwa nini aiingie *pressure* wakati yeye sio aliyeweka saini mkataba huo wala yeye siye aliyesababisha hasara hiyo, isipokuwa haya ni maneno ya kutunga tunga tu.

Mimi ni mfanyakazi wangu sijasikia kama kaanguka kwa *pressure* akapelekwa hospitali kwa sababu ya hasara ya dola laki sita. Nasema kwamba tufanye utafiti wa kutosha halafu ndio tuzungumze katika Baraza hili.

Baraza hili ni chombo kikubwa, chombo kitukufu katika nchi lazima tukipe heshima yake. Milango ya wizara yangu upo wazi wakati wowote naomba mwenye suala aje aulize na ataelezwa na akishaelezwa ana hiyari yake ya kuja kusema. Lakini mambo kama haya ya kupotosha wananchi na kupotosha Baraza hili, haitutendei haki sisi mawaziri, haitendewi haki wizara yangu wala haitendewi haki Baraza hili.

Kwa hivyo naomba niweke *very clear* suala hili kwamba bodi hii mpya na wizara yangu haiingilii kabisa kazi zao wanafanyakazi zao kwa mapana na marefu. Lakini natoa indhari mimi kama waziri sitosikia kunafanyika madudu ZSTC nikanyamaza kimya, kwa sababu mimi ndio *answerable* katika Baraza hili, mimi ndio *answerable* kwa Makamu wa Pili wa Rais huyu hapa, mimi ndiye *answerable* kwa Rais wa Zanzibar. Kwa hivyo hata ikiwa mwenyekiti wa bodi akifanya madudu yake, mkurugenzi mimi ndiye *answerable*, kwa hivyo nitachunga kila hatua inayofanyika bila ya kuathiri sheria na kanuni tulizotunga.

Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti. Ahsante sana. (Makofi)

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa nianze kabisa kumshukuru Mwenyezi kunijaalia leo hii tukawa tupo hapa katika ukumbi wa Baraza la Wawakilishi kutekeleza majukumu ya serikali.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kuwapongeza wajumbe wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari kwa kuweza kuupitia mswada huu kifungu baada ya kifungu na hatimaye ukaja kwenye Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, pia nimpongeze Mwenyekiti wa Kamati kwa kuweza kuwasilisha ripoti yake kwa ufanisi na upeo mkubwa. Mhe. Mwenyekiti, pia niwapongeze wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa kuweza kuuchangia mswada huu kwa upeo na ufanisi mkubwa na hamasa kubwa iliyotokea kwenye Baraza hili la Wawakilishi kwenye mswada huu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitatoa ufafanuzi mdogo unaohusiana na chombo chetu cha habari yaani ZBC. Mhe. Mwenyekiti, wajumbe wengi wamezungumzia kuhusu chombo chetu cha ZBC kama kinafanya kazi kisiasa. Mhe. Mwenyekiti, nataka niwahakikishie wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kuwa chombo chetu hiki cha ZBC hakifanyi kazi kisiasa, kinafanya kazi kwa mfumo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Nawaomba Waheshimiwa Wawakilishi hofu hiyo muiondoshe.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuendelea kutoa mchanganuo unaohusiana na na mswada, niende kwenye wajumbe wamechangia sehemu kubwa kuhusu chombo cha ZBC hiki yanapotokea matokeo ya serikali na ya wananchi huwa hakifiki haraka.

Nataka pia niwatoe wasi wasi Waheshimiwa Wawakilishi musiwe na wasi wasi chombo chetu hiki huwa kinafika panapokuwa na matokeo yote yale ya maafa na hata matokeo yaliyotokea kwenye ajali ya meli. Mimi mwenyewe binafsi nikiwa Naibu Waziri nakuwa nipo na waandishi wa habari bega kwa bega mpaka shughuli hii inamaliza.

Mhe. Mwenyekiti, pia niende kwa mama Mhe. Panya Ali Abdalla, yeye ameeleza kuhusu chombo chetu hiki cha habari kuhusu michezo au vikundi mbali mbali vya wasanii ambavyo vinaoneshwa kwenye TV kuwa vinakiuka maadili. Nataka nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi kuwa ipo bodi ya sensa na filamu. Kwanza inapitia halafu ndio wanapeleka ZBC kwa vile vipindi vioneshwe kwa jamii.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea niendelee kwenye kutoa taarifa mbali mbali za kwenye jamii kama kilimo, afya ya jamii. Kwa kweli nawahakikishia Wajumbe wa Baraza vipindi hivi vipi na vinaendelea kwa sababu ya kusema hivyo mimi mwenyewe binafsi nikiwa pamoja na Naibu Waziri wa Afya tulizindua vipindi hivi vya afya ya jamii ZBC, na kwa kweli vipindi hivi vinatoka siku baada ya siku na vipindi vyengine ambavyo ni vya maadili ya Kiislamu huwa vinatoka na vipindi vyengine vinavyohusiana na jamii na wananchi kwa jumla.

Mhe. Mwenyekiti, niende mchangio alioendelea nao Mhe. Panya kuhusu ving'amuzi. Kwa kweli kuhusu ving'amuzi sasa hivi tunaendelea vizuri na nataka niwahakikishie Wajumbe hivi sasa tumetoa muongozo kwenye Wizara yangu, kila wizara wanaorodhesha majina na kupeleka kwenye Tume yetu ya Utangazaji ili ving'amuzi vitakapotoka wawe ni watu wa mwanzo.
Namuomba Katibu wa Baraza la Wawakilishi aorodheshe majina ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na wafanyakazi ayapeleke Tume ya Utangazaji kwa ajili ya kuja kupata ving'amuzi hivyo. Lakini nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe kuwa ving'amuzi hivyo si bure vinatolewa kwa pesa na kila Mwakilishi ajiandae kwa hilo.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea kuhusu michango iliyotolewa kuhusu mfanyakazi wetu aliyeopo Dar es Salaam Juma Mmanga. Ninataka niwatoe wasi wasi Waheshimiwa Wawakilishi

waliochangia suala hili kuhusu mfanyakazi wetu huyo, niwahakikishie kwamba mimi binafsi tulifanya ziara tukenda TBC na wajumbe wa Kamati ya Habari, kwa kweli mkurugenzi alimwambia pale mfanyakazi huyu nataka nimchukue, akamwambia nakuhakikishia mbele ya Naibu Waziri wa Habari, mimi sitofanya hivyo ninaitumikia Serikali yangu ya Mapinduzi ya Zanzibar wakati wowote ule mpaka mwisho wa maisha yangu. (Makofi).

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia nawaomba Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi nyote kwa heshima na taadhima mswada huu muupitishe na tuendelee na majukumu yetu kwa upeo zaidi moja hadi mbili hadi kumi ili mswada huu ufanye kazi vizuri kwa ufanisi.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. (Makofi).

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi (Kny: Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo): Mhe. Mwenyekiti, awali kabisa sina budi kutoa shukurani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Baraza lako kupokea na kuujadili mswada wa sheria ya kuanzisha Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC).

Kama wajumbe wengi walivyoeleza kwamba mswada huu una umuhimu mkubwa katika kuendeleza tasnia ya utangazaji nchini. Nataka nikubaliane na Wajumbe wote kwamba kuna haja kubwa ya kuimarisha na kuendeleza huduma za habari zitolewazo na vyombo vyetu vya habari ili vyombo hivyo viwe kioo cha jamii.

Mhe. Mwenyekiti, mswada huu umechangiwa na wajumbe takriban 22 akiwemo:-

1. Mhe. Salim Abdalla Hamad
2. Mhe. Mohamed Haji Khalid
3. Mhe. Abdi Mosi Kombo
4. Mhe. Asha Bakari Makame
5. Mhe. Ali Salim Haji
6. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa
7. Mhe. Marina Joe Thomas
8. Mhe. Abdalla Juma Abdalla
9. Mhe. Nassor Ali Salim
10. Mhe. Hamza Hassan Juma
11. Mhe. Ismail Jussa Ladhu
12. Mhe. Rufai Said Rufai
13. Mhe. Hija Hassan Hija
14. Mhe. Bikame Yussuf Hamad
15. Mhe. Hamad Masoud Hamad
16. Mhe. Salmin Awadh Salmin
17. Mhe. Ashura Sharif Ali
18. Mhe. Abdalla Mohamed Ali
19. Mhe. Fatma Said Mbarouk
20. Mhe. Nassor Ahmed Mazrui
21. Mhe. Bihindi Hamad Khamis

Kwa ujumla wajumbe walichangia sana kuhusu suala la utafutaji, ukusanyaji na utoaji habari na kuhusisha na masuala ya maadili, mila, silka na uhuru wa vyombo vya habari na uhuru wa upatikanaji habari.

Aidha, wajumbe walizungumzia sana udhaifu mkubwa uliopo ZBC katika ngazi ya uongozi, watendaji na uchache wa vitendea kazi. Nataka kuwahakikishia Wajumbe kuwa mambo yote yaliyozungumzwa yatachukuliwa kwa uzito mkubwa na kujitahidi kadri itakavyowezekana kuyapatia ufumbuzi yakiwemo matatizo ya wafanyakazi pamoja na maslahi yao.

Mhe. Mwenyekiti, napenda nikubaliane na wachangiaji kuwa vyombo vyetu vinapaswa kuimarishwa na kuwezeshwa kiutendaji kwa lengo la kutimiza azma iliyopelekea kuanzishwa kwa vyombo hivyo. Kutokana na ukweli huo Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo itayachukulia kwa uzito unaostahili michango hiyo na kuifanyia kazi, maelekezo na ushauri uliotolewa na Wajumbe kwa kuamini kwamba kufanya hivyo tutaweza kufanikiwa.

Mhe. Mwenyekiti, napenda nikiri kwa mara nyengine tena kwamba michango yote iliyotolewa na Wajumbe ilikuwa ni mizuri na ya kujenga. Kutokana na ukweli huo ni vyema kueleza kwamba wizara imefarijika sana na michango iliyotolewa na Kamati ya Mifugo, Habari, Uwezeshaji na Utalii na wajumbe wote waliochangia.

Ninachoweza kusema au ninachoweza kuahidi ni kwamba michango hiyo imepokelewa na itazingatiwa kwa kina na itachukuliwa hatua za haraka katika kuifanyia kazi. Miongoni mwa michango iliyotolewa na kamati, mapendekezo mengi yamekubaliwa moja kwa moja kwa kufanya marekebisho kwa baadhi ya vifungu vilivyowasilishwa kwenye mswada.

Marekebisho ya vifungu hivyo ni kama vile vilivyoorodheshwa kwenye jadweli ya marekebisho. Hata hivyo baada ya kutafakari kwa undani kuna baadhi ya mapendekezo yaliyotolewa wizara imeona ni vyema kubakia kama yalivyo kwenye mswada.

Mapendekezo hayo ni kama ifuatavyo.

Kwanza katika kifungu cha 3 ilipendekezwa kuongezwa maneno yatakayobainisha makao makuu ya shirika yatakapokuwepo. Wizara imeona mahali itakapokuwepo makao makuu ni suala zaidi la kiutawala, hivyo isingependeza au isingepaswa kuingizwa kwenye sheria.

Aidha kutotajwa sehemu itakayokuwepo makao makuu ni kuendeleza uzoefu uliopo wa sheria nyingi za mashirika yetu.

Pili katika kifungu cha 11 (2) (a), kamati na baadhi ya wajumbe kutaka kiwango cha shahada ya pili kitumike kuwa ni moja ya sifa ya mtu atakayeteuliwa kuwa mkurugenzi mkuu wa shirika. Wizara inaona sifa iliyopo kwenye mswada ya mteuliwa awe ni mhitimu kutoka katika chuo kikuu iendelee kubakia.

Wizara inaona kwamba kinachohitajika ni kupata watendaji wenye uwezo mkubwa wa kulisimamia shirika hilo. Sifa iliyotajwa ya kuhitimu chuo kikuu inaweza kukidhi mahitaji hayo, kwani mamlaka ya uteuzi itakuwa na wigo mpana wa kutafuta mtendaji mkuu mwenye uwezo

mkubwa wa kiutendaji kwa kuangalia kwa undani sifa za uwezo, uzoefu na maarifa ya mtu badala ya kujifunga sana kwenye kigezo cha taaluma.

Tatu katika kifungu cha 3 (4) kamati na baadhi ya wajumbe wamependekeza kufutwa kwa kifungu kinachoweka masharti ya mkurugenzi mkuu kutekeleza kazi zake kwa kipindi cha miaka mitano na kuweza kuteuliwa tena kwa kipindi kama hiki kutokana na utendaji wake bora.

Wizara imeona kuwa kifungu hicho kiendelee kuwepo. Wizara inaona kuendelea kuwapo kwa kifungu hicho kutaondoa uwezekano wa mtu kujijengea himaya au ufalme katika uongozi kwenye taasisi kama hii, kwani kila mkurugenzi atakayeteuliwa atalazimika kufanya kazi hiyo kwa mkataba maalum ili kuililetea shirika manufaa na tija.

Mkataba huo utaweka wazi uwezo wa kuondolewa kwa Mkurugenzi Mkuu huyo wakati wowote atakapoharibu. Aidha kuwepo kwa kifungu hiki utatoa nafasi kwa watakaoteuliwa kutumia ujuzi na maarifa mwisho wa uwezo wao ili kujijengea sifa za kuweza kuteuliwa tena.

Mhe. Mwenyekiti, hiki ni chombo kinachopaswa kujiendesha kibiashara, hivyo kuwepo kwa kifungu hiki kitasaidia watendaji wakuu kujituma ili kuliletea tija shirika na wanaposhindwa kufanya hivyo, wanajua wazi kwamba watapoteza nafasi zao.

Nne, Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 18 kimeamuliwa kufutwa na kuandikwa upya ili kutoa fursa zaidi kwa shirika katika kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia maelekezo ya sera ya habari ya mwaka 2006 na sheria nambari 2 ya mwaka 1997 ya Tume ya Utangazaji ya Zanzibar, ambayo inasimamia na kuratibu shughuli zote zinazofanywa na vyombo vya utangazaji vya Zanzibar.

Tano, Mhe. Mwenyekiti, imetolewa hoja na Mhe. Mohammed Haji ya kueleza kwamba Shirika la ZBC kwa muda sasa linafanya kazi, lakini hakuna sheria yoyote iliyoanzishwa taasisi hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, ilivyo ni kwamba shirika hilo liliundwa kwa mujibu wa mamlaka ya kikatiba aliyonayo Mhe. Rais wa Zanzibar. Shirika hilo liliundwa chini ya tamko la kisheria yaani *legal notices number 111* la mwaka 2011.

Aidha, aligusia kifungu cha 13(2) kinachozungumzia mfanyakazi kutotiwa hatiani anapofanya kazi zake kwa nia njema. Mhe. Mwenyekiti, kifungu hiki kinakusudia kuwakinga wafanyakazi wa ZBC kutiwa hatiani wakati wakitekeleza majukumu yao

Hiyo ni kutafuta mfumo wa kimataifa wa vyombo vya habari, kwani jukumu la makosa yanayofanywa na waandishi wa habari duniani kote halibebeshwi kwa waandishi na badala yake dhima yote hiyo huchukuliwa na chombo chenyewe.

Hivyo kifungu hiki hakina maana kwamba wafanyakazi wakifanya vitendo vya utovu wa nidhamu na vinavyokwenda kinyume na kanuni za utumishi kwamba hawatochukuliwa hatua zinazofaa.

Saba, Mhe. Abdalla Juma alitaka kufahamishwa, alisema Mhe. Waziri atawateuaje wajumbe watakaoingia kwenye bodi kwa nyadhifa zao, lakini wakapoteza sifa za kuwa wajumbe kwa kushindwa kuhudhuria vikao.

Mhe. Mwenyekiti, wajumbe wote isipokuwa mwenyekiti wanaoingia kwenye bodi wanateuliwa na Waziri. Kwa wale wanaoingia kwa nyadhifa zao watakapopoteza nafasi zao za kuwa wajumbe basi waziri atawasiliana na taasisi zinazohusika kutuma majina mengine, ili waziri aweze kuyateua.

Nane, Mhe. Nassor Salim Ali, alitaka kujua kwa nini Waziri ateue wajumbe watatu badala ya wawili. Mhe. Mwenyekiti, shirika hili kama ilivyoelezwa na wajumbe karibu wote kwamba lina umuhimu mkubwa kwa taifa, hivyo linahitaji kuwa na washauri wenye fani nyingi, zikiwemo za kiuchumi, ufundi, uhusiano wa kitaifa na kimataifa na pia taaluma za mambo ya mawasiliano, habari na biashara. Kutokana na sababu hiyo imeonekana haja ya kuyatumia matakwa yaliyotolewa kwenye sheria ya mitaji ya umma ambayo ndiyo inayozingatiwa kuundwa kwa shirika hili. Mhe. Mwenyekiti, matakwa hayo ni kulitaka shirika kuwa na bodi isiyozidi wajumbe saba.

Mhe. Hamza Hassan Juma, na yeye alitaka kujua kuhusu madai ya wafanyakazi wa *ZBC* kuwa ni miongoni mwa madeni yatakayoridhiwa na Shirika la *ZBC*. Nataka kumuhakikishia Mhe. Hamza Hassan kwamba madeni hayo yataridhiwa na shirika na yatawekewa utaratibu maalum wa kuwalipa wafanyakazi wanaodai. Mhe. Mwenyekiti, madeni hayo ni makubwa kiasi cha kwamba yanaonekana kuwa ni tishio la kushindwa kulipika. Hali hiyo imejitokeza kutokana na idadi kubwa ya wafanyakazi kusafiri katika ziara ambazo sio miongoni mwa zile zilizopangwa na shirika. Safari hizo nyingi ni zile za ziara za masomo ya muda mfupi nchini China, ambazo kuzikataa ni kuwarejesha na kuwakatisha tamaa wafanyakazi na kuzikubali ni kuongeza deni ambalo hivi sasa ni kubwa mno.

Mhe. Mwenyekiti, kinachofanyika hivi sasa ni kuendelea kuwapatia fursa hizo wafanyakazi wa shirika na pia kuwaombea waendelee kuwa wastahamilivu wanapolipwa kidogo kidogo. Kwa hivyo, shirika linaendelea kuwalipa wenye madeni hayo kidogo kidogo.

Kumi, Aidha maslahi ya wafanyakazi kama ilivyoelezwa na wajumbe mbali mbali, yatazingatiwa ikiwa ni pamoja na kuyapatia ufumbuzi matatizo yaliyopo ikiwa ni pamoja na vifaa na vitendea kazi.

Kumi na moja, chuo kinacholingana na Chuo Kikuu ni taasisi zenye kutoa elimu za juu inayolingana na hadhi ya elimu ya Chuo Kikuu, lakini hazijafikia kiwango cha kuitwa Chuo Kikuu, kama ilivyokuwa Chuo cha Mzumbe kilichopo Morogoro.

Vile vile Mhe. Ismail Jussa Ladhu, alitaka kuwekwa tafsiri ya maneno “maslahi ya umma”. Tunakubaliana na hoja hiyo na tafsiri itakayofaa ni misingi inayosimamia na kuendeleza umoja wa kitaifa, maelewano ndani ya jamii, kutetea na kulinda uhuru na haki za raia na haki za kibinadamu.

Kumi na tatu, pia alitaka kufanyiwa marekebisho kifungu cha 3 kilichosema ‘shirika linaweza kukopa kiwango chochote cha fedha kinachohitajika kwa ajili ya shirika’. Jibu ni kwamba tunakubaliana na wazo hilo na sasa kifungu hicho kitasomeka kama ifuatavyo.

‘Kukopa kiasi chochote cha fedha kinachohitajika kwa ajili ya shirika baada ya kupata idhini kutoka serikalini’.
Aidha, Mhe. Ismail Jussa alionesha wasi wasi kwamba kwenye kifungu cha 7(c), kinachoelezea shirika kuingia ubia au ushirikiano na serikali. Taasisi au shirika lolote wasi wasi huu unaweza kuondolewa na kifungu cha (c) cha uwezo wa Waziri.

Vile vile Mhe. Ismail Jussa alitaka kifungu cha 10(2), kilichotoa uwezo wa bodi kukasimu mamlaka yake kwa mjumbe, isipokuwa kwa kijifungu 1(c) (d) na (e). Hiyo maana yake ni kwamba bodi inaweza kukasimu madaraka kwa kazi chache tu ambazo ni zile za kuishauri shirika katika huduma za utangazaji, kuandaa na kupitia sera ya shirika au kufanya tathmini juu ya mfumo na taratibu za utendaji kazi wa shirika na wafanyakazi. Mhe. Mwenyekiti, kimsingi ikiwa ndani ya bodi kutakuwa na mjumbe mwenye taaluma hizo, basi anaweza kupewa jukumu la kutekeleza kwa niaba ya bodi.

Jengine Mhe. Ismail Jussa pia alitaka kujua Mkurugenzi Mkuu atawajibika kwa nani. Mkurugenzi Mkuu atawajibika kwa bodi na kuwa hali hiyo haijitokezi wazi wazi, tutafanya ionekane wazi wazi.

Mhe. Hija Hassan Hija wa Jimbo la Kiwani, alipendekeza kuondolewa kwenye bodi mjumbe kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu. Wizara inaona mjumbe kutoka ofisi hiyo ni muhimu kuwemo, kwani kuwepo kwake kutasaidia kutoa michango katika masuala ya sheria, kwani katibu wa bodi ana majukumu tofauti na wajumbe,

Aidha, Mhe. Hija Hassan na baadhi ya wajumbe walitaka Mwenyekiti wa Bodi awe na sifa ya angalau kiwango cha diploma. Wizara inaona Mwenyekiti, kuwekewa sifa za aina hiyo kunaweza kuzuia watu wenye sifa kuteuliwa kutokana na uzoefu na maarifa waliyonayo. Ipo mifano mingi inayoonesha kwamba fani ya uongozi haitegemei sana sifa za elimu na hata sisi miongoni mwetu tunakosa sifa za aina hiyo na tunaongoza vizuri tu.

Mhe. Hija Hassan alitaka kuongezwa kwa kifungu 10(1) (h) kitakachoipa bodi kazi ya kukusanya maoni ya umma. Kimsingi jukumu la kukusanya maoni na malalamiko ni la utawala na uendeshaji na haliko kwenye bodi.

Kuhusu sifa za Mkurugenzi Mkuu kutamkwa wazi kwamba zianzie kwa mwenye kiwango cha Shahada ya Kwanza. Nakubaliana na wazo hili la Mhe. Hija Hassan.

Vile vile Mhe. Bikame Yussuf Hamad alitaka kufahamu kwa nini wakuu wa vitengo vya shirika wateuliwe na bodi na sio waziri. Jibu ni kwamba kazi ya kuajiri na kuteua wafanyakazi wa shirika ni miongoni mwa majukumu ya bodi, isipokuwa waziri ndiye anayeteua hiyo bodi.

Mhe. Mwenyekiti, pia Mhe. Hamad Masoud Hamad ametaka kujua mswada huu wa sheria umekopiwa kutoka sheria ya nchi gani. Mhe. Mwenyekiti, mswada huu haukukopiwa kutoka

katika nchi yoyote duniani, lakini unatokana na mapitio yaliyofanywa kwenye sheria za mashirika karibu yote makubwa ya Afrika ya Mashariki yanayolingana na mazingira yetu yakiwemo *KBC, UBC, TBC na MBC.*

Mhe. Hamad Masoud pamoja na wajumbe wengine akiwemo Mhe. Abdalla Mohammed Ali, walitaka kujua kwa nini *ZBC* ilianza zamani lakini inashindwa na vyombo vilivyoanzishwa hivi karibuni. Ninachoamini Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo ni kwamba *ZBC* haiko nyuma kama inavyofikiriwa na watu wengine. Inawezekana kigezo cha kulinganisha taasisi hizo hakiko katika uwanja wa taaluma yenyewe, kwani tokea mwaka 1997 mpaka 2011 zimefanyika tafiti tofauti tatu za kitaaluma na zote zimethibitisha kuwa vyombo vya *ZBC* viko juu kitaaluma na kimaadili, na ndio maana taasisi zote za Tanzania Bara na za Zanzibar, zinapoanzishwa vyombo vyao huchukua wafanyakazi kutoka *ZBC.*

Mhe. Salmin Awadh Salmin, alitaka kujua wafanyakazi wanaokaa zamu za usiku kama wanalipwa maposho yao. Jibu ni kwamba wafanyakazi wa vituo vya redio na TV wanaingia kwa zamu na wale wanaozidi muda wa saa zao za kazi wanalipwa posho zao.

Vile vile Mhe. Salmin Awadh alipendekeza wajumbe wa bodi wasizidi sita kama ilivyo katika sheria ya mitaji ya umma. Ilivyo ni kwamba sheria ya mtaji wa umma inataka wajumbe wasizidi saba ambao ndio waliomo kwenye mswada huu. Aidha, alitaka awepo Makamu Mwenyekiti wa Bodi. Wazo hili tunalikubali.

Pia Mhe. Salmin Awadh na wajumbe wengine wakiwemo Mhe. Ismail Jussa na Mhe. Ashura Sharif, walitaka kifungu cha 9(3) kirekebishwe. Wazo hili tunalikubali na kwamba sasa kitasomeka kama ifuatavyo:

“Ikiwa Katibu atakuwepo kutokana na ugonjwa au sababu nyengine yoyote ile, basi bodi itateua mfanyakazi mwengine wa shirika mwenye sifa kama alizonazo katibu kutekeleza majukumu ya katibu wa bodi kwa muda ambao hatokuwepo”.

Mhe. Abdalla na Mhe. Fatma Mbarouk Said walitoa pendelezo la sheria ya shirika hili, kuunganisha gazeti la Zanzibar Leo au kuleta sheria ya habari. Mhe. Mwenyekiti, katika tasnia ya habari vyombo kukusanya na kusambaza habari vinatofautiana kimalengo, matakwa na teknolojia. Sekta ya utangazaji haiwezi kuchanganywa na sekta ya uchapaji, hizi ni sekta mbili tofauti na ndio maana serikali ikaleta mswada huu wa utangazaji, tofauti na ule ulioletwa wa Shirika la Magazeti ya Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kutoa ufafanuzi wa baadhi ya hoja zilizotolewa na Wajumbe. Sasa naomba Baraza lako tukufu kukubali na hatimaye kuupitisha mswada huu, ili uweze kuwa ni sheria. Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, sasa niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyooshe mikono juu. Waliokataa. Waliokubali wameshinda. *(Makofi).*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: (Kny: Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo): Mhe. Mwenyekiti, ilivyokuwa Kamati ya kutunga sheria imeupitia mswada wangu kifungu kwa kifungu na kuukubali pamoja na marekebisho yake. Sasa naliomba Baraza lako tukufu likubali. Naomba kutoa hoja.

Samahani Mhe. Mwenyekiti kuna marekebisho hapa.

Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba kutoa taarifa kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya kutunga sheria ili kuupitia mswada kifungu baada ya kifungu.

KAMATI YA KUTUNGA SHERIA

Mswada wa Sheria ya Shirika la Utangazaji la Zanzibar ya Mwaka 2012

Sehemu ya Kwanza

Masharti ya Awali

Kifungu 1 Jina fupi na kuanza kutumika

Kifungu 2 Ufafanuzi

SEHEMU YA PILI

Kuanzishwa kwa Shirika, Kazi na Majukumu yake

Kifungu 3 Kuanzishwa kwa shirika pamoja na marekebisho yake

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, naomba nitumie fursa hii kumshukuru sana Mhe. Kaimu Waziri kwa ufafanuzi wake mzuri na wa kina wa hoja mbali mbali ambazo tulizitoa. Pia namshukuru kwa kukubali pendekezo ambalo nililitoa katika kifungu hiki kwenye kijifungu kidogo cha (3), nilichokuwa naomba marekebisho madogo tu katika lile pendekezo lake. Hiki kinahusu Mhe. Mwenyekiti, pale mwisho kabisa kiliposema kwamba ule uwezo wa kukopa kiasi chochote cha fedha kitahitajika kwa ajili ya shirika, nilisema kuwa ni muhimu kikawekewa kidogo kidhibiti fulani ili kisije kikakopwa kiasi kikubwa cha fedha ukawa mzigo kwa serikali.

Sasa katika marekebisho aliyoyafanya Mhe. Waziri amesema kwamba tuongezee pale baada ya kupata idhini kutoka serikalini. Kwa hivyo, serikalini *is too general*, lakini ile *concept* au dhana naikubali. Kwa hivyo, nilikuwa nadhani na kwa sababu Waziri mwenye dhamana ya mashirika haya ni waziri wa fedha, ambaye bahati nzuri vile vile pia ndiye mwenye dhamana ya masuala

yote ya fedha katika nchi hii. Mimi nilikuwa naomba tungekuwa na zaidi kwa kuweka kwamba ‘baada ya kupata idhini ya waziri wa fedha, au waziri anayeshughulika na masuala ya fedha’, itakuwa ni serikali lakini tungetaja hasa kitaratibu mtu ambaye ndiye mwenye dhamana ya yale mashirika, lakini kwa wakati mwengine ndiye mwenye dhamana ya fedha katika nchi hii. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: (Kny: Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo): Nashukuru Mhe. Mwenyekiti, nimeyasikia mawazo ya Mhe. Ismail Jussa na ninayakubali ni baada ya kupata idhini kutoka kwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Nashukuru Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Kifungu 3

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka nimpongeze sana Mhe. Waziri, kwa kuwa msikivu na kila pale penye matatizo alikubali yale matatizo yawe ni yetu pamoja na tushirikiane kwa ajili ya kuyatekeleza. Naamini tukienda kwa moyo huu basi mambo yetu mengi yatakwenda vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nina ushauri katika kifungu cha 3(3) kwamba kwa kuwa Mhe. Waziri alikubali kwamba uanzishwaji wa hili shirika ni moja kwamba litarithi mali zilizokuwepo pamoja na madeni.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri ameelezea kwamba haya madeni mengine yapo muda mrefu na mengine ni ya hivi karibuni, kwa hivyo yataanza kushughulikiwa kwa utaratibu maalum. Sasa mimi kitu ambacho nakiomba, basi itumike busara zaidi katika kuyalipa haya madeni, yangeangaliwa zaidi kwanza yale yaliyokuwa ni ya muda mrefu sana, halafu baadae tukamalizia na haya mengine. Sasa na huko kwengine Mhe. Mwenyekiti, katika suala zima la maslahi ya wafanyakazi wetu, niliwahi kushauri kwamba ni vizuri sasa hili shirika, kwa sababu sasa hivi kazi zao zitakuwa ni nyingi na ni ngumu zaidi na za ufanisi zaidi, basi ni vizuri kuangaliwa ile *scheme* ya watendaji wa shirika la habari ili kuweza kwenda sambamba na kasi ya mabadiliko. Lakini vile vile na wao kuwajenga ari katika kuhakikisha kwamba huo ubunifu wao baada ya kwamba sasa hivi wanakuwa wanaibiwa na mashirika mengine, na wengine sasa shirika liweze kuwaiba na wale waliokuwa huko katika mashirika mengine au kuweza kuwaendeleza zaidi hao waliokuwepo.

Kwa hivyo, kitu ambacho kitatuwezesha kuweza kufikia hatua hiyo, ni kuangalia *scheme*, kuangalia na majukumu yao ili kuweza kuwapa motisha zaidi wafanyakazi wetu wa mashirika haya ya utangazaji ili waweze kufanya kazi kwa ufanisi.

Mhe. Mwenyekiti, nadhani kama atahitaji kutoa ufafanuzi zaidi, lakini kubwa nilikuwa nataka kusisitiza na mimi kutoa mawazo yangu, kwa sababu huko kwenye bodi nitakuwa sipo. Kwa hivyo, natoa mawazo yangu hapa hapa ili waweze kuyafanyia kazi. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: (Kny: Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo): Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nimeyasikia mawazo ya Mhe. Hamza Hassan na kwa kweli ni mawazo mazuri tu. Kwa yale madeni ambayo kama alivyopendekeza kuwa wale wenye madeni makubwa basi tutaanza na wao, kwa sababu ni kweli hatupendelei kuona kwamba shirika tunakwenda kwenye mfumo mwengine, halafu bado kuna malalamiko. Kwa hivyo, hilo tutalitekeleza na namuomba Mhe. Hamza Hassan, nachukua ahadi kwamba tutalitekeleza kwa wale ambao wenye madeni makubwa na vile vile *scheme of work* tutaiangalia kama alivyopendekeza. Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu 3 Kuanzishwa kwa shirika pamoja na marekebisho yake

Kifungu 4 Muhuri wa shirika pamoja na marekebisho yake

Kifungu 5 Malengo ya shirika pamoja na marekebisho yake

Kifungu 6 Kazi za shirika pamoja na marekebisho yake

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Nashukuru tena Mhe. Mwenyekiti. Mhe. Mwenyekiti, katika mchango wangu nilitanabahisha kwamba kifungu cha 6(b) kama kilivyorekebishwa na kamati na tukichukulia tunaposema pamoja na marekebisho yake ni kwamba tunajumuisha pamoja na marekebisho ya kamati, kwamba tukikipokea hivyo kitakuwa kinapotosha kabisa kwa maoni yangu ile dhamira iliyokusudiwa ambayo unaifahamu kwa ufasaha zaidi ukisoma ule mswada wa Kiingereza.

Sasa pamoja na kumshukuru Mhe. Waziri kwa kufanya kazi nzuri ya majumuisho, lakini katika hili sikumsikia, naomba kama sikumsikia vizuri basi anisaidie tena. Nilichokuwa nimekisema, kwa ajili ya kumkumbusha zaidi Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, ukisoma waraka wa kamati kwenye kifungu cha 6(b) neno “kuchukua” lililo baina ya neno “na vipindi” linafutwa na badala yake linaingizwa neno “kutumia” hilo halina matatizo.

Lakini halafu inasema maneno “vya kigeni” yanafutwa na badala yake yanaingizwa maneno “vya ndani” na neno “wazawa” linafutwa na kuingizwa neno “jamii”.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, katika mchango wangu nilisema kwamba tukiyakubali mapendekezo ya kamati, maana yake tunaizuia kabisa *ZBC* kwamba haitoweza kutangaza kabisa vipindi vya kigeni.
Vile vile Mhe. Mwenyekiti, ukiisoma ile ya Kiingereza, naomba niisome,

Kifungu cha 6(b)

“The functions of the Corporation shall be to:-

(b) *Produce quality local programming and to adapt foreign programs to suit local needs;*

Sasa imeweka msisitizo wa kuandaa vipindi vya ndani, lakini pia kuchukua vipindi vya nje ambavyo vitakuwa vinakwenda sambamba na mahitaji na maadili ya ndani. Ndio maana mimi nikasema turekebishe zaidi kwamba mbali kuwa tukibakishe kwanza kama kilivyokuwa kile cha Kiingereza. Lakini na lile neno lililokuwa limewekwa katika Kiswahili kwamba "wazawa" na kamati ikapendekeza neno "jamii". Nikasema tuseme hasa kwamba "kwa mujibu wa mahitaji ya jamii ya Kizanzibari, au maadili ya jamii ya Kizanzibari".

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa nataka kutoa hoja, kama nilivyotoa katika mchango wangu, na sasa namuomba waziri anipe maelezo yake kwamba je tunapitisha vipi, kwamba ni vile ambavyo kamati ilipendekeza katika marekebisho, ama tunabakia na yale maudhui ambayo yalikuwemo katika Kiingereza na ambayo tunatakiwa tuyatafsiri vizuri katika Kiswahili ili yaweze kuleta ile maana ambayo imekusudiwa. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: (Kny: Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo): Ahsante Mhe. Mwenyekiti. Unajua katika majumuisho kuna mambo mengine huwa tunayasahau, lakini alivyoeleza ni sawa sawa na tutafanya marekebisho, badala ya neno "wazawa" itakuwa kama ilivyosomeka katika Kiingereza.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Nashukuru Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Kifungu 6 Kazi za shirika pamoja na marekebisho yake

Kifungu 7 Uwezo wa shirika pamoja na marekebisho yake

Sehemu ya Tatu

Kuanzishwa kwa Bodi ya Wakurugenzi,
Kazi na Majukumu yake

Kifungu 8 Kuanzishwa kwa bodi pamoja na marekebisho yake

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Mwenyekiti, katika mswada huu nilizungumzia kwenye kifungu cha 8(f) ambacho kinasema kwamba wajumbe wasiozidi wawili. Katika mswada wa mwanzo ulisema kwamba wajumbe wasiozidi wawili, lakini katika marekebisho ikawa wajumbe wasiozidi watatu. Ingawa mbali na majibu ya Mhe. Waziri, lakini ningeomba tuendelee na ule mswada wa mwanzo ambao unasema; wajumbe wasiozidi wawili, badala ya watatu tumpe waziri wajumbe wawili, tusimpe watatu. Mimi napingana na hii ya wajumbe watatu.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: (Kny: Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo): Mhe. Mwenyekiti, tulisema hivyo kwamba wasiozidi watatu, lakini tulisema huyo mmoja anatokana na *NGO.* Kwa hivyo, tumeona kwamba tuiache vile vile, kwa sababu tunahitaji mjumbe kutoka *NGO.* Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Mwakilishi aniruhusu na aniachie hilo, ili tuweze kupanua wigo katika hii tasnia. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Nassor Salim Ali: Tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Mwenyekiti, ahsante wakati nilipokuwa nikichangia mswada huu nilipendekeza kifungu cha 8(2) kifutwe, ambapo Mwanasheria kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali yeye amteue mjumbe kwenda katika Bodi na mjumbe kutoka wizara inayohusika na mambo ya fedha, basi na mkuu wa taasisi hiyo naye ateue mjumbe ampeleke kwenye bodi badala ya hivi kifungu kilivyo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu bodi hii hivi sasa inaonekana ina wajumbe wanane, sasa ukiachia wajumbe wawili maana yake waliobakia wote wanatakiwa wateuliwe na Waziri. Sasa hapa waziri atakuwa na mamlaka makubwa mno juu ya uendeshaji.

Kwa hivyo, naomba hawa wateuliwe na taasisi inayohusika. Vile vile nilijaribu kupitia katika Maktaba yangu ya Sheria ambayo tunapitisha wengi wa wajumbe kama hawa tunaopitisha wanaoingia kwa nyadhifa zao wanapendekezwa katika taasisi zinazohusika badala ya kumuachia Waziri ateue.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kifungu hichi akitoe, ili tutoe nafasi katika ofisi hizi mbili ziweze kuteua watu kwa ajili ya kuwapeleka katika bodi, ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi (Kny: Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo): Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana nimesikia mawazo ya Mhe. Mjumbe na bila ya shaka yeye ameona upande wake na sisi tumeona upande mwengine, nimemuelewa hivyo kwa sababu kama nilivyosema awali kwamba mjumbe mmoja atoke Wizara ya Fedha na mwengine atoke *NGO's*.

Lakini kama mwenyewe anahisi kwamba labda hatokidhi hapa, basi naomba nimfafanulie zaidi kwa nini asiwepo huyu mtu, kwa sababu sisi tunahisi kwamba huyu mtu anahitajika miongoni mwa wajumbe hawa, kwa sababu kama hoja nzito basi sisi tunaweza kukubali.

Kwa hivyo, naomba ajaribu kuni-*convince* mpaka nione kweli hahitajiki. Kwa maana hiyo, naomba maelezo zaidi labda, ili niridhike na sisi tumeona hivi na tumefanya utafiti na sio kama tumeamua tu hapana, isipokuwa tumeangalia kwa upeo kabisa umuhimu wa kila sekta kuwepo hapo. Kwa hiyo, kama anayo hoja zaidi naomba maelezo.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Mwenyekiti, nadhani Mhe. Waziri hajanifahamu vizuri. Kwa kweli mimi sijasema kwamba hawa wajumbe wawili wasiwemo, ambao wameingia kwa nyadhifa zao, isipokuwa wajumbe hawa watoke moja kwa moja kwenye taasisi badala ya hii *statement* iliyokuwemo kwamba watateuliwa na Waziri.

Kwa hivyo, hawa watoke katika taasisi inayohusika na Afisi ya Mwanasheria Mkuu wajumbe wawili, ili waende kwenye bodi kama zilivyo sheria nyengine ambazo tunapitisha hapa na hiyo ndio *concern* yangu.

Mhe. Waziri wa Sheria na Katiba: Mhe. Mwenyekiti, ukitizama hichi kifungu cha 8 hakijasema kwamba waziri ndiye atakayeteua, lakini kinachosema ni kwamba kwenye hiyo bodi wajumbe hawa ndio watafanya hiyo bodi. Mhe. Mwenyekiti, naomba kunukuu.

Kifungu cha 8 kinaeleza hivi:-

"(a) Mwenyekiti, ambaye huyu atateuliwa na Rais;
(b) Mkurugenzi Mkuu wa Shirika ambaye ni mjumbe kwa wadhifa;
(c) Wakuu wa Idara ni wajumbe kwa nyadhifa zao;
(d) Mwanasheria wa Serikali kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali;"

Kwa hivyo, hapa haijasema kwamba waziri ndiye atakayemteua aa! Isipokuwa ni Mwanasheria wa Serikali kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu. Kwa maana hiyo, ni Afisi ya Mwanasheria Mkuu inayopeleka mwanasheria mmoja kuwa ni mjumbe wa bodi na wala si waziri ambaye anateua. Halikadhali na mjumbe mmoja kutoka Wizara inayohusika na mambo ya fedha na wala si waziri ambaye atateua, lakini Wizara ya Fedha ndio inapeleka mtu mmoja ambaye ndiye mjumbe wa bodi itakapoteuliwa.

Mhe. Mwenyekiti, lile suala la kusema kwamba waziri anayehusika ndiye anayeteua hapa halipo, hivyo waziri anapohusika ni kwenye kifungu 'f' peke yake na hapa ndipo ilipotajwa waziri hasa kwamba yeye ndiye atakayeteua hapa. Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri nadhani ulikuwa hujamfahamu Mhe. Mjumbe, kwa sababu Mhe. Mjumbe anasema kwamba kifungu cha 8(2) ndicho ambacho alichokuwa akikizungumzia na hichi kifungu cha 8(2) ninasema hivi.

Kifungu cha 8(2) kinaeleza hivi:-

> "Wajumbe waliotajwa chini ya kifungu kidogo (d) na (e) cha kifungu hichi watateuliwa na Waziri baada ya kushauriana na Mkuu wa taasisi husika".

Kwa kweli hicho ndicho tunachokijadili, Mhe. Waziri naomba utuongoze

Mhe. Waziri wa Sheria na Katiba: Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli ndivyo nilivyokusudia, lakini pengine kwa njia nyengine nilivyosema, kwa sababu hapa hateui Waziri, isipokuwa yeye waziri anapeleka kule taasisi inayohusika na halafu taasisi inayohusika ndio inayosema sisi mtu wetu atakuwa huyu.

Kwa hivyo, kikawaida kisheria sasa waziri anatangaza tu na wala si kama waziri ndiye anayetua aa! Afisi ya Mwanasheria Mkuu inapelekewa kwamba tunataka mtu mmoja, ili aingie kwenye bodi, kwa maana hiyo wao ndio wanapeleka na halafu waziri kwa ule utaratibu lazima ateuliwe. Lakini atateuliwa baada ya kupata jina kutoka kwa Mwanasheria Mkuu na yeyote atakayempeleka Mwanasheria Mkuu ndiye atakayetangazwa na waziri, ndivyo nilivyokusudia kwa misingi hiyo.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Mwenyekiti, kama hivyo ndivyo anavyozungumza Mhe. Waziri basi kifungu hichi kitoke kifungu cha 8(2), kwa sababu naomba kurudia Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu cha 8(2) kinaeleza hivi:-

"Wajumbe waliotajwa chini ya kifungu kidogo cha'd' na 'e' cha kifungu hichi watateuliwa na Waziri na hiyo ndiyo lugha iliyokuja baada ya kushauriana".

Mhe. Mwenyekiti, kama wakeshatajwa humu moja kwa moja, basi kifungu hichi kitoke kama zilivyo sheria nyengine, kwa sababu nimenukuu kwenye sheria nyengine ambapo wajumbe hawa huwa wanatoka kwenye zile taasisi moja kwa moja badala ya kuambiwa watateuliwa na waziri kwa kushauriana. Kwa hivyo, napendekeza kifungu hichi cha 8(2) kitoke.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, hebu kisaidieni kiti, kwa sababu mimi bado sijafahamu kimsingi, yaani *logic* hapa ni ipi kwamba ni kuchaguliwa kwao na waziri au kuna tatizo waziri atakapoletewa mtu atayeteuliwa labda atakuwa na mushkel, hebu nisaidieni hapo. Kwa hivyo, waziri ndiye atakayekuwa mtu wa mwisho wa kumaliza haya na hata kama ameteuliwa na taasisi yake au amependekezwa na jopo la watu kutoka eneo husika, lakini ndio jina lililoletwa.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, labda ni suala la uandishi tu, lakini turudi sisi kwenye Kanuni inasema kwamba bodi inawajibika kwa waziri ndio kanuni ya msingi. Kwa hiyo, kwa nini inawajibika kwa waziri, kwa sababu waziri kisheria ndiye ambaye anayeiteua na hawa wengine wanapendekeza hata kama hatokataa waziri mapendekezo yao, lakini yeye anabeba dhima kwa yale mapendekezo kuyakubali maana yake amewateua.

Kwa maana hiyo, hata kwenye hizo sheria nyengine ambazo Mhe. Salmin Awadh Salmin amezitaja ni kweli wakati mwengine inakuwa haiandikwi hivyo na inasemwa tu kwamba atatoka huko.

Mhe. Mwenyekiti, takriban bodi zote zinazoundwa sisi ndio waandishi wa yale matangazo ya kisheria ya uteuzi wa bodi, basi waziri ndiye ambaye ana-*sign* kama kuwateua wale, isipokuwa yule mjumbe ambaye ameteuliwa kwa nafasi yake. Sasa lile tangazo huwa linasema na hawa wataingia kwenye bodi kwa sababu ya nyadhifa zao. Lakini wale wote wanaopendekezwa basi mwenye kuteua ni Waziri.

Nadhani kinachopatikana inapatikana ile ku-*balance*, kwamba upande mmoja waziri ameshauriana na taasisi nyengine, lakini upande wa pili wale walioteuliwa wajue kuwa wanawajibika kwa waziri na hata hawa *ex officers or members* pia wanawajibika kwa waziri, na linapotokea tatizo kuhusiana na ujumbe wao, basi waziri anapaswa awaarifu ile mamlaka ambayo inahusika na uteuzi wake.

Kwa hivyo, nafikiri hii ni kanuni ya msingi katika uteuzi wa hizi bodi na wala sioni kama kuna tatizo kwenye kifungu hichi na hata kama kisiposema basi bado waziri ata-*sign* tangazo la kuteuliwa kwao, kwa sababu ndio utaratibu wa kisheria unavyotaka.

Mhe. Mwenyekiti: Kwa maana hiyo, kuwepo kwa kifungu hichi ni sawa na kutowepo ni sawa.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, hivi kilivyo ni vizuri zaidi kwa sababu kinaweka bayana zaidi hii Kanuni ambayo ipo ya Uteuzi wa Bodi.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Kifungu 8 Kuanzishwa kwa Bodi pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 9

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, wakati Mhe. Waziri alipokuwa akitoa ufafanuzi nilikuwa nikimsikia kupitia kwenye chombo cha habari kuanzia mwanzo mpaka naingia hapa nilikuwa nikienda naye sambamba. Kuhusu ufafanuzi kifungu cha 9(3), lakini kwanza kwenye kifungu cha 9(1) naomba kunukuu Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu cha 9(1) kinaeleza hivi:-

> "Bodi itamteua mtu mwenye taaluma katika fani ya sheria ya kiwango angalau shahada ya kwanza na uzoefu wa kazi usiopungua miaka miwili katika fani hiyo kuwa Katibu wa Bodi".

Lakini kwenye kifungu cha 9(3) naomba kunukuu Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu cha 9(3) kinaeleza hivi:-

> "Ikiwa Katibu hatokuwepo kutokana na ugonjwa au sababu nyengine yoyote hawezi kutekeleza majukumu yake. Bodi itateua mfanyakazi yeyote mwengine wa shirika kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya Katibu kwa muda ambao Katibu hatokuwepo mpaka nafasi yake itakapojazwa".

Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nikichangia nilielezea hisia zangu kwamba huyu Katibu ameteuliwa kwa sifa na hasa kutokana na uzito wa hichi chombo na katibu ndiye mwenye kazi kubwa sana kwenye bodi kama vile kuweka kumbukumbu pamoja na mambo mengine yote.

Kwa hivyo, pale anapokuwa hayupo shirika au bodi itamteua mfanyakazi yeyote, kwa hivyo unaposema yeyote hata kama hana sifa zinazokaribiana na za yule Katibu wa Bodi. Mhe. Mwenyekiti, wasi wasi wangu tunaweza kuja kumpa mtu kazi ambaye pengine atakosa sifa na umakini katika kutekeleza haya majukumu.

Sasa sijui Mhe. Waziri kama suala langu alilisikia na kuweza kulijadili pamoja na wasaidizi wake, kwa hiyo kidogo naomba nipate ufafanuzi na ikiwa sijaridhika nitatoa ushauri wangu katika hili. Mhe. Mwenyekiti, ahsante.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi (Kny: Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo): Mhe. Mwenyekiti, ahsante labda Mhe. Mjumbe wakati alipokuwa akifuatilia hotuba yangu bila ya shaka alikuwa akiendesha gari na pengine kipengele kile hajakisikia vizuri. Lakini nilieleza kwenye maelezo yangu kwamba atachaguliwa mtu mwengine mwenye sifa kama zake yule Katibu aliyeondoka. Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, kweli nilikuwa nikiendesha gari, tuendelee. *(Kicheko/Makofi)*

Kifungu 9 Katibu wa Bodi pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 10

Mhe. Panya Ali Abdalla: Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nikichangia kwenye kifungu cha 10 kuhusu kazi za bodi, ambapo moja wapo ilikuwa ni kuandaa na kusimamia Kanuni za Wafanyakazi, Kanuni za Fedha, Muundo wa Mishahara ya Wafanyakazi pamoja na maslahi yao.

Kwa kweli Mhe. Waziri alijibu lakini mimi sikusikia vizuri huku, kwa hiyo naomba ufafanuzi zaidi kwamba ni jinsi gani wataweza bodi hii ikishaundwa ijue kama ina dhima kubwa ya kuwasimamia wafanyakazi hawa waweze kupata maslahi yao kwa wakati kama inavyotakiwa.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri anihakikishie kama bodi yake hiyo itakuwa na uadilifu wa kuweza kuyafanya hayo. Mhe. Mwenyekiti, ahsante.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi (Kny: Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo): Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nikimjibu Mhe. Mjumbe labda hakunifahamu vizuri kuhusu kifungu cha 10 kazi za bodi Mhe. Mwenyekiti naomba kunukuu.

Kifungu 10(1) kinaeleza hivi:-

"Kazi za Bodi zitakuwa:-

(a) Kulishauri Shirika katika huduma za utangazaji;

(b) Kuandaa na kupitia sera …"

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri, kama hujamfahamu Mhe. Mjumbe basi ni vyema arejee.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi (Kny: Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo): Mhe. Mwenyekiti, labda arejee kifungu gani ambacho ana wasi wasi nacho pengine hajakifahamu vizuri, ili tuweze kufafanua zaidi.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, rudia tena, ili Mhe. Waziri aweze kukufahamu vizuri zaidi.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Mhe. Mwenyekiti, ahsante wakati nilipokuwa nikichangia juu ya hizi Kazi za Bodi kifungu cha 10(1) (d) naomba kunukuu Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu cha 10(1) (d) kinaeleza hivi:-

"Kuandaa na kusimamia kanuni za wafanyakazi, kanuni za fedha na muundo wa mishahara ya wafanyakazi pamoja na maslahi mengine;"

Mhe. Mwenyekiti, hili ni jambo muhimu sana ambalo linawakwaza sana wafanyakazi wetu mishahara yao pamoja na maposho yao mbali mbali wanachelewa kuyapata, na wakiyapata wanayapata pengine ni madogo.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kama yeye ndiye atakuwa ni msimamizi wa hii bodi, basi nilitaka alihakikishe hiyo kwamba bodi inafanya kazi zake vizuri

ya kuwasimamia wafanyakazi hawa, ili waweze kupata maslahi yao kama inavyotakiwa. Mhe. Mwenyekiti, ahsante.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi (Kny: Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo): Mhe. Mwenyekiti, ahsante nimemfahamu Mhe. Mjumbe na kama alivyoeleza basi tutatekeleza kama alivyosema kwamba Waziri ndiye msimamizi na kuhakikisha kwamba maslahi pamoja na ufanisi unapatikana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, ahsante Mhe. Waziri amekubali mapendekezo. Tunaendelea.

Kifungu 10 Kazi za Bodi.

Sehemu ya Nne

Uongozi na Wafanyakazi wa Shirika

Kifungu 11

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nikichangia nilitaka kidogo ufafanuzi au kama mapendekezo yangu yamekubalika marekebisho kwenye kifungu cha 11(3) naomba kunukuu Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu 11(3) kinaeleza hivi:-

> "Mkurugenzi Mkuu atakuwa ndiye Mtendaji Mkuu wa Shirika na atawajibika katika utekelezaji wa kazi za kila siku za Shirika".

Mhe. Mwenyekiti, nilihoji hapa kwamba atawajibika aidha kwa bodi, waziri au kwa nini na nilisema naomba nielezwe mantiki yake na kama ilikuwa imesahaulika basi iwekwe. Sasa kwenye majumuisho ya Mhe. Waziri na kwa bahati nzuri mimi nilikuwa siendeshi gari nadhani sikulifahamu vizuri, nadhani Mhe. Waziri atanisaidia. Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi (Kny: Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo): Mhe. Mwenyekiti, katika maelezo yangu nilieleza hapa kwamba Mhe. Ismail Jussa Ladhu alitaka kujua Mkurugenzi Mkuu atawajibika kwa nani, na mimi nilisema kwamba Mkurugenzi Mkuu atawajibika kwa bodi na kwa kuwa hali hiyo haijitokezi wazi wazi basi tutaifanya ionekane wazi wazi. Mhe. Mwenyekiti, ahsante.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru nadhani kutokana na ule usuhuba wangu na Mhe. Hamza Hassan Juma basi akiendesha gari yeye mpaka na mimi huwa naathirika. Kwa hivyo, ahsante sana nimepokea maelezo yake na naomba tuendelee. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, najua ndio tatizo la mapenzi mkipendana sana ukiendesha gari wewe basi na mwenzako anatikisika. Mhe. Mwenyekiti, kwenye kifungu cha 11 wakati nilipokuwa nikichangia kuna kifungu nilikipendekeza kitolewe kifungu cha 2(d) kifungu ambacho, ili nieleweke vizuri basi nitaomba ninukuu kuanzia kifungu cha 11(1), ili nipate kueleweka nilichokusudia.

Kifungu cha 11 kinaeleza hivi:-

"(1) Kutakuwa na Mkurugenzi wa Shirika ambaye atateuliwa na Rais.

(2) Mtu atakuwa na sifa za kuteuliwa kuwa Mkurugenzi Mkuu ikiwa atakuwa:-

(a) Amehitimu katika Chuo Kikuu kinachotambulika au kutoka Chuo kinacholingana na hicho na hichi nilipokuwa kwenye gari nilikisia vizuri na wala sina matatizo nacho.

(b) Mwenye uzoefu angalau katika moja au zaidi ya taaluma za mawasiliano ya habari, usimamizi wa biashara, habari na mawasiliano na utumishi wa umma, hili pia sina tatizo nalo.

(c) Mwenye uzoefu na maarifa ya kutosha katika sekta ya utangazaji na

(d) Sifa nyengine yoyote kama itakavyoamuliwa na Rais.

Mhe. Mwenyekiti, nadhani ni kweli huwa tunapendekeza kwamba Rais tumpunguzie majukumu na hapa Mhe. Rais ameekewa vigezo vya kumteua huyu Mkurugenzi Mkuu. Lakini hichi kifungu cha 'd' sawa sawa kwamba kinafuta yale mapendekezo yote ya zile sifa za mwanzo zilizotajwa, maana yake unaposema (d) au sifa nyengine yoyote kama itakavyoamuliwa na Rais.

Kwa hivyo, inawezekana haya ya huku juu yote hatoweza kuyaangalia kwa sababu hii sheria tumempa nafasi ya kuangalia mtu mwengine yeyote ambaye pengine hata hizi sifa za huku juu hana, kwa hiyo labda nipewe maelezo ya ufafanuzi wa kisheria zaidi ili niweze kuelewa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu kifungu kimoja kinazuiliwa mara tatu, basi nitaomba nipate tena ufafanuzi kwenye kifungu hichi cha 11(4), ambapo naomba kunukuu Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu cha 11(4) kinaeleza hivi:-

"Mkurugenzi Mkuu atateuliwa kwa kipindi cha miaka mitano na kutokana na utendaji wake bora wa kuridhisha anaweza kuteuliwa tena katika kipindi chengine cha miaka mitano".

Sasa hapa nilipendekeza kwa sababu hii Mamlaka ya uteuzi ni ya Mhe. Rais mwenyewe na huyu Mkurugenzi sio kama anateuliwa Mkurugenzi kwa madhumuni ya kuundwa bodi, isipokuwa huyu Mkurugenzi moja kwa moja anakuwa ni Mkurugenzi Mtendaji.

Kwa hivyo, tunaposema atateuliwa na kufanya kazi kwa kipindi cha miaka mitano na baadaye kama amefanya kazi vizuri atateuliwa miaka mitano mingine. Kwa maana hiyo, ndani ya vipindi viwili atakuwa tayari ameshamaliza ule muda wake. Mhe. Mwenyekiti, inawezekana pengine kutokana na ufanisi wake mzuri Mhe. Rais akaja akashindwa kumteua katika kipindi cha tatu, kwa sababu tayari sheria imeshasema atateuliwa kwa kipindi cha miaka mitano na baadaye atateuliwa kipindi cha miaka mitano mingine.

Kwa kweli kwenye mambo haya ya habari uzoefu pamoja na taaluma ni vitu ambavyo vinasaidia sana, sasa Mkurugenzi akikaa miaka mitano, baadaye miaka mitano mingine atakuwa tayari lile shirika au taasisi anayoiongoza anaijua kama pesa. Mhe. Mwenyekiti, ikiwa kuna kikwazo cha kuteuliwa vipindi viwili basi kipindi cha tatu atakuja kushindwa kuteuliwa.

Nadhani hakuna haja ya kumuwekea kipindi cha uteuzi Mkurugenzi, isipokuwa ateuliwe tu na Mhe. Rais basi atakapoona anahisi kuteua mtu mwengine wakati wowote anaweza kumteua mtu mwengine au anahisi anaweza kuendelea kama wanavyoendelea wakurugenzi wengine, kwa hivyo vifungu hivyo viwili naomba ufafanuzi.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Hamza Hassan Juma, huoni kwamba hicho kifungu cha'd' ndicho kinachosababisha hiyo sifa nyengine umeihifadhi, ambayo Rais huyu ataona kwamba huyu aendelee tena, lakini zaidi Mhe. Waziri atatusaidia.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi (Kny: Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo): Mhe. Mwenyekiti, labda nije kwenye suala la kikomo cha Mkurugenzi Mkuu na nilieleza hapa kwamba wizara inaona kifungu hichi kiendelee kuwepo kwa sababu gani. Kwa kweli wizara inaona kuwepo kwa kifungu hichi kwanza kutaondoa uwezekano wa mtu kujijengea ufalme wa kujijengea himaya katika uongozi wa nafasi kama hii, kwani kile Mkurugenzi atakayeteuliwa bila ya shaka atalazimika kufanya kazi hiyo kwa mkataba maalum wa kuitetea serikali pamoja na kuleta tija.

Kwa hivyo, tumeona kwamba kifungu hichi kibakie, kwa sababu kusema tu Rais aachiwe tu, tunahisi kwamba bado itakuwa Mkurugenzi yule, kwa sababu yeye anajua. Kwa maana hiyo, kwanza sisi tutakwenda kibiashara na anajielewa kwamba kama nikivuruga hapa, basi kipindi kijacho mimi sipo. Kwa hiyo, yeye ameshajua kwamba lazima afanye kazi kuhakikisha kwamba shirika linaleta tija, ili kipindi kijacho Rais aweze kumteua tena.

Kutokana na hali hiyo, ndio tumeona ibaki hivyo, ili tuone ule ushindani wa Mkurugenzi yule unaonekana kuliko vile Mhe. Mjumbe anavyopendekeza yeye nahisi kidogo itakuwa mushkeli.

Mhe. Mwenyekiti, wakati huo huo Mhe. Mjumbe amesema kuhusu kifungu cha 11(d) sifa nyengine yoyote kama itakavyoamuliwa na Rais. Kwa hivyo, tunaweza kuondoa na itakavyoamuliwa na Rais ibakie na sifa nyengine yoyote na hiyo nakubali. Lakini kwa lile ambalo nimelizungumza mwanzo naomba libakie vile vile, ili tuone kwamba kuna ushindani wa Mkurugenzi Mkuu. Mhe. Mwenyekiti, ahsante.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nadhani kama ingelikuwa hii nafasi imetangazwa, basi ingelikuwa ni busara kuweka kipindi, lakini hii nafasi ya Ukurugenzi haikutangazwa. Kwa mfano, hivi sasa Bara tayari wameshaanza utaratibu wa hizi bodi kwamba watu wanakuwa wanaomba wenye sifa, kwa hiyo ina maana hizi mtu anapoomba bila ya shaka kuna *conditions* pamoja na mikataba.

Lakini mimi bado sijaona umuhimu wa nafasi ya Mkurugenzi ambayo moja kwa moja ni mamlaka ya Rais ya uteuzi kumuwekea hivi vipindi, kwa sababu kama alivyosema Mhe. Waziri,

kwamba mtu atajitahidi afanye kazi vizuri asiharibu, ili Mhe. Rais kipindi chengine amteue tena, sawa ameshafanyakazi vizuri miaka mitano, pia amefanya kazi miaka mitano ya pili.

Sasa Rais ameridhika na utendaji wake wa kazi katika vipindi vyote viwili anataka kumpa tena kuendelea kuongoza hili shirika. Lakini sasa tayari kuna *limitation* kwamba vipindi viwili tayari na wala hapa hatuoni kama Mhe. Rais tunamnyima nafasi ya kuendelea kumteua huyu mtu ambaye tayari ile taasisi ameshaiboresha na anahisi aiendeleze kwa kumuwekea vipindi hivi viwili.

Kwa hivyo, nadhani Mhe. Waziri anikubalie kwamba Mkurugenzi atateuliwa na Mhe. Waziri, bora wangelisema kipindi cha miaka mitano mitano. Lakini unaposema kwamba anaweza kuteuliwa tena katika kipindi cha miaka mitano, ina maana sawa sawa kama tumeweka vipindi viwili.

Mhe. Mwenyekiti, bora ingekuwa anaweza kuteuliwa tena katika kipindi cha miaka mitano mitano, yaani inaweza kuwa mitano, mitano, mitano, mitano, mitano na kuliko kuweka tu kipindi fulani, kwa sababu hapa wakati mwengine tunaweza kumnyima Rais kumpa nafasi mtu ambaye tayari ameshaiboresha sana hii taasisi.
Kwa maana hiyo, pengine mimi ni mwanasheria wa zamani hasa kule Chuo Kikuu cha Kwamtipura, naomba kupata ufafanuzi zaidi ili niweze kuridhika.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Hamza Hassan, kwa mujibu wa mapendekezo ya Kamati, kamati walipendekeza kifungu hichi kifutwe kabisa. Sasa sijui Mhe. Waziri atatuelekeza nini katika hili. Hiki kifungu cha 4, Mhe. Waziri tupe muuongozo katika hili.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi (Kny Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo): Ahsante Mhe. Mwenyekiti, umeeleza, umenisaidia kwamba Kamati imependekeza hivyo. Lakini pamoja na kwamba kamati ilipendekeza naona hakuna haja ya kuvutana sana kwa sababu huu ni uteuzi wa mwenyewe Mhe. Rais, kwa hivyo sina hoja kubwa tunaweza tukamuachia Mhe. Rais mwenyewe akaamua anavyohisi. Ingekuwa ni uteuzi wetu labda tungeweza kuamua lakini ni uteuzi wa Rais, kwa hivyo wacha tumpe mamlaka yake ataamua mwenyewe anavyotaka.
Mhe. Mwenyekiti: Tunachohitaji Mhe. Waziri, tupate kumbukumbu sahihi kwenye Hansard zetu na huu Mswada wetu tunaokwenda nao. Tusaidie tufanye nini katika hili. Kwa sababu Rais, ndio Rais, yupo yeye. Lakini haya masuala ya utendaji tunayosisi hapa. Tusaidie zaidi Mheshimiwa.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi (Kny Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo): Nilichokusudia kusema kwamba tumuachie Mhe. Rais ateuwe katika kipindi cha miaka mitano mitano, mpaka mwenyewe anapohisi kwamba huyu tena basi.

Kifungu 11 Mkurugenzi Mkuu Pamoja na Marekebisho Yake
Kifungu 12 Uanzishwaji wa Idara Pamoja na Marekebisho Yake
Kifungu 13 Wafanyakazi wa Shirika Pamoja na Marekebisho Yake

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia hoja iliyombele yetu nilizungumzia juu ya kifungu hiki cha 13 kilichoongezwa na Mwenyekiti, ambacho chenye

maneno ya pembeni "Uwezo wa Waziri" na kukawa na kifungu cha 13(a), (2), (3) (a), (b), (c). Katika maelezo yangu Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nna wasi wasi juu ya uwezo wa Mhe. Waziri na maelezo ambayo yametolewa.

Katika maelezo yangu nilitoa mfano wa wizara kuyaingilia mashirika juu ya uwezo ambao unapewa. Juu ya wasi wasi wangu juu ya uwezo huo wa Mhe. Waziri ambao umetajwa hapa. Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko alipokuwa akichangia alitoa maelezo kinyume na maelezo ambayo niliyatoa. Kwamba nimelipotosha Baraza.

Hoja yangu sio kulipotosha Baraza, hoja yangu ni juu ya Hoja iliyoko mbele yangu na nilitoa mfano tu juu ya fedha ambazo zimepotea. Nikasema kwamba mambo haya yanapoweza kufanikiwa yanakuwa ni ya wote lakini yanapoharibika inaachiwa Bodi au mkurugenzi. Na ndio kama vile nilivyosema ilivyotokea, kwamba wamefanya kwa nia nzuri lakini matokeo yake limeharibika suala sasa limekuwa la mtu mmoja au la bodi.

Nikaonesha wasi wasi kwamba uwezo huo wa Waziri ulioelezwa hapa pengine unaweza ukawa hauna matatizo lakini sura inayoonekana hapa ni uwezo mkubwa. Nikamuomba Mhe. Waziri *at least* basi lugha iweze kubadilika na kuandikwa vyenginevyo. Nilitegemea Mhe. Waziri badala ya lugha hii iliyotumika katika kifungu cha 13 (1) basi labda angebadilisha lakini pengine hakuwa na lugha nyengine.

Sasa nipendekeze kwa Mhe. Waziri lugha ambayo inaweza kuwa sawa na hii kuliko haya maelezo yaliyopo, kwamba ielezwe kwamba Bodi itawajibika kwa Mhe. Waziri kuliko haya maelezo yaliyopo. Naomba Mhe. Waziri anikubalie kwamba ieleze *statement* hii kwamba 'Bodi itawajibika kwa Mhe. Waziri' kuliko haya maelezo yaliyoandikwa hapa.

Mhe. Mwenyekiti: Kwa msingi huu unapendekeza kwamba haya maneno yanayosomeka "Shirika linaweza kuajiri wafanyakazi wengine kama vile Bodi itakavyoamua kwa kuzingatia masharti ya Utumishi wa Wafanyakazi". Sasa yakae maneno hayo unayoyazungumza.

Mhe. Salmin Awadh Salmini: Mhe. Mwenyekiti, nipo kwenye karatasi ya marekebisho.

Mhe. Mwenyekiti: Hii tuliyokuwa nayo sisi haina marekebisho ya kifungu cha 13

Mhe. Salmin Awadh Salmini: Ehee! Hayakukubaliwa! Mhe. Mwenyekiti, kwenye marekebisho au pengine Mhe. Waziri hakuyakubali, kuna kifungu cha 13 kimeongezwa. Ukiangalia kwenye marekebisho ya Mhe. Waziri kuna kifungu kimeongezwa, labda pengine Mhe. Waziri anieleze kwamba kifungu hichi kilichoongezwa labda hakikukubalika, Kuna kifungu kimeongezwa cha (a), (b) na (c) kimeongezwa badala ya kifungu hichi kilichopo. Kama maelekezo haya hayakukubalika naiondosha hoja yangu.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi (Kny Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo): Samahani Mhe. Mwenyekiti, naona hicho kifungu anachosema mimi sikioni humu. Kwenye marekebisho yangu.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri, kwa muongozo wa Katibu hapa anatuelekeza kwamba hayo mapendekezo ni mapendekezo ya Kamati, iko karatasi mbali, halafu kuna mapendekezo ya jadweli iko kwenye *document* nyengine. Tukisha tuna Mswada wenyewe kurasa 296. Sasa sijui haya mapendekezo ya Kamati uliyachukua au uliyawacha, hatujafahamu hapo. Tunaomba muongozo wako.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi (Kny Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo): Mapendekezo ya Kamati baadhi tuliyachukua na mengine tumeyawacha na tulitoa sababu zetu kwa nini tuliyawacha.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, naomba nisaidie kidogo kidogo maana naona tunachelewesha Baraza bila ya sababu ya msingi.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nadhani kiutaratibu tunapopitisha vifungu tunafata Mswada ambao tunao katika gazeti la Serikali. Kwa hivyo hicho kifungu cha 13 anachokisema Mhe. Mjumbe hizi ni *serial numbers* ambazo Kamati imeorodhesha mapendekezo yake au marekebisho yake. Lakini tunapopitisha vifungu hatufati haya tunafata vile ambavyo vimo humu. Nafikiri ndio maana tunapoanza hapa unatwambia kwamba tunatumia gazeti rasmi la serikali ukurasa kadhaa kwa hivyo tunakuwa tunakwenda na vifungu hivi.

Sasa kilichokuwepo ni sahihi kinachoelezwa kwamba tuna waraka wa marekebisho ya Kamati ambayo bila ya shaka kwa yale ambayo Waziri hakutoa kauli ya kuyakataa pale maana yake inachukuliwa kwamba imekubalika. Inamaana unapotuhoji na marekebisho yake ufahamu wetu kwamba pamoja na haya.

Lakini vile vile kwa yale ambayo serikali ilikuwa na mawazo tofauti tupeleke jadweli la marekebisho ambalo limetolewa kwa mujibu wa Kanuni na imetejwa pale kanuni na ndio utaratibu wa Mabunge yote ya Jumuiya ya Madola. Kwa hivyo nadhani tukisoma vifungu unavyotuhoji ni hivi ambavyo zimo ndani ya Mswada ambavyo vimo ndani ya gazeti rasmi la serikali, lakini unatakiwa mjumbe uwe *alert* kila moja kwamba una–*refer* kwa yale ambayo yameletwa na Kamati na kama kuna ya ziada kama haya na tuzowee. Maana iko siku unaweza *amendment* hata mia humu maana yake unaweza ukaona mjumbe kila mmoja akaleta yake, ndio utaratibu wa kutunga sheria.

Kwa hivyo nadhani tunafuata vifungu hivi Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo kifungu cha 13 kinachozungumzwa hapa ni kile ambacho kiko katika Mswada na nadhani kifungu anachokizungumzia Mhe. Mjumbe hiki kinahusu kifungu cha 19. Kwa hivyo nadhani mawazo yake anaweza akayatoa atakapofika kifungu cha 19. Naomba tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi (Kny Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo): Mhe. Mwenyekiti, labda Mjumbe zaidi wasi wasi mkubwa ilikuwa ni kusema madaraka ya Mhe. Waziri kamba yalikuwa makubwa mno. Sisi tukasema kwamba hapana madaraka yabakie kama yalivyo kwa kuzingatia kwamba Waziri ndio kiungo kikubwa baina ya Baraza na Wizara. Na yeye ndiye mas-ul mkubwa atakaekuja kuulizwa baadaye, haulizwi Mkurugenzi Mkuu na tumeona mifano kadhaa wa kadhaa kwenye makosa ambayo yamefanywa kwenye mashirika mbali mbali lakini aliyekuja kuitwa hapa ni Mhe. Waziri, hakuita Mkurugenzi Mkuu wala nani.

Huu ni wajibu wa Waziri wote na *paper* tumeipitisha Shirika la juzi tu la mambo ya masuala ya meli na utakuta takriban ndio yale na tumeyakubali bila ya matatizo. Kwa hivyo mimi nahisi Mhe. Mjumbe aachie madaraka ya Mhe. Waziri ili awajibike vizuri katika shirika au katika Wizara kwa ujumla kwa sababu yeye ndiye atakaekuja kusumbuliwa hasumbuliwi mtu mwengine. Kwa hivyo ili kukinga haya asijeakasumbuliwa bila ya makosa basi tumhusishe na lile shirika ingawaje litakuwa lipo huru lakini na yeye atakuwa na mkono wake ili kushauriana nao ili kuhakikisha kwamba lile shirika linakwenda vizuri. Hilo tu Mhe. Mwenyekiti ahsante.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa maelezo ya Mhe. Waziri inaonekana mabadiliko haya yaliyofanywa na Kamati yamekubalika kuongeza kifungu cha 13 (1) (a), (b), (c).

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Kifungu cha 13 au cha 19 kwa sababu haya maelezo yanayozungumzwa yanahusu kifungu cha 19 Mhe. Mwenyekiti, tumetanabahisha hapa. Kifungu cha 13 umetusomea hapa kinahusu wafanyakazi wa Shirika. Sasa nadhani tuendelee na utaratibu kwamba yakifika haya maelezo ya kifungu cha 19, kila mwenye hoja yake atazungumza wakati huo. Naomba sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, suala la Uwezo wa Waziri nadhani umesungumzwa vizuri na ukiangalia hii *schedule of amendment* ilivyotolewa imeelezea kuhusu kifungu kinachopendekezwa kuhusiana na uwezo wa Waziri ambacho kama anavyosema Mhe. Ismail Jussa kwamba kipo chini ya kifungu cha 19. Kwa hivyo mimi nadhani kama kuna hoja yoyote kuhusiana na uwezo wa Waziri nadhani tusubiri katika kile kifungu cha 19 yaani kama kuna marekebisho ya Kamati basi nadhani yalikosewa katika namba. Sasa hivi tuje tuyajadili katika kifungu cha 19, lakini hapa ni kuhusiana na *immunity* au kinga ya wafanyakazi inayohusiana na suala la Waziri.

Kifungu cha 13 Wafanyakazi wa Shirika Pamoja na Marekebisho Yake

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, mimi hapa sina jambo kubwa isipokuwa nilipendekeza nilipokuwa nikichangia kuhusu wafanyakazi wa Shirika kwamba Shirika linaweza kuajiri wafanyakazi wengi kama vile bodi itakavyoamua kwa kuzingatia masharti ya utumishi wa wafanyakazi.

Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia sehemu hii nilizungumzia sana suala la wenzetu wenye ulemavu wa masikio wanavyokosa taarifa muhimu. Wenzetu wenye ulemavu wa macho wanasikia matukio kupitia kwenye vyombo vya habari. Lakini wenzetu wenye upungufu wa usikivu kwenye masikio wanakosa sana habari. Zanzibar katika nchi za Afrika Mashariki Zanzibar sisi ndio tulikuwa wa mwanzo kuanzisha mpaka Sheria ya Watu Wenye Ulemavu. Mkurungezi Mkuu wa Walemavu Zanzibar alikwenda kutoa semina kubwa sana katika nchi za Afrika Mashariki katika Masuala mazima ya ulemavu. Na tulisifiwa katika vikao vya Afrika Mashariki kwamba Zanzibar ni nchi ambayo imepiga hatua sana katika kuunda Sheria ya Watu Wenye Ulemavu.

Bado katika vyombo vya habari wenzetu hawa wenye ulemavu wa masikio bado wanakosa taarifa muhimu. Sasa hivi serikali yetu tunaishukuru sana, kumeanzishwa shule nyingi ambazo elimu mjumuisho. Ndugu zetu hawa wanapata taaluma na tena wana ufahamu mzuri sana. Lakini

pia Wizara yako ya Habari Mhe. Mwenyekiti, katika michezo imewapa nafasi kubwa sana walemavu tena hawa walemavu ambao hawasiki. Hata juzi katika sherehe pale Uwanja wa Amani katika siku ya kukabidhi mipira walikuwepo, tena sasa hivi wapo wengi kweli kweli, wanazungumza pale katika lugha zao kwa kweli ingawa hujisikii raha kwasababu ule ni ulemavu lakini unaona namna gani wanavyohitaji na wao taaluma.

Nilipendekeza tunapokuwa katika Vikao vya Baraza wawepo watu wenye lugha ya alama, jana walikuwepo leo hawapo. Kwa hivyo ina maana hawa bado wanafanya kazi katika kubahatisha. Kwa hivyo napendekeza kwa kuwa hapa Shirika tunalianzisha na unalipa mamlaka ya kuajiri wafanyakazi kama bodi itakavyoaamua basi mimi nadhani suala la watu wakalimani wa lugha ya alama wazingatiwe vya kutosha Mhe. Mwenyekiti. Huo ulikuwa ni ushauri wangu.
Kifungu 13 Wafanyakazi wa Shirika Pamoja na Marekebisho Yake

Sehemu ya Tano

Masharti ya Fedha

Kifungu 14 Fedha na Rasilimali za Shirika
Kifungu 15 Matumizi Pamoja na Bajeti Pamoja na Marekebisho Yake
Kifungu 16 Hesabu na Ukaguzi
Kifungu 17 Manunuzi
Kifungu 18 Sera za Uhariri Pamoja na Marekebisho Yake
Kifungu 19 Uwezo wa Kutunga Kanuni Pamoja na Marekebisho Yake
Kifungu 20 Kufuta na Kubakisha

Jadweli
Muda na Utumishi wa Vikao vya Bodi Chini ya Kifungu cha 8 (4)

Kifungu 1 Muda wa Utumishi wa Mjumbe wa Bodi
Kifungu 2 Kutohudhuria Vikao
Kifungu 3 Vikao vya Bodi
Kifungu 4 Mgongano wa Maslahi
Kifungu 5 Akidi Pamoja na Marekebisho Yake

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nataka nikiri kwanza kwa sababu si kawaida yangu huwa sipendi kurukia mambo. Kwamba sikukichangia kifungu hiki mahsusi katika jadweli lakini katika marekebisho yaliyoletwa hapa nilikubaliana na mapandekezo ya marekebisho ya muundo wa bodi. Nilichokigundua hapa nimeona Baraza lisijelikafikishwa pahala likafanya maamuzi ambayo yanaweza yakaja yakaathiri misingi ya uwajibikaji. Ukitizama kifungu cha 5 na cha 6 naomba tukisome kwa pamoja kinachozungumzia akili na uwamuzi wa Bodi.
Kifungu cha 5 kinazungumzia uwamuzi wa kikao utafanywa kwa wingi wa kura za wajumbe waliohudhuria na kupiga kura.

Kifungu cha 6 kinasema wajumbe wane watafanya akidi ya kikao cha Bodi na katika marekebisho haya hayakuzingatiwa. Wanne katika 7 waliokuwa mwanzo katika Mswada kama

ulivyokuwa awali ndio *majority* kwa sababu walikuwa 7. Lakini sasa baada ya kumba ni 8 na imepitishwa hapa, wane wanakuwa ni nusu yao tu. Sasa nilikuwa naomba vyote hivi cha 5 na cha 6 vizingatia hilo ama iwe zaidi ya nusu ama tuseme angalau watano kwa maana ya kuonesha kwamba ni zaidi ya nusu. Nilikuwa nataka tulirekebisho hilo tu.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi (Kny Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo): Naomba nikubaliana na Mhe. Mjumbe yaani zaidi ya nusu.

Kifungu 5 Akidi Pamoja na Marekebisho Yake
Kifungu 6 Uwamuzi wa Bodi Pamoja na Marekebisho Yake
Kifungu 7

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, Kifungu cha 7 (2) nilimuomba Mhe. Waziri kuhusu vikao vya Bodi kwamba uwamuzi wa Bodi unaweza kufanywa bila ya kikao kwa kusambaza nyaraka zinazohusika kwa wajumbe na maamuzi ya wajumbe waliowengi husika. Nikamshauri Mhe. Waziri kwamba tuondoshe kwa sababu tumeweka muda wa kutosha kwa vikao vya Kamati na vile tunawaachia Bodi wanaweza wakafanya vikao vya dharura pale vinapohitajika. Na hata Kamati kifungu cha 7(2) walikubaliana kwamba kifungu hiki kiondoke maana yake ni kwamba tusitoe maamuzi kwa njia ya nyaraka bali tuwaachie Bodi wafanye vikao na hasa kwa vile vikao vimewekwa vya kutosha kwenye sheria.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi (Kny Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo): Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na mawazo ya mjumbe kwamba Kikao cha Bodi kifanye maamuzi. Ahsante.

Kifungu 7 Pamoja na Marekebisho Yake
Kifungu 8 Mwenendo wa Vikao vya Bodi
Kifungu 9 Posho la Bodi

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 9 kuna wajumbe wa Bodi watalipwa posho ada na malipo mengine kwa ajili ya kujikimu kama itakavyoamuliwa na Waziri. Nikapendekeza kwamba tusiwapangie matumizi ya fedha watakayolipwa. Tuseme tu Wajumbe wa Bodi watalipwa posho kwa mujibu wa vikao kama ambavyo Waziri ataamua, ili tusilazimishe kwamba pesa hiyo ya kujikimu pengine, nauli, malazi, tusiwatafsirie kwamba nja posho, tuweke wazi kwa mujibu wa sheria kwamba wajumbe wa Bodi walipwe posho kama ilivyotanguliwa na Waziri na hivyo ndivyo ilivyo katika Mishwada mingi au sheria nyingi za Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi (Kny Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo): Ahsante nakubaliana nae.

Kifungu 9 Posho la Bodi
Kifungu 10 Kamati za Bodi
Kifungu 11 Mkutano Mkuu wa Mwaka…

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nimeelimishwa hapa na jirani yangu, kwa sababu hoja yangu ilikuwa ni kwamba kifungu cha 11 kwamba tuweke Mkutano Mkuu wa Bodi na

Wizara nikasema kwamba hakuna haja kwa sababu ni mambo ya ndani. Lakini kama kimefutwa kwa mujibu ya mapendekezo ya Kamati basi naunga mkono hilo. Kama hakijafutwa basi tuondoshe kifungu cha 11 kwa sababu hakuna haja ya kutoa kwenye Sheria kwamba Bodi na Wizara ifanye Mkutano Mkuu kwa Kila mwaka. Naomba tukubaliane kwamba tukifute kwa mapendekezo ya Kamati ilivyopendekeza.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi (Kny Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo): Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nimejaribu kuangalia, sawa nakubaliana nae mapendekezo yake kwamba kinafutwa.

Kifungu 11 Mkutano Mkuu wa Mwaka Pamoja na Marekebisho Yake.

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi (Kny Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo): Mhe. Mwenyekiti, ilivyokuwa Kamati ya Kutunga Sheria imeupitia Mswada wangu kifungu baada ya kifungu na kuukubali pamoja na marekebisho yake. Sasa naliomba Baraza lako tukufu liukubali. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mswada wa Sheria wa Shirika la Utangazaji la Zanzibar Mwaka 2012

(Kusomwa kwa mara ya Tatu)

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi (Kny Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo): Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kuwa Mswada wa Sheria la Shirika la Utangazaji la Zanzibar Mwaka 2012, usomwe mara ya tatu. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafiikiwa)

(Mswada wa Sheria ya Serikali ulisomwa mara ya tatu na kupitishwa)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe kwa kuwa kazi tuliyokuwa tumeifanya hapa ni kubwa sana na ni nzito na kwa kuwa muda wa kuendelea na shughuli zetu bado ungalipo. Kuna taarifa ya kuja kusomwa ripoti ambayo itakuwa ni refu sana. Nimemuuliza hapa muhusika mwenyewe anasema akipewa muda mdogo basi angalau saa moja au moja na nusu ndipo amalize na muda wetu utakuwa haukubali hivyo.

Sasa nafikiria tumuombe Mhe. Waziri katika Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais ili tuweze kuweka Kanuni kando tuweze kutumia muda huu ili tuweze kuakhirisha Baraza hili hadi kesho asubuhi saa: 3:00 tuendelee na shughuli zetu.

KUAHIRISHA BARAZA KABLA YA WAKATI WAKE

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti na Waheshimiwa Wajumbe kama ilivyoelezwa muda uliobakia hautoshi kwa Mhe. Mwenyekiti kuweza kuwasilisha ripoti yake hii leo. Hivyo Mhe. Mwenyekiti, naliomba Baraza lako tuweke kando muda ili uweze kuliakhirisha Baraza mpaka kesho asubuhi saa 3:00.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafiikiwa)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsanteni sana Waheshimiwa Wajumbe kwa mashirikiano ambayo mliyokuwa mkinipa kuweza kufanya kazi hii na kuwa nyepesi kabisa. Sasa nachukua fursa hii kuakhirisha Baraza hili hadi kesho tarehe 24/01/2013 saa 3:00 za asubuhi.

(Baraza liliakhirishwa saa 1:15 hadi tarehe 24/01/2013 saa 3:00asubuhi)